Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Nne – Tarehe 30 Januari, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 39

**Mtiririko wa Mikutano ya Bunge**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa mkutano wa Bunge wa Kumi na mbili (12) umeisha hivi kairbuni:-

(a) Je, Mkutano huo ni wa Bunge la ngapi tokea kuanza kwa Bunge la Tanzania?

(b) Je, Mtiririko wa Bunge la Tanzania ukoje tokea kuanza kwake hadi kufikia Bunge hili ?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mkutano wa 12 wa Bunge uliokwisha ni wa Bunge la Tisa (9) tangu kuanza kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Bunge la kwanza la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilianza mwaka 1965 baada ya Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya watu wa Zanzibar. Ikumbukwe kwamba Bunge la iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika ilidumu kwa muda mfupi sana.

Kwa mujibu wa Ibara ya 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, toleo la 2005, maisha ya Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania ni muda wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Ibara ya 65, mtiririko wa maisha ya Bunge umekuwa kama ifuatavyo:-

Mwaka 1965 – 1970 Bunge la Kwanza, 1970 – 1975 Bunge la Pili, 1975 -1980 Bunge la Tatu, 1980 – 1985 Bunge la Nne, 1985 – 1990 Bunge la Tano, 1990 – 1995 Bunge la Sita, 1995 – 2000 Bunge la Saba, 2000 – 2005 Bunge la Nane, 2005 – 2010 Bunge la Tisa.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI :** Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba Bunge lina umri wa miaka mitano kila Bunge lakini mkutano huu ni wa kumi na nne. Sasa sijui hapa kutofautisha kati ya hii Bunge na mkutano kwa sababu ikiwa tano mara 14 ni idadi zaidi sasa ni kitu gani kilicho au sababu gani zilizosababisha kwamba huu uwe mkutano wa 14 lakini Bunge la Tisa panatofauti gani hapa kati ya Mkutano huu na hili Bunge ?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza tuanze na kikao, hiki sasa hivi tulichonacho ni kikao cha mkutano wa Bunge la Tisa, Bunge moja linakuwa na mikutano 20 na kila mkutano inakuwa na vikao vingi iwezekanavyo kutegemeana na siku ambazo zimepangwa mkutano wa Bunge kufanyika. Kwa hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 65 ya Katiba Bunge lina maisha ya miaka mitano kila Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lina muda wa kuishi miaka mitano baada ya pale kunakuwa na uchaguzi na kunakuwa na Bunge lingine. Sasa Bunge huwa linafanya mikutano kila wakati na mkutano mmoja huwa na vikao mbalimbali vinavyoanza Jumanne kwa kawaida hadi Ijumaa.

**SPIKA:** Kwa faida ya Dr. Haji na wengine suala hili liko wazi kabisa katika Kanuni ya tatu ufafanuzi wa maneno mbalimbali kikao cha Bunge. Kikao cha Bunge ni kikao cha siku moja kinachoanza kwa kusomwa Dua na kumalizika kwa Kuahirisha Bunge hadi siku inayotajwa. Hicho ndicho kikao. Sasa mkutano wa Bunge ni mfululizo wa vile vikao, mfululizo wa vikao vya Bunge kuanzia kikao cha kwanza hadi cha mwisho. Bunge lenyewe sasa ndiyo hilo lenye uhai wa miaka mitano yote yamo humu kwenye Kanuni ya tatu.

Na. 40

**Maombi ya Kusajili Vijiji kwa Ajili ya Huduma Muhimu**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali hupeleka huduma muhimu kwenye maeneo ya vijiji vilivyosajiliwa; na kwa kuwa, maombi ya kuvisajili vitongoji vya Kigina na Magarama vilivyoko Kata ya Rugongwe Wilayani Kibondo vyenye zaidi ya wakazi 5,000 ili viwe vijiji yalishapelekewa TAMISEMI tangu mwaka 2003:-

Je, Serikali inawaambia nini wananchi hawa wanaoishi bila huduma muhimu kama maji Zahanati na Barabara kwa muda mrefu sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ilipokea na kufanyia kazi maombi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya kusajili vijiji vipya vya Kigina na Magarama.

Maombi kama hayo pia yalipokelwa kutoka Halmashauri mbalimbali nchini. Kutokana na taarifa za maombi hayo kuwasilishwa pasipo kumbukumbu muhimu kama mihtasari ya vikao vya Baraza la Madiwani la Halmashauri; maombi mengi hayakufanyiwa kazi kwani Mihtasari ya vikao hivyo ndiyo inayothibitisha uamuzi halali wa Halmashauri kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya mwaka 1982.

Kutokana na upungufu huo, Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini walielekezwa kupitia na kuandaa upya maombi hayo na kuhakikisha kuwa mchakato wa kuanzisha vijiji vipya unazingatia misingi ya Sheria na unashirikisha wananchi na wadau wengine ili kuepuka malalamiko.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Desemba 2008, jumla ya maombi 17 yaliyokuwa yamepokelewa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya kuanzisha vijiji vipya na yamefanyiwa kazi. Maombi hayo ni pamoja na uanzishaji wa vijiji vipya vya Kigina na Magarama. Halmashauri ya Wilaya itafahamishwa rasmi uamuzi utakaotolewa kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa haujafanyika hapo Oktoba, 2009. Kwa sasa napenda kumWomba Mheshimiwa Mbunge kuvuta subira ili tuweze kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa kitongoji vya Kigina na Magarama wamekuwa wakipata huduma muhimu za Afya, Elimu, Maji na Barabara. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, wananchi wa Kitongoji cha Kigina na Magarama wamekuwa wakipata huduma ya maji kutoka kwenye mito iliyoko karibu na makazi yao.

Aidha, wananchi wa Kigina wanapata huduma za Afya na elimu katika Kitongoji cha Kigaga na wananchi wa Magarama wanapata huduma kama hizo katika Kitongoji cha Maendeleo. Hata hivyo, huduma hizo ziko umbali wa kilomita zaidi ya kumi na mbili kutoka walipo wananchi wa Vitongoji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa huduma muhimu katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ni wajibu wa Halmashauri kuhakikisha kwamba huduma hizo zinapatikana kwa kuzingatia mipango na vipaumbele vya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

Napenda kusisitiza kuwa Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo waendelee kuwashirikisha wananchi katika maeneo yao katika kuimarisha huduma na miundombinu iliyopo. Kwa upande wa Serikali itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuboresha huduma kwa wananchi kadri uchumi wa nchi unavyoimarika kwa kuzingatia vipaumbele vinavyowekwa na wananchi wenyewe wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya yao.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Naibu Waziri alivyoweza kujibu swali lake, lakini kimsingi ni lazima aelewe kwamba hoja yangu nilileta wakati wa kipindi cha Bajeti ya mwaka jana na wazungu wanasema *first in first out*, mwenyewe amekiri kwamba hao wananchi wa vijiji viwili wanapata huduma maili 12 atakubaliana na mimi kwamba bado wananchi hao wanapata usumbufu wakati baada ya hilo kuwasilishwa hapa Bunge lingeweza kufanyiwa kazi na sasa hivi wananchi wangekuwa wanapata huduma bila matatizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kabisa kwamba ni kweli kwamba maombi haya yamekuja mapema sana wakati wa kipindi cha Bajeti kama ilivyo kwa vijiji vingine vingi sana ambavyo vinatokana na Mikoa yetu na Wilaya na anachozungumza hapa anasema kwamba kwa vile walikuwa wa kwanza basi ingekuwa ni vizuri Serikali ikaona kwamba wanapewa sasa hiyo fursa ya kuanzisha hivyo vijiji.

Vijiji hivyo vinapoanzishwa, vinafuata taratibu na vinapitishwa katika Halmashauri zinazohusika na kuna vigezo ambavyo vimewekwa ili kusema kwamba kijiji hiki kiwe kijiji au kisiwe kijiji mtakumbuka Waziri wan chi aliposimama hapa alieleza katika Bunge lako Tukufu hili kwamba zoezi hili limekuwa linaendelea na sasa hivi tunavyozungumza linaelekea kwenye kukamilika.

Kwa hiyo maombi yote ambayo yameletwa hapa na ambayo yataonekana kwamba yametimiza vigezo vilivyowekwa yatakuwa yamefikiriwa na tutahakikisha kwamba tunafanya hivyo kabla ya uchaguzi mkuu ambao unakuja kwa ajili ya vijiji vyetu mwaka 2009 mwezi Oktoba. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa avute subira lakini tumesikia concern yake na sisi tutaona kwamba tunakwenda kama Mheshimiwa mwenyewe anavyotaka.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa suala la maombi ya vijiji hata na kata pia limekuwa ni suala la siasa na eti unakuwa umefanikiwa kisiasa kama tu umefanikisha kuwapatia vijiji au kata badala ya kufikiria maendeleo na kwa kuwa hili tatizo ni kubwa sana na kila Mbunge hapa nadhani anatatizo hilo hivi Serikali kama taratibu zote zinafanyika kwenye Halmashauri kama vigezo vyote vinapimwa na Halmashauri husika kwanini Halmashauri zenyewe zisiamue kutoa hizo leseni za vijiji au kutokutoa kwa sababu kwa kutumia vigezo hivyo hivyo vilivyowekwa na Wizara? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, unapoamua kuanzisha Mamlaka mpya kwa maana ya Vijiji, Vitongoji, Halmashauri na mkoa kimsingi unachozungumza pale unazungumzia habari ya kupeleka huduma karibu zaidi na wananchi ndicho unachotaka kufanya pale na kurahisisha maamuzi ili waweze kufikia maamuzi ambayo yatakuwa yameleta maendeleo katika eneo lao.

Mheshimiwa Simbachawene anapendekeza kwamba Mamlaka hizi zingepewa fursa au ruksa ya kuamua zenyewe mradi ziwe zinahakikisha kwamba zinafikia vigezo vilivyowekwa. Hatari iliyoko hapa ni kwamba hivi vijiji na hizi Halmashauri pamoja na Mikoa yote tunayozungumza hapa, maendeleo yake yanategemeana na ruzuku ambayo inatoka kutoka kwenye *centre* na ruzuku ile kwa vile ni kidogo na *resources* zetu ni kidogo ukiruhusu tu watu wakaanzisha wao wenyewe kule waliko bila ya kuwa na *controls* kwa maana ya kuweza ku-*meet* vile vigezo vilivyowekwa pale. Iko hatari kwamba itakuwa wewe na vijiji vingi na maeneo mengi ya kiutawala lakini uwezo wako wa kuendesha hivyo vijiji ukawa ni mdogo. Ndiyo maana ikaonekana kwamba kuna haja ya kuratibu mpango huu na kimsingi tunachojua ni kwamba hatuendi kinyume kabisa na maamuzi ambayo yanafanywa na Halmashauri zinazohusika tunachoangalia pale ni kwa ajili ya kuona tu kama vigezo vile vimetimizwa.

Lakini pia kuangalia uwezo wetu wa kuweza kuendesha sasa hizo Mamlaka mpya zinazozungumziwa hapo na ielewe hoja ya Mheshimiwa George Simbachawene, ni ya msingi lakini sasa huu utaratibu ndiyo utaratibu unaotumika na ambao unatamkwa katika Sheria Na. 7 na 8 inayoanzisha Mamlaka hizi. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Mamlaka mbalimbali unatokana na Sheria zilizotungwa na Bunge kwa upande wa kata, vijiji na vitogoji mwenye Mamlaka ya kugawa ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Tukisema tuziachie Wilaya au Halmashauri 133 kila mmoja ifanye igawe kwa vigezo ambavyo vipo haitawezekana mpaka tubadilishe Sheria tuzipeleke huko kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Naomba tu niwaeleweshe Waheshimiwa Wabunge kwamba vijiji, kata na vitogoji pamoja na mitaa tunavigawa mara moja kwa miaka mitano na mara nyingi tunavitangaza karibu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa hiyo kwa mwaka huu vijiji vyote ambavyo vimekidhi vitoji pamoja na mitaa vilivyokidhi mahitaji vitagawanywa na

tutatangaza hivi karibuni ni vijiji gani ambavyo vimekubalika na ni mitaa gani na vitogoji gani. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira zoezi hili linakamilika hivi karibuni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado Mheshimiwa Msindai una hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, bado ninayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, kwa kuwa toka uchaguzi uliopita wananchi wengi kwenye maeneo mbalimbali walitoa mapendekezo ya kugawa maeneo yao ya vitogoji kuwa vijiji na ya kapita kwenye Halmashauri na kupelekwa Wizarani. Waziri haoni kwamba kama kuna Halmashauri imezembea kuwanyima haki wananchi hao wahusika ni lazima wachukuliwe hatua, hatua zinazostahili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Maombi haya yameletwa na tulisimama hapa Bungeni hapa kuwataadharisha Wabunge kwamba zoezi hili sasa linakamilika na tuliposema vile kwa kweli maombi yakaongezeka kwa wingi sana na ambayo yalifuata taratibu zilizowekwa. Sipati tabu sana kuwaelezea Waheshimiwa Wabunge kuhusu utaratibu unaotakiwa kufuatwa kwa sababu najua kwamba wako katika Halmashauri kwa hiyo wanajua kwa hiyo ndiyo maana sipati tabu sana kueleza jambo hili. *(Makofi)*

Sasa kinasemwa hapa kuna jambo linalozungumzwa hapa kwamba kuna mtu amekiuka hakufuata taratibu na japo amecheleweshsa na maombi hayakufika na hatua gani zichukuliwe? Bado mchakato utakuwa ni ule ule Halmashauri inayohusika ina Mamlaka na madaraka ya kusema kwamba huyu mtu tulimwagiza afanye hivi hakufanya.

Kwa hiyo, Mamlaka za juu zinazohusika zitapewa taarifa kupitia kwa mkuu wa mkoa kuja mpaka TAMISEMI na kusema huyu alifanya hivi na tunafikiri kwamba amezembea na sidhani kama Seriakali inaweza ikakaa hapa ikasikia kwamba eti kuna mtumishi mzembe huko anainyima sasa Halmashauri pale haki yake ya kuwa na tawala mpya halafu tunasema tunamvumilia, tutamvumiliaje. Hii ni *serious government* haiwezi kuvumilia mambo ya namna hiyo kama kuna jambo la namna hiyo tutaomba tuletewe, na tukiletewa kwamba mtu amechelewesha eti maombi pale Urambo hakuleta maombi ya vijiji tutachukua hatua. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nashukuru kwa msisitizo wako hasa pale Urambo wanatakiwa waonyeshe.

Na. 41

**Kodi ya Dharura kwa Wasafiri wa Meli-Ziwa Victoria**

**MHE. KABWE Z. ZITTO** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 1994/1995 katika hotuba ya bajeti ndogo, Serikali iliamrisha kodi ya wasafiri wa meli katika Ziwa Victoria kama njia ya Dharura ya kupata mapato ya kodi ambayo imelipwa na watu wa Ukerewe na Bukoba tu, na kwa kuwa, kodi hiyo imekuwa kero kubwa kwa wasafiri kwa sababu ya kupanda kwa gharama za usafiri kwa wananchi wa kawaida lakini pia imekuwa ya kibaguzi kwa sababu inalipwa na watu wa Ukerewe na Bukoba tu:-

(a) Kwa kuwa, kodi hiyo imefikia shilingi 600/= kwa safari; Je ni lini Serikali itaifuta kodi hiyo?

(b) Kama kodi hiyo ina ulazima wowote wa kuendelea kuwepo; Je, kwa nini mapato yake yanayokusanywa yasipelekwe kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo meli hutia Nanga ili zitumike kwa ajili ya shughuli za maendeleo mfano Ukerewe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Sheria ya Tozo za Huduma za Bandari ya Mwaka 1973, kifungu cha tatu, kila abiria analazimika kulipa tozo ya matumizi ya huduma ya bandari anapoondoka kwa kutumia kivuko au meli kwa umbali wa kilometa tatu au zaidi katika Tanzania Bara. Abiria ambao ni raia wa Tanzania wanatakiwa kulipa shilingi 500 wakati abiria ambao sio raia wa Tanzania wanatakiwa kulipa dola za Kimarekani 5. Kodi hii ni ya msingi na ya kawaida katika sheria za kodi za Jamhuri ya Muungano na kwa hiyo siyo ya dharura. Aidha, ulipaji wa kodi hii sio wa kibaguzi kwa sababu unawahusisha wasafiri wote wa meli wanaotumia Ziwa Victoria.

(b) Mheshimiwa Spika, mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali Kuu kimsingi ni wa kuzingatia vipaumbele Kitaifa, na si wa kutumia mapato katika maeneo mapato hayo yalipokusanywa. Hata hivyo, Serikali imeupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuangalia uwezekano wa kupeleka kwenye Halmashauri mapato yanayokusanywa ili yatumike kwa shughuli za maendeleo.

Na. 42

**Kuanzisha Huduma za Benki ya Posta Itigi Mitundu**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Miji ya Itigi na Mitundu inazidi kushamiri na kupanuka kibiashara. Je, ni lini Benki ya Posta itaanza huduma za Kibenki katika miji hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini na biashara ya kibenki kwa sasa ni biashara huria ambayo anayowekeza anatarajia kupata faida. Hivyo, kabla ya kufanyika kwa uamuzi wa kufungua tawi la benki, ikiwemo benki ya posta hufanywa tathmini ya kina ili kuona kama vigezo muhimu vinavyokidhi matarajio ya biashara ya kibenki vinatimizwa.

Vigezo hivyo ni pamoja na:-

(i) Upembuzi yakinifu ili kutambua kuwa tawi linalotarajiwa kufunguliwa litakidhi malengo ya kibiashara (faida);

(ii) Kuwepo kwa miundombinu muhimu ya kuwezesha tawi kufanyakazi kama vile usafiri, umeme, ulinzi, mawasiliano ya simu na upatikanaji wa jengo linalofaa kwa kuendesha biashara ya benki; na

(iii) Uwezo wa kifedha wa wananchi wa eneo hilo kutokana na shughuli zao wanazozifanya za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, kama ifuatavyo:-

Benki ya Posta Tanzania hivi sasa inatoa huduma za kibenki katika matawi yake 26 yaliyo katika Makao Makuu ya Mikoa. Aidha, benki imefikisha huduma zake katika ngazi ya Wilaya na baadhi ya Tarafa kwa kutumia vituo vya Shirika la Posta kwa Mkataba wa uwakala. Lengo la Benki ya Posta ni kutoa huduma za kibenki kwa wananchi.

Benki ya Posta kwa kushirikiana na Shirika la Posta itaangalia uwezekano wa kuwa na huduma za kibenki mji wa Itigi na mji wa Mitundu, baada ya kufanya tathimini ya kufahamu ukubwa wa kibiashara iliyopo kama inakidhi vigego vya biashara vya benki.

**MHE. JOHN P. LWANJI :** Mheshimiwa Spika, asante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotajwa cha pili na cha tatu vyote viko tuna miundombinu mizuri kabisa na hayo yaliyoainishwa pamoja na wananchi wake na matukio yanayotokea sasa hivi ya uporwaji wa watu fedha zao wakati wanapeleka benki

ni ushahidi ni juzi tu actually na mwaka jana anatoa pesa kutoka Itigi kwenda Manyoni shilingi milioni 7 na nusu aliporwa.

Sasa matukio haya Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Ndani yanajua na tunadhani kwamba suluhu pekee ni kurahakisha benki.

Swali ni lini hasa maana tunaambiwa kuna upembuzi yakinifu na ukishatoka upembuzi yakinifu huja usanifu na ndipo rasilimali ianze kutafutwa. Sasa huo muda ni lini Waziri atuhakikishie kwamba watu wa Itigi na watu wa Mitundu wanaweza wakapata hudumza za kibenki.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo kwamba kuna matukio ya uporaji ambayo yametokea mara kwa mara kati ya Mitundu na Itigi na Manyoni je, Wizara hizi mbili zinafanya nini kuhakikisha kwamba uporaji huu hauendelei.

**SPIKA:** Swali la uporaji halihusu Wizara ya Fedha, kwa hiyo kwa kiwango hicho basi hilo naliondoa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI – (MHE. OMAR YUSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni lini mimi nadhani Mheshimiwa Mbunge tungeendelea kushirikiana tu na Wizara iko tayari kufanya kazi karibu zaidi na wewe ili tuendeleze mazungumzo na benki ya posta pamoja na shirika la posta hatimaye waweze kufungua kituo cha Benki pale Itigi haraka.

Mheshimiwa Spika, nadhani Mheshimiwa mbunge tuendelee kushirikiana katika suala hili. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kuniona, kwa kuwa wananchi wote nchi wametambua kuweka akiba fedha zao katika benki mbalimbali zilizoko hapa nchini pamoja na wananchi wa mkoa wa Singida, na kwa kuwa katika benki hizo pamoja na *NMB* mkoani Singida hasa iliyopo Singida mjini imekuwa na wateja wengi sana karibu kila siku licha ya mwisho wa mwezi.

Je, Serikali kwa kuwa ATM ni moja tu iliyopo Singida Mjini iko tayari kuongeza tawi lingine la ATM ili kuondoa msongamano wa watumiaji wa benki hiyo mjini Singida ?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE):** Mheshimiwa Spika, utakumbuka hivi juzi tu nilijibu suala la NMB na nikaeleza kwamba tatizo hilo la Benki ya NMB wamekwisha kuliona, na sisi kama Wizara ya Fedha tumeliona na tunalifanyia kazi ili kuweza kupunguza huu msongamano uliopo katika Benki zetu za NMB hasa wakati wa mwisho wa mwezi. Namwomba Mheshimiwa

Mbunge avute subira katika kipindi cha karibuni ataona mabadiliko katika maeneo mengi yenye Benki za *NMB.* (*Makofi*)

Na. 43

**Mwambata wa Afya Kupelekwa Nchini India**

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wizara ya Afya ilisaini Mkataba na Hospitali ya Apollo nchini India ili kutoa matibabu kwa Watanzania; na kwa kuwa, nchi yetu imekuwa ikipeleka wagonjwa wengi nchini India na kwamba Serikali iliahidi kupeleka Mwambata wa Afya (*Medical Attache*) ambaye atadhibiti aina ya ugonjwa na gharama za matibabu zitolewazo ili kupunguza gharama kubwa zinazotolewa:-

(a)Je, ahadi hiyo imetimizwa na ni nani aliyepelekwa na sifa zake ni zipi?

(b)Je, kuna faida au manufaa gani baada ya Afisa huyo kupelekwa Ubalozini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali iliahidi kumpeleka Mwambata wa Afya (*Medical Attache*) ambaye pamoja na kushughulikia masuala mengine atahakiki gharama za matibabu ili kuipunguzia Serikali gharama inazotozwa.

Daktari atakayepelekwa ni Daktari Msaidizi Mwandamizi, ambaye ana uzoefu mkubwa wa rufaa za wagonjwa. Wizara ipo katika hatua za mwisho za kumpeleka huko India. Nyumba imepatikana na utaratibu unafanyika hivi sasa wa kumpatia "*orientation*" na kumwekwa katika safu ya Maafisa wanaofanya kazi kwenye Balozi.

(b)Mheshimiwa Spika, manufaa yanayotarajiwa kutokana na kumpeleka Mwambata huyo India ni pamoja na haya yafuatayo:-

- Ataweza kuishauri Serikali nini kifanyike katika uboreshaji wa huduma hizo nje na ndani ya nchi.

- Atasaidia kuharakisha mawasiliano kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Hospitali husika zilizopo India na hivyo kuharakisha ulipaji madeni.

- Atasaidia kuhakiki madeni na kutoa ushauri kwa Serikali na hivyo kupunguza athari zinazoweza kutokea kutokana na madai yaliyo makubwa kuliko gharama halisi. Hii inatokana na ukweli kwamba ana taaluma ya afya.

- Ataweza kufuatilia kwa karibu afya za wagonjwa walio kwenye matibabu na waliokwishapewa matibabu na kufanya tathmini, na kutoa ushauri au mapendekezo kwa Serikali.

- Vilevile kuwepo kwake kutapunguza kazi za Afisa Balozi ambaye kwa sasa analazimika kufanya kazi nyingi nje ya zile alizopangiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa *Engineer* John Kijazi, Balozi wetu nchini India, na Bwana Seneta Makorongo, Afisa katika Ubalozi huo kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika kuwahudumia wagonjwa wanaopelekwa India kwa matibabu. (*Makofi*)

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mhesimiwa Spika, ahsante. Pamoja na kwamba swali hili nililiuliza mwezi Juni mwaka jana, lakini najua kwa sababu ya wingi wa maswali halikuja kwa wakati, lakini pamoja na kwamba swali hili limekwishazungumzwa mara mbili, tatu na Wizara hii hii ya Afya na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje. Nimshukuru Waziri wa majibu yake mazuri, lakini ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kama Mheshimiwa Waziri alivyosema na mimi ninawapongeza Balozi Kijazi pamoja na huyo Afisa Makorongo, lakini siyo tu kwamba nawapongeza nawapa pole kwa kazi wanayoifanya.

La kwanza, je, sasa ni lini hatimaye Wizara itatwambia huyo Afisa wanayemuandaa kwa ukamilifu hivyo, ni lini sasa atakwenda Ubalozini ili kuwapunguzia hao kazi ili wafanye kazi yao ambayo imewapeleka Ubalozini?

La pili, Wizara yetu ya Afya kwa sababu iliingia Mkataba na Hospitali ya Apollo tuna deni kubwa sana. Hali ambayo sasa kwa ambao wanakwenda kwenda India hususan mimi mwenyewe na wengine wengi ambao wanapeleka wagonjwa hali inapelekea kwamba aidha itafika mwishoni wasitishe au huduma itakuwa ni ya kusuasua sana au hafifu.

Mheshimiwa Hoogan akiwepo huko mwezi Desemba na Januari alizungumza na Balozi wetu Kijazi na kuwambia kwamba tunadaiwa jumla ya *dollar* za Kimarekani 600,000 na labda zitakuwa zimezidi. Je, Mheshimiwa Waziri atatoa tamko gani au atachukua hatua gani za haraka kuhakikisha kwamba deni hilo linalipwa na kuliarifu Bunge lako Tukufu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza anataka nitamke ni lini? Uwezo wa kutamka tarehe sina, lakini kama nilivyosema katika jibu langu kwa swali la msingi ni kwamba tupo katika hatua za mwisho.

Tulikwisha tenga hata fedha kwa ajili ya huyo mtaalam katika mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, fedha zipo. Mchakato ni mrefu kidogo kama nilivyosema kwamba kwa upande wetu kusema kweli tumemaliza, lakini kuna kum-*oriented* katika masuala ya

mambo ya nje, lakini nilitaka nisitamke pia kuna mambo ya *vetting* ndiyo hayo tunangojea ambayo yapo nje ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikiri kwamba suala la madeni na sisi linatukera, linatukera kwa sababu tunadaiwa, na huko nyuma imewahi kutokea kwamba hospitali inakataa kupokea wagonjwa wetu kwa sababu ya madeni, na nilikuwa India mwanzoni mwa mwaka huu nikiongoza ujumbe wa wataalam katika Tume ya Pamoja na India na hili suala tulilizungumza na wakati huo madeni yalifikia shilingi bilioni 1.7 ambazo sijacheki leo, lakini zilikuwa zinaandaliwa ili tuzipeleke.

Mheshimiwa Spika, nikirudia majibu yangu ya swali la msingi tunategemea kwamba kumpeleka mwambata ni moja ya manufaa tutakayoyapata kwamba haya masuala yataharakishwa. Kwa sababu hizi ankara zinapokuja pale Ubalozi ni lazima zihakikiwe, na ukiwa na mtu ambaye hana taaluma ya udaktari inakuwa vigumu. Kwa hiyo, ni matumaini yetu kwamba kuwepo kwa mwambata kutaharakisha mambo haya na labda pale ambapo gharama ni juu kuliko ambavyo ingestahili ataweza kuuliza maswali na hii itatupunguzia, lakini mawasiliano yatakuwa ni mazuri zaidi na ya haraka akiwepo pale.

**MHE. HAMAD RASHID MOHEMAD**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina swali mojal a nyongeza. Kwa kuwa hatua ya kupeleka Daktari huko Apollo ni hatua ya muda mfupi, lakini Apollo hospitali tayari wamekwishaingia mkataba na NSSF kwa ajili ya kujenga hospitali nzuri hapo Dar es Salaam. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha mpango huu ili kuwa na jambo la muda mrefu zaidi na la kudumu na la kuwasaidia watanzania wengi ambao wanahitaji huduma bora za afya badala ya kushikilia tu kuendelea kuwapeleka wagonjwa India wakati jambo hili lipo tayari hivi sasa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika hatua za muda mrefu za kupunguza wananchi tunaowapeleka India kwa matibabu, mchakato uliopo sasa hivi ni kujenga hospitali ya Apollo hapo Jijini Dar es Salaam. Kazi ya Serikali ni kuweka mazingira, na swali lilikuwa kwamba hatuwezi kuharakisha na ni kweli tunaliharakisha. NSSF wameingia mkataba na Hospitali ya Apollo. Hatua za awali ilikuwa ni kutafuta wapi hospitali ijengwe. Wenzetu walitaka katikati ya Jiji la Dar es Salaam na sisi tuliona kwamba pamejaa. Lakini nitamke kwamba sasa hivi tumepata kiwanja eneo la Chuo Kikuu na wamekubaliana kwamba NSSF watajenga jengo lakini wenzetu wa India wataleta vifaa na wataalam wa kuanzia. Kwa hiyo, sisi tumeweka mazingira na kila wakati tunalisukuma na tuna imani kwamba katika muda si mrefu jengo litaanza kujengwa. (*Makofi*)

**Na. 44**

**Ujenzi wa "National Traditional Medicine Laboratory"**

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA K.n.y. VICTOR K. MWAMBALASWA):**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuomba kujibiwa hili swali, naomba nitoe maelezo kidogo kwamba kumbukumbu zinaonyesha kwamba hili swali lilikwishaulizwa katika kikao kilichopita cha Kumi na Tatu, na baada ya kuwasiliana na muuliza swali na yeye vilevile ana kumbukumbu hizo hizo. Sasa endapo kama labda yale majibu yaliyotolewa hayakutosheleza, basi naomba hayo majibu ambayo hayakutosheleza yaweze kujibu katika swali namba 44.

**SPIKA:** Kwa maelezo hayo naona yametosheleza. Kwa hiyo, sasa tunahamia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi naona ni Mheshimiwa Diana Chilolo kwa masikilizano kwa niaba ya Mheshimiwa MohamMed Dewji.

Na. 45

**Ugawaji wa Vitabu kwenye Shule za Msingi na Sekondari**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kutokana na mabadiliko ya mfumo wa ufundishaji wa mitaala mipya Serikali ilitoa vitabu vyenye thamani ya Tshs bilioni 50 kwenda katika shule za msingi na sekondari zote nchini; na kwa kuwa utaratibu wa usambazaji wa vitabu hivyo huwa mbovu na baadhi ya Mikoa bado haijapokea fungu lolote la vitabu hadi sasa kama katika Jimbo la Singida Mjini ambako hatujapokea kitabu hata kimoja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa na kusimamia ugawaji wa vitabu hivyo kwa uwiano sawa katika shule zote nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA FUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijawahi kutoa vitabu vya thamani ya shilingi bilioni 50 kama swali linavyosema. Baada ya mabadiliko ya mitaala ya shule za msingi na sekondari mwaka 2005, Wizara yangu iliendelea kutumia utaratibu wa Kamati za Shule kununua vitabu kupitia ruzuku iliyokuwa inapelekwa.

Shule za msingi zilinunua vitabu kupitia ruzuku iliyotolewa na Serikali Kuu kupitia TAMISEMI na zile za sekondari kupitia ruzuku iliyopelekwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kulingana na utaratibu huo suala la Wizara kusambaza vitabu halikuwepo.

Mheshimiwa Spika, miaka 2 baada ya mtaala kuanza kutumia, Wizara ilibaini kuwepo tatizo kubwa la vifaa katika shule za msingi hususan vitabu vya madarasa yaliyoanza na mtaala mpya wa darasa la kwanza hadi la nne, uhaba mkubwa wa madawati na zana za kufundishia Sayansi.

Katika kulitafutia ufumbuzi wa haraka tatizo hili, Wizara ilitenga shiling bilioni 8,401,459,000 na kuzipeleka kwenye Halmashauri zote. Mgao wa fedha hizo ulizingatia idadi ya wanafunzi katika kila Halmashauri. Halmashauri zote ziliarifiwa kwa barua ya Wizara Kumb. Na. *ED/PEDP/ACT/PL/Vol.1/61* ya tarehe 14/03/08. Halmashauri ya Singida Mjini ilikuwa na shule 43 zilizokuwa na wanafunzi 28,704 wakati huo, hivyo, ilipelekewa shilingi milioni 23,822,000/= kupitia akaunti Na.5081200008 tawi la NMB Singida.

Aidha, kwa mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Manispaa ya Singida imetengewa shilingi milioni 73,022,400/= kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 24,217,600 zilikuwa zimeishapelekwa Wilayani humo hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekondari utaratibu wa utoaji vitabu ni huo huo nilioueleza kwa shule kujinunulia vitabu. Kati ya mwaka wa fedha 2005/2006 na 2008/2009, jumla ya shilingi bilioni 19,732,591,200 zimepelekwa kwenye shule za Serikali kama ruzuku ya ununuzi wa vifaa vya kufundisha vikiwemo vitabu. Shule zisizo za Serikali zilipelekwa shilingi milioini 500,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Wizara hupeleke hela kupitia ruzuku na Kamati za shule ndizo ambazo huwa zinanunua vitabu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba shule zingine hazinunui vitabu kupitia fedha hizo na upata vipaumbele vingine licha ya Serikali kutoa agizo hilo na kupeleka fedha.

(b) Kwa kuwa, ununuaji wa vitabu hivi kulingana na mitaala hii mipya bado ina utata. Je, Serikali haioni kwamba ina kila sababu kurudia utaratibu wa zamani. Serikali kununua vitabu yenyewe na kupeleka mashuleni kuliko wanavyofanya sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA FUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, hatunazo taarifa kwamba Wakuu wa

shule au walimu Wakuu hawanunui vitabu. Hivyo, naomba kupata ushirikiano kama upo ushahidi wa kutosha Halmashauri au Afisa Elimu katika Halmashauri yoyote anao uwezo wa kuchukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naahidi kufuatilia tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba hata hii njia ya tatu ambayo ndiyo tunaitumia inaleta utata. Awali miaka ya 70 hadi 80 Wizara ilikuwa inanunua vitabu na kuvipeleka katika shule, baadaye ikaonekana vitabu vinachelewa hadi mwaka havijafika shuleni. Tukabadili Halmashauri zikawa zipelekewa fedha zinunue napo ikaonekana ni tatizo. L akini baada ya kuleta ungatuaji tukaona tuwape mamlaka shule zenye zijinunulie.

Mheshimiwa Spika, hivyo endapo utaratibu huu nao umeonekana kutoleta ufanisi, basi tutaufanyia kazi na sisi tupo tayari kutoa huduma kwa haraka na kwa kadri tutakavyoweza ili wanafunzi waweze kupata vifaa wanavyostahili katika kujifunzia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali moja tu la nyongeza kwa ambaye hajauliza kwa muda mrefu. Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza.

Kwa kuwa sekondari zote nchini zinafanya mtihani moja unaofanana kwa shule za kidato cha nne kwenda kidato cha tano bila kujali kwamba hizo shule zina nyenzo za kutosha kama vile vitabu, walimu, maabara na kadhalika.

Je, Serikali inatenda haki vipi katika kupima ufaulu wa wanafunzi katika shule hizo ambazo zinafanya mtihani moja bila kuangalia uchache wa nyenzo hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA FUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba mtaala unaotumika kwa shule zote za sekondari ni moja ukiondoa shule zile ambazo ni za Kimataifa. Hivyo, tuna matarajio na ndicho kinachofanyika kwamba ufundishwaji uzingatia mtaala na muhtasari wa masomo tukiamini kwamba wanakwenda kwa wakati kwa kadri walivyojiandalia maazimio yao ya kazi. Ni matarajio yetu kwamba wanafahamu kila ifikapo mwezi wa mitihani wote wanapaswa wawe wamekamilisha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba vifaa vya kufundishia na kujifunzia hupelekewe fedha mashuleni ili walimu wenyewe wanunue, na hivyo wanapaswa kutoa vipaumbele pale ambapo wanaona wanahitaji.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo endapo Wizara ya Elimu itaingilia kwenda hata kuagiza au kuwaagiza vitabu kwa ajili ya shule fulani, basi tutakuwa tumekiuka utaratibu, na hivyo naomba tu tuseme kama hili suala linaonekana halileti ufanisi tupate maoni ya wadau na sisi tupo tayari kulifuatilia na kulifanyia kazi.

Na. 46

**Utaratibu wa Kujiunga na Vyuo vya Ualimu**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, utaratibu wa kuchagua wanafunzi wanaomaliza darasa la 12 kujiunga na Vyuo vya mafunzo ya ualimu umekuwa mgumu na kuwa kero kwa vijana na jamii nzima kwa ujumla; na kwa kuwa utaratibu huo umekuwa ukibadilishwa mara kwa mara kama vile Wakuu wa Vyuo kuchagua wanafunzi, Wizara yenyewe kuchagua au wanafunzi kujaza fomu maalum na pia Wabunge kupeleka orodha ya vijana wao Wizarani:-

(a)Je, Serikali ipo tayari kuweka utaratibu wa wazi usio na mashaka na usiobadilika wa kupata wanafunzi hao?

(b)Je, kwa mwaka 2008 ni wanafunzi wangapi waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu toka Mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya, Tabora na Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Kuanzia mwaka 2009, utaratibu rasmi wa kuchagua waombaji wa mafunzo ya ualimu utazingatiwa. Utaratibu huu unawataka waombaji kuelekeza maombi yao kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wakitumia fomu za Chaguo la Wahitimu wa K4 *(FIV Selform)* baada ya uchaguzi wa Kidato cha V. Lengo la utaratibu huu ni kutoa kipaumbele kwa wahitimu wanaotokea shuleni moja kwa moja, kupunguza udanganyifu na matumizi ya vyeti vya kugushi.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa waombaji wa mafunzo ya ualimu hufanyika kwa kuzingatia kanuni kuu nne ambazo ni:- Kuzingatia sifa, uwiano jumuishi, kupunguza tofauti za uwiano wa walimu kwa mwanafunzi na nne ni kupata waombaji waliofaulu masomo yenye upungufu mkubwa wa walimu.

Pamoja na utaratibu huu mzuri, uzoefu umeonesha kuwa wengi wanaochaguliwa hawaripoti kwa sababu mbalimbali. Sababu hizi ni pmaoja na kupata nafasi za kuendelea na masomo katiak shule zisizo za Serikali, na kujiunga na vyuo vingine na hivyo Wizara kulazimika kuchagua waombaji wengine wa kutumia njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, njia mbadala zilizowahi kutumika ikiwa ni suluhisho la muda tu kwa ajili ya kukidhi mahitaji makubwa ya walimu ni waombaji kupeleka maombi vyuoni. Utaratibu huu uliwahi kutumika kati ya mwaka 2001 na mwaka 2004 kwa lengo la kukasimu madaraka ngazi ya chini katika Serikali. Utaratibu huu ulisitishwa kutokana na matatizo yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na waombaji wengi kuomba zaidi ya chuo kimoja na hivyo wakati wa kuripoti idadi iliyokusudiwa kutotimia. Kwa kuzingatia matatizo yaliyojitokeza ilibidi kuangalia upya utaratibu huu na hatimaye kurudi katika utaratibu rasmi nilioutaja hapo awali.

(b) Mheshimiwa Spika, tunavyo vyuo 34 vinavyotoa mafunzo ya ualimu kwa ngazi ya cheti na *diploma* ikilinganishwa na idadi ya waombaji. Kwa mfano, mwaka 2008 idadi ya waombaji ilikuwa 61,330 na nafasi za mafunzo vyuoni zilikuwa 5,972 (10%) ya waombaji.

Katika mwaka wa masomo 2008/2009 waombaji wa mafunzo ya ualimu waliochaguliwa kutoka Mkoa wa Mwanza ni 391, kati ya waombaji 3,720 (11%); Kilimanjaro ni 495 kati ya waombaji 5,530 (9%); Mbeya ni 285 kati ya waombaji 3,940 (7%); Tabora ni 102 kati ya waombaji 1,673 (6%) na Lindi ni 63 kati ya waombaji 837 (8%) Mikoa walikotoka imebainishwa kutokana na anwani walizoandika katiak barua zao za maombi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwingiliano mkubwa wa Watanzania ni dhahiri kuwa anwani wanazoonesha waombaji siyo asilimia mia moja kwamba ndiyo huko wanakotoka.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hizi njia mbadala ambazo wameainisha hapa zimepelekea kutoa mwanya kwa baadhi ya maofisa wa Wizara kwamba kuna tuhuma hawa maafisa pamoja na baadhi ya wakuu wa vyuo wamekuwa wakiweka nafasi zao na kuziuza kwa rushwa kwamba nafasi moja inakwenda mpaka 700,000 mpaka 800,000.

(a) Je, Serikali iko tayari kulifanyia kazi hili na baadaye kuliarifu Bunge kwa miaka mitatu iliyopita kama hili lipo?

(b) Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kuona uwiano wa wanafunzi wanaochaguliwa kuingia vyuoni kwa kuzingatia idadi ya watu katika Mikoa hali halisi ya elimu kwamba mingine iko nyuma kama vile Shinyanga, Mwanza, Kigoma, kila sehemu, sehemu ziko nyingi zinafahamika kwamba wanafunzi wanachaguliwa maeneo hayo ili wawe kichocheo na pengine kupunguza matatizo kama haya ya mauaji ya vikongwe na *Albino*? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika**,** nakiri kwamba hatuna taarifa ya rushwa zinazofanyika katika vyuo vya ualimu au maafisa katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu *selection*. Tunaomba Mheshimiwa Mbunge, tushirikiane atupatie taarifa kama ana taarifa *specific* tuweze kuanzia hapo katika kulifanyia kazi jambo hili kwa sababu kwa kweli siyo zuri kama linafanyika hivyo. *(Makofi)*

La pili, kwamba *selection* ya walimu kuzingatia hali halisi ya Mkoa kama nilivyosema hapo awali *selection* inazingatia sifa na vigezo na vigezo vingine vinne nilivyotaja. Kwa hiyo, tunapopata yale ya maombi kutoka Mikoani kama nilivyotoa takwimu ndiyo tunavyofanya *selection* kulingana na sifa za wale walioomba. Kama ulivyohisi na ulivyosema kwamba tunapotumia hizi njia mbadala za Wabunge kubeba majina au watu wengine kupeleka majina kwa mkono yanaweza yakazaa mianya ya rushwa. Kwa hiyo, tungependa tuachane na hizo njia mbadala ili kuondoa hii mianya hii ya rushwa badala yake tutumie hii njia rasmi ya kutumia *Selform.*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wapo vijana waliomaliza *form four* mwakajuzi na mwaka jana walituma maombi hawakuweza kuchaguliwa na vijana hawa walikuwa wamepata *division three* na walipotuma maombi hawakuweza kuchaguliwa na mara nyingi wamekuwa wakiwafuata Wabunge kuwaomba wasaidiwe. Je, Serikali iko tayari kuwasaidia vijana hao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza tunatarajia kutumia njia yaani kutumia *selform* kwa wale waliomaliza. Kwa hawa wanafunzi ambao wamemaliza miaka ya nyuma na walipeleka maombi na hawakuchaguliwa itategemea kama tutakuwa na nafasi hizo na kama ushindi wa masomo waliyonayo utakuwa unahitajika.

Na. 47

**Mradi wa Umeme – Tabora – Kigoma**

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2006 Serikali ilitenga shilingi bilioni 10 kama kianzio cha mradi wa umeme wa Gridi ya Taifa toka Tabora hadi Kigoma na katika bajeti ya 2007 haielezi chochote juu ya mpango huo badala yake imeonyesha mipango mipya itakayotegemea wafadhili tofauti na wale wa mpango wa awali wa *ADB*:-

(a) Je, kwa nini mipango ya awali ilisitishwa?

(b) Je, fedha zilizokuwa zimepangwa zilitumika kwa kazi gani na kwa nini Bunge halikujulishwa juu ya matumizi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa na mipango ya usambazaji umeme wa muda mfupi na mrefu kwa kipindi kirefu sasa cha zaidi ya miaka arobaini. Mikakati hiyo imezingatia mahitaji ya nishati hiyo kwa matumizi ya maendeleo na utekelezaji wake umekuwa ukizingatia uwezo wa kiuchumi uliokuwepo kwa wakati huo au unaotarajiwa.

Hata hivyo kwa sababu mbalimbali utekelezaji wa mipango hiyo inakuwa na mabadiliko ambayo inalazimu kuandaa mipango mipya au kuiahirisha kwa muda.

Miradi mikubwa ya umeme kwa kawaida huhitaji mipango yakinifu hata kabla ya utekelezaji na hivyo vipindi vya mipango na hatua zake na vipindi vya utekelezaji ni kawaida kukumbwa na mabadiliko ya namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya awali sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli katika bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2006/2007 Serikali imetenga shilingi bilioni 10 kama kianzio cha mradi wa umeme wa gridi ya taifa toka Tabora hadi Kigoma.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kupeleka umeme wa uhakika Mkoani Kigoma, Serikali iliamua kufanya upembuzi yakinifu wa kupeleka umeme Kigoma kutokea Tabora.

Matokeo ya upembuzi huo yalionyesha kuwa kiufundi na kiuchumi njia hiyo si muafaka kufikisha umeme Kigoma na ikaonekana ni vema kutafuta njia nyingine.

Aidha, gharama za mradi huo wa kuunganisha umeme Kigoma kutoka Tabora zilikuwa kubwa kwani ilikadiriwa kugharimu Dola za Marekani 68,875,480.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu mbalimbali za kiutalamu na za kiuwezo zilizotajwa hapo awali mpango huu wa kutoa umeme Tabora zilizotajwa hapo awali mpango huu wa kutoa umeme Tabora na kuupeleka Kigoma ulisitishwa na kubuniwa mipango ya muda wa kati na mrefu. Mpango wa muda wa kati ni kwa kutumia maporomoko ya Mto Malagarasi.

Mradi huu unajumuisha ujenzi wa kituo cha umeme kwenye mto Malagarasi pamoja na njia ya umeme kwenye Mto Malagarasi pamoja na njia ya umeme kwenda Uvinza, Kigoma, Kasulu na vijiji vya njiani na unafadhiliwa na *Millennium Challenge Corporation (MCC)* ambapo utekelezaji wake umeshaanza.

Katika mipango ya muda mfupi, Serikali ilitenga kwenye bajeti yake ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha wa 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 13.8 kwa ajili ya kununua mitambo mipya ya kuzalisha umeme wa MW 6 mradi ambao ulikuwa unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2009. Wiki iliyopita *TANESCO* wamekamilisha taratibu za zabuni.

(b)Mheshimiwa Spika, fedha zilizopangwa za kiasi cha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Kigoma ni kati ya fedha ambazo hazikutolewa na HAZINA *(Unutilized Budget).* Itakumbukwa mwaka 2006/2007 uchumi wetu ulikumbwa na tatizo kubwa la ukame na kuilazima Serikali kufanya uhamisho wa fedha ili kukabiliana na tatizo la umeme na njaa kufuatia tatizo la ukame, ambalo pia liliathiri ukusanyaji wa mapato ya Serkali.

Kitabu cha hesabu za Serikali zinaozishia tarehe 30 Juni, 2007 *(appropriation Account and other statement for the year ended 30th June, 2007)* zinaonyesha kuwa kati ya bajeti ya shilingi bilioni 432.5 iliyopitishwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 151.2 hazikupatikana *(unutilized Budget)* jambo lililosababisha miradi mingi kutopatiwa fedha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri akitoa majibu ya Serikali kwanza amenichanganya, amesema kwamba *feasibility study* imeonyesha kwamba mradi wa umeme wa bilioni 10 haukuwa *viable*. Lakini kipindi hicho tuliambiwa kwamba *feasibility study* imefanyika na tutapatiwa umeme kupitia Urambo, Kaliua, Tabora.

Sasa mwaka 2007 tulipewa tena mradi mpya wa umeme kupitia Geita, Kibondo, Kasulu ndio ufike Kigoma Mjini, lakini huo hajaelezea. Mwaka 2008 ndio tumeambiwa tutapata umeme kwa kupitia mradi wa *MCC.* Nataka kujua umefikia wapi na utagharimu kiasi gani kwa sababu naogopa inawezekana 2009/2010 tukaletewa mradi mpya kwa sababu imekuwa ni kawaida.

Swali la pili, sasa hivi Kigoma iko gizani na uchumi wa wananchi unazidi kudidimia. Kuna vijana ambao wamejiajiri katika kazi za *welding machines* kuna akinamama kutoka maeneo mbalimbali wa mijini na vijijini wamejiajiri katika viwanda vidogo vya *SIDO* wanatengeneza sabuni kutokana na miche ya michikichi nao mitaji yao inaendelea kudidimia na kuna wale wenye mabucha ya samaki na nyama nao mitaji inaendelea kudidimia kwa sababu umeme haupatikani kabisa. Sasa Waziri amesema fedha za awali zile bilioni 10 zilitumika katika maeneo yenye njaa na maeneo ambayo yana tatizo la umeme. Sasa Kigoma hatukuwa na njaa tulikuwa na tatizo la umeme kwa nini ile shilingi bilioni 10 isingetumika kununua mitambo ili tunusuru hali iliyopo sasa?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Nishati na Madini. Na huu mchezo jamani Serikali wa kupeperusha miradi kila inapokaribia Urambo mnaondoa. Ninyi mna nia njema na Spika kweli? (*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, namwomba radhi Mheshimiwa Mhonga nadhani wakati najibu swali langu hukunielewa. Nimesema hivi mwaka 2006/2007 zilitengwa shilingi bilioni 10 za kianzio kwa ajili ya mradi huo ambao thamani yake ulikuwa ni shilingi bilioni 69 kutoka Tabora kwenda Kigoma. Mradi huo ulikuwa unategemea kuchukua umeme wa gridi. Lakini tunafahamu wazi kabisa kwamba umeme wetu wa gridi kwanza hautoshi, lakini pili unakumbwa na matatizo makubwa ya miundombinu.

Kwa hiyo, katika hatua za *transmission* tofauti na maeneo mengine ambapo *efficiency* za *transmission* zinafanya kwamba umeme ambao unatoka *Southern Islands* kwenda mpaka Kigoma utapoteza labda asilimia 10 mpaka kufika Kigoma. Sisi umeme wetu kwa sababu ya udhaifu wa miundombinu tunapoteza asilimia 30.

Kwa hiyo ili kupeleka umeme wa mahitaji ya Kigoma ya megawati 5 kusema kweli inabidi tupeleke umeme wa megawati 7 au 8. kwa hiyo *in the long term efficiencies* zake na gharama zake ni kubwa. Sasa Serikali nadhani ni haki kabisa kwamba tuwe tunakwenda tunafanya *evaluation.* Wakati wa kufanya *evaluation* hiyo ikaonekana kwamba tupate mradi mbadala. Mradi mbadala kwa sababu ya imani waliyokuwa nayo wafadhili na watu wengine na Serikali hii, tumepata mradi mbadala wa *MCC.* Mradi wa *MCC* unagharimu dola milioni 53. Ukitoka pale Malagarasi unapeleka umeme Kigoma wa megawati 8. Umeme ambao ukifika pale Kigoma pia utagharimu mambo ya *transmission* pale Kigoma lakini utakwenda mpaka Kasulu na utafikisha umeme kwenye vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini ndani ya nafsi yangu kwamba mradi huu wa dola milioni 53 kwanza una unafuu zaidi lakini *scope* yake na yale mambo yanakuwa *accomplish* na mradi huu ni mengi sana kuliko hizo bilioni 69 ambazo zingetumika kutoa umeme Tabora kupeleka Kigoma umeme ambao tayari ungeongeza *load* kubwa zaidi kwenye gridi ambayo iko *over-weight* hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, amesema hivi sasa Kigoma iko gizani. Naomba nilielekeze swali hili kwa wananchi wa Kigoma. Hili tatizo ni kubwa, tunalifanyia kazi muda wote hivi sasa asubuhi hii. Nimetoka kuongeaa na *Gener*al *Manager* Ndugu Mhando, nimetoka kuongea na *Zonal Manager* Ndugu Kingo tunalifanyia kazi on 24 *on our basis*, tatizo lililokuwepo ni kwamba Kigoma kuna mashine 6 ambazo *capacity* yake ni kama ku-*generate* 3 megawati hivi, 3 zilishaharibika hata kidogo sasa hizo 6, 3 zimekufa. Katika hizo 3 ina maana umeme wa 2.8 megawati ambao unakuwa *generated* kwa ajili ya Kigoma sasa hivi Kigoma ina *generate megawatt* moja. Kwa hiyo kusema kweli hali ya umeme wa Kigoma ni mbaya. Sisi Serikali tunalijua tumemwagiza *Zonal Manager* ametoka Kigoma jana amekwenda Mwanza anakwenda kuandaa mafundi zaidi na anarudi na hivi sasa mafundi wanafanya kazi in

*compulsory*. Wako mafundi wanalifanyia kazi Kigoma ya kufungua huo mtambo *crane shaft* imekufa, sasa *crane shaft* ilikuwepo sasa hivi Mtwara.

Kwa hiyo, kwa wakati huo huo tumeagiza mafundi wamekwenda Mtwara wanafungua *crane shaft* ya Mtwara. Hizi kazi ni kubwa lakini tumewaambia *TANESCO* tumewaagiza wanafanya kazi *overtime*.

Mheshimiwa Spika, hata tutakapofanya hivyo bado tutaleta 500 kilowatts tu kwenye umeme wa Kigoma. Kwa hiyo tutakapokamilisha hilo tutakuwa tumefika 1.5 kwa mashine moja, mashine mbili bado zitakuwa zina matatizo. Vipuri vya mashine hizo 2 tumeahidiwa na *TANESCO* kwamba baadhi ziko bandarini na baadhi ziko njiani. Kwa hiyo sisi Wizara ya Nishati na Madini tunaendelea kulifanyia kazi hili jambo kwa kazi kabisa. Naomba wananchi wa Kigoma mnivutie subira kidogo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi ambalo Mheshimiwa Mhonga aliuliza. Baada ya kuwa Serikali imeahirisha mradi ule wa shilingi bilioni 10 wa kutokea Tabora walisema kwamba katika bajeti iliyofuata kuna mradi wa kutokea Geita na Naibu Waziri hajauelezea kabisa.

Lakini pia katika huu mradi wa shilingi bilioni 10 licha ya umeme kufika Kigoma umeme ule wa gridi ungeweza kufika Urambo, Kaliua mpaka Kigoma. Lakini katika majibu ya Waziri nakupongeza hatua ya mradi wa *MCC* kwa Kigoma lakini nini *alternative* ya hii miji mingine ambayo umeme ulikuwa upite?

**SPIKA:** Hili swali zuri sana nadhani pia hata Uvinza ambacho ni Kiwanda cha Chumvi kina chumvi bora ni njia hiyo hiyo. Sasa sijui hizi *feasibility study* zinazobadilika kama kinyonga hizi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mradi unaozungumzwa au unaokuwa *referred to* ambao ulitajwa hapa ni ule mradi wa *Northeast Grid.* Mradi huo ulikuwa ni mpango wa kuunganisha umeme kwenda Kigoma, Kagera na Sumbawanga kutokea gridi ya Taifa kutokea Geita *kilowatt* 220.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa kutokea Geita kuja chini huku kwa *system* nyingine ya *Northeast grid.* Kwa namna yoyote ile ukilinganisha na huu mpango wa umeme uliokuja wa *MCC. MCC* na mradi wa kutoka Malagarasi ni *more efficient* kwa kuzingatia mahitaji ya umeme ya maeneo yale ya karibu. Kwa hiyo kupanga ni kuchagua.

Tulichofanya sisi au walichofanya Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba imevunja ule mradi na kusema kwamba umeme wa Malagarasi kwenda Uvinza. Naomba tu nisisitize kwamba katika umeme huu utakaotoka Malagarasi Uvinza pia iko *included.*

Tunasema *generation* ya umeme uliokuja pale ni *megawatt* 8 lakini *capacity* iliyokuwepo pale ni kwamba baadaye pana uwezo wa kufanya *extension* ukapata hata *megawatt* 28. Sasa wakati unafanya mpango wa kupeleka umeme Kigoma lazima

uzingatie kwamba pana *infrastracture development* ya njia ya katikati ambayo ina maana kwamba Dodoma, Manyoni, Itigi na Kigoma zitakuwa zinaunganishwa kwa barabara. Kwa maana kwamba uchumi wa Kigoma unatarajiwa ufunguke kwa kiwango kikubwa, kwa hiyo mahitaji ya umeme pia yanatarajiwa yawe makubwa zaidi.

Sasa unapofanya hivyo nadhani unakuwa na akiba ya kwamba mradi huu wa Malagarasi hapo umeme wa Kigoma sasa hivi mahitaji yake ni megawati 4 au 5, lakini ukifika megawati 10, 15 basi uwe na *capacity* ya kuuongeza. *Capacity* ya ku-*expand* umeme wa Kigoma uko zaidi Malagarasi kuliko zaidi miradi hiyo mingine.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo busara ninayoiamini wataalamu walitumia katika kutuongoza.

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri ingawa yanakera.

Na. 48

**Hitaji la Umeme Isyesye**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwaa, eneo la Isyesye – Mbeya Mjini lina mradi wa viwanja 5,000 vipya; na kwa kuwa, umeme ni moja ya huduma muhimu ya kupelekwa huko kwa wananchi wa eneo hilo ambalo waliomba kupatiwa umeme takribani miaka mitatu sasa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme maeneo hayo ya Isyesye?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, japo sehemu kubwa ya Kitongoji cha Isyesye katika Jiji la Mbeya haijapata umeme, baadhi ya maeneo ya Kitongoji hicho tayari yameshapata umeme uliounganishwa kutoka kwenye njia ya umeme ya msongo wa *KV 11* inayotoka katika kituo cha umeme cha Iyunga (Iyunga *Substation*).

*TANESCO* katika Bajeti yake ya mwaka 2009 imetenga shilingi milioni 34 kwa ajili ya kusambaza umeme katika sehemu kubwa ya Kitongoji cha Isyesye likiwepo eneo la soko ambapo wateja wapatao 120 wataunganishiwa umeme na mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2009.

Eneo lililobaki linakadiriwa kuhudumia wateja 40 ambapo kutahitajika kujenga njia ya umeme yenye urefu wa kilometa 1 ya msongo wa KV 33 na kuweka transforma moja ya *KVA 100.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi wa umeme Isyesye ni kati ya miradi iliyopangwa kufadhiliwa na fedha za *MCC* eneo lililobaki litafadhiliwa kwa fedha za *MCC.* Kwa kutambua mradi wa viwanja 5,000 na mahitaji ya umeme yanayotarajiwa, mradi huu umejumuishwa, na Isyesye ni sehemu ya miradi itakayofadhiliwa na fedha za *MCC* kwa maeneo yale ambayo hayajafikiwa na mradi wa awali uliotajwa wa shilingi milioni 34 unaofadhiliwa na *TANESCO* kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Marekani ilitiliana saini na Serikali ya Tanzania kuhusu ufadhili wa miradi iliyo chini ya programu ya *MCC* tarehe 17 Februari, 2008.

Mchakato wa utekelezaji wake ulianza mwezi Novemba, 2008 kwa kuajiri Mhandisi Mwelekezaji *ESBI International* ya Ireland kwa kushirikiana na *Norconsult A. S.* ya *Norway* na *Africare* ya Marekani, ambaye kwa sasa anafanya upembuzi yakinifu ili kuandaa Makadirio hitajika kwa ajili ya kuandaa zabuni kama Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 inavyoelekeza, baada ya tathmini ya gharama kukamilika fedha za mradi zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Isyesye kuwa na subira wakati utekelezaji wa mradi huyo ambao tayari upo katika hatua mbalimbali nilizozitaja ambazo tayari upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kupitia fedha za ndani za *TANESCO* na fedha za *MCC* unavyotekelezwa.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba nikiri kwamba ninapata ushirikiano wa karibu sana na Meneja wa *TANESCO* Mbeya, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu wa kupeleka umeme Isyesye ni wa miaka karibu 5 sasa na kwa sababu *Concentration* ya watu kama alivyosema kwenye eneo la soko linahitaji nguzo 10 tu zifike pale.

Je, isingekuwa vyema sasa kwa Serikali kuhakikisha kwamba umeme unafikishwa pale angalau ndani ya miezi 3 hasa baada ya kuusubiri umeme huo kwa takribani ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa ipo miradi mingi nchini ambayo imekuwa ni ya muda mrefu sana hasa katika Wilaya ya Mbeya ukiwemo mradi wa kupeleka umeme Nyanda za Juu kule Umalila kuanzia Isangati, Isuto, Ilembo, Iwiji ambazo nguzo zilizokuwa zimewekwa zinaanguka na umedumu zaidi ya miaka 10 Serikali inatoa kauli gani juu ya mradi huu wa kupeleka umeme maeneo ya Ilembo na Iwiji, Isuto pamoja Isangati?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba majibu ya swali langu la msingi, tathmini iliyofanywa inaonyesha kwamba Isyesye mbali ya ile *potential* ya *growth* iliyokuwepo ambayo ndiyo maana imefanya vile viwanja 5,000 viwepo. Pale sokoni pana wateja zaidi ya 120.

Kwa hiyo, kwa makusudi hayo basi ndiyo maana Serikali kwa kushirikiana na *TANESCO* ikapeleka shilingi 34 milioni ambazo zinakadiriwa kwamba zitakidhi mahitaji ya wateja hao 120 kwenye eneo hilo ambalo lina *concentration* kubwa ya wateja hapo sokoni wakati tunasubiri utekelezaji wa mradi wa *MCC* kwenye maeneo hayo mengine yaliyotajwa ambayo kusema kweli ni utekelezaji ambao utachukua muda mrefu kidogo zaidi.

Mheshimiwa Mpesya ameomba tuangalie kama katika kipindi cha miezi 3 ijayo mradi huu wa kupeleka umeme Isyesye unaweza kukamilika. Kwenye majibu yangu ya msingi nilisema mradi huu unatarajiwa ukamilike Julai, 2009 ambayo ni miezi 5 kutokea sasa. Kwa hiyo, nimelipokea na mimi nakwenda kuwasiliana na wataalamu wetu kama wanaweza kufanya njia zozote na lakini kama vinginevyo hatuwezi kuliharakisha zaidi na ni tathmini ya kitaalamu kwamba utakamilika Julai, 2009 naomba kusema kwamba tutahakikisha kwamba kwa kuwa umeshaanza kutekelezwa ukamilike kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, hili swali la kupeleka umeme Umalila, Usangati, Iwiji, mimi naomba nilipokee niende nikawasiliane na wataalamu wa TANESCO tujue hali ya sasa hivi ya nguzo na vifaa vingine vilivyowekwa ikoje ili tujue kwamba katika kumalizia huu mradi ni kiasi cha gharama ngapi zitahitajika na ni kazi gani inatakiwa kufanyika ili mradi huu uweze kukamilika halafu nitawasiliana na Mheshimiwa Mbunge na nitamfahamisha.

Na. 49

**Kukamatwa Wanaofanya Hujuma Dhidi ya Maalibino**

Swali lililotajwa hapo juu lilifutwa na Muuliza swali.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ame kwa uungwana huo. Wale wengine wabishi wabishi wangeendelea tu. Ahsante sana. Lakini kwa kawaida watu wa Zanzibar wastaarabu sana. (*Makofi/Kicheko)*

Na. 50

**Askari Wapya Kutakiwa Wasiwe na Familia**

**MHE. USSI AME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwa na utaratibu kwa Askari Polisi vijana wanapoajiriwa hutakiwa kutooa au kuolewa kutokana na Sheria za Polisi:-

Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inaweza kuchangia ongezeko la ugonjwa wa UKIMWI na kuna mpango gani wa kuondokana na utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, Mbunge wa Mtoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa utaratibu wa Jeshi la Polisi Askari Polisi kijana (*Rank and File*) anapojiunga na Jeshi haruhusiwi kuoa au kuolewa mpaka atakapomaliza miaka mitatu ya utumishi wake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu na utumishi katika Jeshi la Polisi si chachu ya askari wetu kuchangia ongezeko la ugonjwa wa UKIMWI. Maambukizi ya UKIMWI hutokana na baadhi ya binadamu kutaka kujiingiza katika ngono zembe na zisizo salama. Kutokuoa au kutokuolewa siyo sababu ya kumfanya kijana kujiingiza katika vitendo vya kuhatarisha maisha yake au ya wengine. Askari hao katika kipindi chote cha utumishi wao Jeshi hupata elimu ya kuepukana na UKIMWI na kuishi katika maadili mema ya kijamii na hata misingi ya imani zao za dini.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haifikirii kurekebisha utaratibu huo, kwani utaratibu huo umelenga kwa vijana hao kutojiingiza katika matatizo yanayoendana na kuwa na familia katika miaka yao ya uchanga wao Jeshini.

**MHE. USSI AME PANDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumwuliza suala moja la nyongeza.

Endapo Askari Polisi amevunja utaratibu huo na akaoa au kuolewa kabla ya miaka 3. Je, ni hatua gani zinachukuliwa kwa askari hao ambao wamevunja utaratibu huo. Ahsante sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Askari Polisi wanapoingia katika Jeshi la Polisi huwa wanachukua viapo na huwa wanakuwa na mikataba na maelewano maalum. Katika masharti ambayo wanakuwa nayo wakati wanajiunga na Jeshi la Polisi mojawapo ni hiyo.

Kwa hiyo, iwapo atakwenda kinyume na utaratibu huo atakuwa amejiondoa katika ajira ambayo atakuwa amekuwepo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa jambo hili la Askari Polisi vijana wanaoajiriwa, kutoruhusiwa kuoa au kuolewa linalalamikiwa sana na Askari husika. Lakini Wizara imeshikilia utaratibu wake huo huo wa zamani japokuwa inavunja Katiba,

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu Ibara ya 16 (1) ambayo inasema kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafasi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba mpaka mwisho”.

Je, Wizara imefanya utafiti wowote kuona kwamba jambo hili la ndoa za askari inaathiri utendaji wa kazi zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Ibara ya 16 ya Katiba haisemi ulivyosema. Hapa nchini hakuna haki ya kuoa au yaani si haki ya kikatiba kuoa na kuolewa ni matashi binafsi kwa maana hiyo wale wanaobaki waseja hawaoi, hawaolewi hawavunji Katiba na kwa hiyo kuidai hapa kama ni haki ya Kikatiba inapotosha Ibara ya 16 inaishia tu kwamba, hifadhi ya maskani, familia na unyumba wake hapa ni kwa maana ya akishakuwa tayari kaoa au kuolewa basi anaheshimika.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango madhubuti wa kusambaza maji katika Wilaya ya Temeke kutokana na mradi wa maji wa Kisima cha Kimbiji na Kisarawe II:-

(a) Je, mradi huo umefikia wapi mpaka sasa?

(b) Je, mradi utagharimu fedha kiasi gani hadi ukamilike?

(c) Je, mfadhili wa mradi ni nani na lini usambazaji wa maji utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi tu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Temeke inapata maji kutoka kwenye mtambo wa maji wa Mtoni na kutoka kwenye visima.

Visima hivyo vilichimbwa na Serikali kupitia *DAWASA* chini ya mradi wa ukarabati na upanuzi wa Miundombinu ya Maji Jijini Dar es Salaam.

Visima hivyo viko Kongowe, Yombo Relini, Makangarawe na Kibedea. Upatikanaji wa Maji kwa maeneo yanayohudumiwa na Mtambo wa Mtoni ni wa mgao kwa hivi sasa kama ilivyo kwenye maeneo mengine ya Jiji la Dar es Salaam.

Maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi wa upatikanaji wa maji ni Tuangoma na Temeke yenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia DAWASA imefanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Kisarawe II.

Visima viwili vya uchunguzi vyenye kina cha mita 250 na 600, sawia vilichimbwa mwaka 2007. Kisima kimoja kina uwezo wa kutoa maji safi na salama kiasi cha mita za ujazo 13,000 kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2009 usanifu kwa ajili ya uchimbaji visima na ujenzi wa mitambo ya kusukuma maji na miundombinu ya kusambaza maji kwa wateja utakuwa umekamilika.

Jumla ya visima 14 vimekadiriwa kuchimbwa ili kupata kiasi cha maji mita za ujazo 182,000 kwa siku ambayo yatatosha mahitaji ya wananchi wa Temeke.

Visima hivyo vitachimbwa kwa awamu kwa kuanzia na visima 6. Ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2009/2010 utekelezaji ambao tayari unaendelea baada ya usanifu na utakamilika ndani ya mwaka mmoja na nusu.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama za awali za mradi huo zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 161 hadi ukamilike.

Gharama hizo zitahusisha uchimbaji wa visima 14 pamoja na miundombinu yake kwa shilingi bilioni 109, ununuzi na ulazaji bomba kwa shilingi bilioni 19, ujenzi wa matanki ya maji kwa shillingi bilioni 3.5 na mitambo ya kusukuma maji na kuvuta umeme kwa shilingi bilioni 29.5.

(c) Mheshimiwa Spika, mradi huo utagharimiwa na Serikali ikishirikiana na washirika wake wa maendeleo chini ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Maji.

Utekelezaji wa mradi huu utaongeza upatikanaji wa maji Dar es Salaam kwa kuwa, maji yanayopelekwa Temeke kwa sasa yataelekezwa kwenye maeneo mengine yenye upungufu wa maji.

Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wakazi wa maeneo husika wakati wa utekelezaji wa mradi huu, utekelezaji ambao unaendelea.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, ni kwamba kwa kuwa hivi sasa kuna mgogoro au kuna malalamiko ya wananchi kuhusu fidia ya ardhi na mazao ambayo imepelekea baina ya *DAWASA* na Serikali yetu ngazi ya Wilaya kutofikia muafaka na wananchi. Je, Wizara ina mpango gani wa kushirikiana na *DAWASA* pamoja na Wilaya kusawazisha tatizo hilo?

Je, Serikali haioni sasa kama tumefikia wakati muafaka wa kutoa fidia kwa mujibu wa bei huria yaani *market value* ili wananchi waweze kupata ridhaa ambayo wanaitaka ambao utaratibu huu Wizara ya Ardhi hivi sasa wanautumia?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa kweli masuala haya yanajitokeza mahali pengi na tunapata matatizo kutokana na wafidiwa kuwa mara nyingi hawawi wa kweli.

Mheshimiwa Spika, kila mkifanya tathimin basi hujitokeza tathimini zingine. Lakini nimwahidi Mheshimiwa Mwinchumu kwamba Wizara inaendelea kutafiti suala hilo na pale ambapo tutajiridhisha kabisa kwamba sasa wafidiwa ni hawa kwa uhakika bila wengine kujitokeza tokeza, basi fidia hiyo itafanyika.

Kuhusu huu utaratibu wa kutoa fidia wa kufuata bei huria sina hakika nimjibu nini Mheshimiwa Mbunge labda niseme kwamba tutaliangalia sisi kama Wizara tutizame Wizara ya ardhi inatumia utaratibu gani kwa kufuata huo utaratibu wa kutazama bei ya soko au bei huria halafu tutaona kinachofaa ili tusije tukaingiza hasara upande wa Serikali na kunufaisha upande mmoja maana vyote ni muhimu kwetu.

Na. 52

**Huduma ya Maji Kigoma na Kibondo**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania ni pamoja na kuwepo kwa huduma bora ya maji; na kwa kuwa mji wa Kigoma na Kibondo kuna ukosefu wa maji kwa muda mrefu:-

Je, Serikali itawasaidiaje wananchi hao ili waweze kuondokana na tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge Viti Maalum, na hongera kwa kuwa Mwenyekiti mpya wa UWT Mkoa wa Kigoma, napena kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kigoma unakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 144,850 Mahitaji ya maji ni mita za ujazo ni 26,000 kwa siku. Lakini maji yanayozalishwa ni mita za ujazo 9,650 kwa siku sawa na asilimia 37 ya mahitaji. Upungufu wa maji Mjini Kigoma unasabibishwa na uchakavu wa mtandao, kuharibika mara kwa mara kwa mitambo ya kusukuma maji, kutokuwepo umeme wa uhakika wa kuendesha mitambo ya kuendesha maji na ongezeko la wakazi.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kibondo unakadiriwa kuwa na wakazi 27,536 Mahitaji ya maji ni mita za ujazo ni 1,600 kwa siku. Lakini maji yanayozalishwa ni mita za ujazo 370 kwa siku sawa na asilimia 22 ya mahitaji. Upungufu wa maji Mjini Kibondo

unasabibishwa na uchakavu wa mitambo ya kusukuma maji pamoja na mabomba yaliyofungwa miaka mingi na kuchakaa na hivyo kupoteza maji mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Kigoma inaandaa mpango wa muda mfupi na muda mrefu wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Kigoma na hatimaye kuondoa kabisa tatizo lililopo mwezi Oktoba,2008.

Wizara yangu iliunda Kikosi kazi cha Wahandisi wa Maji ambao walikwenda Kigoma kufanya tathimini ya hali halisi ya upatikanaji wa maji na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kukidhi mahitaji ya maji ya wakazi wa Mji wa Kigoma Ujiji.

Wataalam hao kwa kushirikiana na uongozi wa Kigoma waliandaa mpango wa muda mfupi ambao unahusisha kukarabati mitambo iliyopo ya kusukuma maji, kununua mitambo mingine miwili yenye uwezo mkubwa, kukarabati mtandao wa mabomba yaliyochakaa na kukarabati transifoma ya umeme yenye uwezo wa *KVA 800* iliyokuwa yameungua. Transifoma hii ndiyo yenye uwezo wa kuendesha mitambo yote ya kusukuma maji. Mpango huu wa muda mfupi unaokadiriwa kugharimu shilingi milioni 457 utaongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 27 hadi asilimia 45.

Hatua iliyofikiwa ni kwamba transifoma hiyo tayari imefanyiwa ukarabati na kufungwa na sasa inafanya kazi. Ununuzi wa mitambo unaendelea kwa kuzingatia taratibu za manunuzi tayari shilingi milioni 457 zimetumwa kwa Mmalaka ya Majasafi na Majitaka Kigoma ili kuendelea na utekelezaji. Wizara yangu inaelewa upungufu wa wataalam wenye sifa na uzoefu katika fani ya maji uliopo katika Halmashauri za Wilaya na Mamlaka za Maji nchini. Kwa kutambua hilo Wizara yangu imetuma Wahandasi kwenda Kigoma kusimamia ufungaji wa mitambo ikiwa ni pamoja na *submersible floating pump* itakayoazimwa kutoka Mwanza. Hata hivyo suluhisho la kudumu la upatikanaji wa maji katika Mji wa Kigoma itapatikana baada ya hali ya umeme kuimarika na hivyo kuwa na nishati ya kutosha kuendesha mitambo ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mji wa Kigoma umefanya majadiliano ya kusaini Mkataba na Mhandisi Mshauri mwezi Oktoba 2008 kufanya uchanguzi na usanifu wa miundombinu pamoja na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuondoa tatizo la maji. Mhandisi Mshauri huyu atafanya pia usanifu wa mradi wa maji katika Mji wa Kasulu na Kibondo. Shilingi milioni 370 zitatumika mwaka huu kumlipa Mhandisi hutu na tayari shilingi milioni zimetumwa Kigoma kwa kazi hii. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kibondo. Fedha hiyo itatumika kununua mitambo miwili ya kusukuma maji, kununua mabomba yatakayotandazwa katika sehemu ambazo mtandao umechakaa ili kupunguza uvujaji wa maji kununu na kufunga dira za maji 100 kwa wateja. Fedha hizo tayari zimetumwa Kibondo ili kuanza utekelezaji. Aidha Serikali imetuma shilingi milioni 10,

kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa mradi wa maji ya mtiririko utakaopeleka maji katika mji wa Kakonko Wilayani Kibondo unaogharamiwa na Kanisa Katoliki kupitia Shirika la *CARITAS* na Serikali ambao kwa pamoja watachangia jumla ya shilingi milioni 478.

Mhesbimiwa Spika, nachukua nafasi hii kulishukuru Kanisa Katoliki kwa mchango huo kwa maendeleo ya jamii.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mara nyingi maji ili yatoke katika Miji ya Kigoma na Kibondo ni lazima umeme uwepo.

Lakini kutokana na ukosefu wa umeme wananchi wameendelea kupata shida sana kwa ukosefu wa maji sasa wakati tunasubiri huo mpango wa muda mfupi na mrefu. Je, Serikali isingefanya utaratibu wa kuchimba visima ili viendelee kupunguza tatizo la maji Miji ya Kigoma na Kibondo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwamba ametambua kuwa kuna mipango ya muda mfupi na muda mrefu ambao kwa taratibu zake zinachukua muda mrefu. Lakini kuhusu suala la visima kwa Mji wa Kigoma na kama unaelewa mji wa Kigoma upo Mlimani. Kwa hiyo, utegemezi mkubwa upo kwenye Ziwa Tanganyika suala ambalo linahitaji maji kusukumwa kutoka Ziwani kiasi cha mita 250 kwenda juu.

Kwa mji wa Kibondo suala la visima linawezekana na mpaka sasa tunaendelea kuboresha upatikanaji wa maji kwa kupeleka pesa kwa ajili ya visima na hivi sasa tumepeleka fedha shilingi milioni 100 kwa ajili ya mitambo. Lakini pia tumepeleka fedha chini ya utaratibu wa *quick win* ambazo hizo ndizo zinafanya kazi ya uchimbaji wa visima.

Na. 53

**Huduma ya Simu za Mezani za TTCL**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa huduma ya Simu za mezani inayotolewa na kampuni ya *TTCL* ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wote nchini pamoja na wale wa Karagwe.

Je, ni lini huduma hiyo itapelekwa katika maeneo yote ya taarifa za Bugene, Nyaishozi, Nyabiyonza, Ndama, Kituntu, Igurwa na Kihanga?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Huduma za simu za mezani za *TTCL* zimeenea katika Makao Makuu ya Wilaya zote nchini. Hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuanza ujenzi wa mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ya aina zote (simu za mezani, simu za viganjani pamoja na mawasiliano ya mtandao –intaneti), simu za viganjani pamoja na mawasiliano ya mtandao –intaneti). Pia *TTCL* hutoa huduma za Takwimu *Broadband*. Ujenzi wa Mkongo unatarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia sasa, na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa simu za mezani zinazotolewa na Kampuni ya *TTCL* ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi ikiwa ni pamoja na wale wa Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Spika, huduma za simu za mezani zinatolewa na Kampuni ya *TTCL* katika Jimbo la Karagwe kwa sasa zinapatikana katika maeneo ya Kayanga na Bugene. Aidha, miongoni mwa mipango ambayo itakapokamilika itasaidia kufikisha mawasiliano katika maeneo yote ya nchi mijini na vijijini ni pamoja na kukamilika kwa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge Serikali inafanya juhudi kupitia Makampuni yote ya simu nchini, kuona uharakishwa wa usambazaji wa mawasiliano ya simu nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Karagwe.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nataka kusema kwamba hii ni ahadi ya pili Serikali inatoa kwa Jimbo la Karagwe. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, yupo tayari kuhakikisha kwamba Serikali ina harakisha mpango huu kwa huduma za simu za mezani na mkoni zinafika maeneo yote ya ya Karagwe kabla ya mwaka 2009?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swala la nyongeza la Mheshimiwa Blandes kama ifuatavyo:-

Sipendi nimhakikishie kwamba kabla ya 2009 mawasiliano ya simu yatafika katika maeneo yote ya Karagwe. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kwamba tutaendelea kuwasiliana na makampuni ya simu lakini pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba shughuli hizi za mawasiliano zinafanyika na ndiyo maana kule kwake mawasiliano ya aina zote yanapatikana. Kuna maeneo tu mengine ambayo hayajafika mawasiliano ya simu hamu yake ni mawasiliano ya simu ya *TTCL* kitu ambacho kitafika karibuni baada ya huu mkonga kuanza, mkonga ukianza leo hauwezi kumalizika leo

Mheshimiwa utamalizika 2010 ndiyo mawasiliano yatasambaa katika maeneo yote nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo nikianza na wageni kwa furaha na ni heshima kubwa kutambulisha kwenye *Speaker's Gallery* Mheshimiwa Balozi wa Sweden katika nchi yetu Mheshimiwa Stephan Haston pamoja na Msaidizi wake. *Once again welcome to the House in Dodoma Excellence Ambassador. We very much value the excellent relation between Tanzania and Sweden for since independence we have been a true friend and it is very nice to interrupt with you thank you very much.(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi ambao wamo katika mafunzo ya vitendo katika Taasisi ya Uhasibu sijui ya wapi hii labda ya Dar es Salaam, ni wafuatao nitawataja wasimame ili Waheshimiwa wabunge waweze kuwatambua.

Ndugu Mwakabuku, Dr. Deo Richard, Ndugu Tembei Abela, Ndugu Kigundu Rogas, Ndugu Jastin Boniface, Ndugu Julius Bura sijui ana uhusiano wowote na Mbunge mwenzetu hapa ahsante sana. Karibuni sana tunawatakia mafanikio katika masomo yenu.

Wapo pia wanafunzi wa Mahakama kuu ya Tanzania au Chuo cha Sheria *anyway* waliopo Bungeni kujifunza jinsi ya kutayarisha *HANSARD* wanasindikizwa na Bwana Prophil Lyimo, Msajili wa Mahakama, yule pale ahsante sana, karibu sana Mr. Lyimo. *(Makofi)*

Sasa wanafunzi ni David Mashenene, Saada Moshi, Janeth Mwamanga, Lucy Kilawe, Frida Ayuke na Jasmin Kichawele.

Hapo uwiano umeelekea asilimia 90 ni wanawake (*Makofi*) Kwa hiyo, mambo makubwa haya.

Wageni kutoka *Bank* ya *NMB,* Meneja wetu Kanda ya Kati maarufu sana Ndugu William Kilula yule pale ahsante. Kwa huduma sijatumia sana hii *ATM* hapa ofisini kwetu nadhani kama ina matatizo hebu irekebishe.

**WABUNGE FULANI:** Haipo?

**SPIKA:** Haipo, haya sasa hakuna *ATM* sasa wewe. (K*icheko*)

Nilianza kukusifia kumbe. Bwana Felix Nyaluko *Chief Operating Officer NMB* Makao Makuu Dar es Salaam, *this name sounds I don't thing Tanzanians may be from Tarime may be I don't know. But we are happy to receive you and MP's are claiming for an ATM for better service in NMB Branch within the Bunge Complex.* Yupo pia Bwana Colman Kiwia Meneja *NMB* hapa Dodoma ahsante sana karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Matangazo ya kazi, Mheshimiwa Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi mkutane leo tarehe 30 Januari, 2009 katika ukumbi Na 231 saa tano asubuhi mara baada ya kipindi hiki cha maswali. Kwa hiyo, Kamati ya Fedha na Uchumi saa tano kamili ukumbi na 231 leo.

Mheshimiwa William Shelukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini anahitaji Wajumbe wote wa Kamati ya Nishati na Madini mkutane leo saa saba mchana ukumbi na 227. Kwa hiyo, Kamati ya Nishati na Madini saa saba mchana ukumbi na 227.

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo Mifugo na Maji anahitaji kuwepo Kikao cha Kamati hiyo ya Kilimo Mifugo na Maji saa tano asubuhi hii ukumbi na 227.

Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anatoa wito kwa wajumbe wa Kamati ya Miundombinu muwe na kikao leo saa tano asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa. Sijui humu ndani tutabaki wajumbe wangapi.

Mheshimiwa William Masilingi, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anahitaji Wajumbe wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama mkutane saa tano na dakika kumi na tano ukumbi na 219. Kwa hiyo, Kamati hii ni saa tano na robo ukumbi namba 219.

Mheshimiwa Omary Kwaangw' kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya masuala ya UKIMWI anahitaji wajumbe wote Mkutane saa tano asubuhi katika eneo la *Speaker's lounge.*

Sijui nani amewaruhusu kukutana *Speakers Lounge* bila idhini yangu. Nadhani basi wamefanya kosa lakini leo nawasamehe, huwezi kuvamia tu *Speaker's Lounge* kama vile ni sebule tu ya kawaida. Lakini basi kwa leo nawasamehe hawa. (K*icheko*)

Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, afadhali huyu anatoa notisi ya kutosha. Kamati ya Hesabu za Serikali Kesho 31 Januari saa nne asubuhi ukumbi na 231, mkumbuke tuna semina. Kwa hiyo, labda muwe na kikao kifupi ili mfaidike na Semina.

Mheshimiwa Eliata Switi, Katibu wa *TWPD* anaomba waheshimiwa Wajumbe wa Chama cha *TWPD* kwa maana hiyo Wabunge wote wanawake saa saba mchana ukumbi namba 428. *TWPD* saa saba mchana ukumbi na 428.

Tangazo la semina Waheshimiwa Wabunge kama tulivyotangaza awali katika *breafing* kesho tarehe 31 Januari kutakuwa na Semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote itakayoanza saa tatu asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa Semina hii ni nzito, nzuri inahusu Sera ya Taifa ya Umwagiliaji imeandaliwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Itifaki zote zimezingatiwa.

Huo ndio mwisho wa matangazo, Katibu tuingie katika hatua nyingine. *(Makofi)*

## Hoja Binafsi ya Mbunge

### Hoja Kuhusu Kuvunjwa kwa Haki za Bu nge

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kutumia nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa hoja binafsi chini ya Kanuni Namba 51 ambayo inasomeka kama ifuatavyo:-

Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na Haki za Bunge atafanya hivyo wakati anaona unatoa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge uliowekwa na Kanuni hizi na atakuwa amemwarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake la kutoa hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimeona ni wajibu wangu kwa niaba ya Wabunge wote kuleta hoja hii kwa sababu lazima kazi ya kwanza ya Wabunge ni kulinda hadhi ya Bunge lenyewe na maamuzi ya Bunge yanatakiwa yaheshimiwe na kuzingatiwa bila kupuuzwa.

Jana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alitoa maelezo kuonyesha kwa nini Wizara imeshindwa kutelekeza Azimio la Bunge na kusababisha Wizara kuongeza muda wa Umiliki wa vitalu kwa muda wa miaka mitatu ijayo wakati Azimio lilikuwa linaitaka Serikali kutekeleza na ilikubaliwa iwe mwaka huu 2009.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Waziri mwenyewe alisimama na akasema kwa moyo wa dhati kabisa kwamba watatekeleza Azimio la Bunge. Nakutokana na kuthibitisha kwake kwamba atatekeleza Azimio la Bunge mimi nilitarajia kwamba wanapoona kuna tatizo basi Waziri huyo angekuja Bungeni kuja kulieleza Bunge kuonyesha kwanini hataki kutekeleza Azimio la Bunge.

Lakini nataka nieleze kwamba ninavyoamini mimi Wizara haijashindwa kutekeleza Azimio la Bunge. Wamebadilisha uamuzi wa Bunge kwa msukumo na wamiliki wa vitalu. (*Makofi*)

Nina ushahidi nimeutoa kwenye Azimio, barua mmeiona ambayo imeambatanishwa. Kwa hiyo, serikali imeongeza muda wa kumiliki vitalu kwa matakwa ya wamiliki wa vitalu maana waliandika barua kuomba uongezwe muda.

Kwa hiyo, kwa maelezo hayo siyo kwamba Serikali imeshindwa kutelekeza Azimio. Hilo ndio jambo kubwa la msingi; lakini vilevile ningependa kusema kwamba

Wizara hiyo hiyo mwaka 2006 iliunda Kamati ya wataalamu na bahati nzuri mimi na Mheshimiwa Ndugai tulikuwa Wajumbe, na walitaka tukamilishe kazi hiyo haraka iwezekanavyo tukakamilisha kazi hiyo 2006. Baadhi ya mapendekezo yaliyokuwa sehemu ya Azimio la Bunge yalitokana na mapendekezo ya Kamati hiyo. Vilevile miaka 10 iliyopita Mheshimiwa Marmo aliwahi kuongoza Kamati ya Bunge na iliweka mapendekezo mpaka leo bado yapo kwenye makabati.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kwamba kuna tabia ya kuwa na Kamati na maamuzi lakini hayatekelezwi. Nia ya hoja hii sasa ni kuweka nguvu kwamba maamuzi yanapofanyika lazima yatekelezwe vilevile na hakuna kutafuta visingizio. Kamati yetu iliwasilisha Taarifa kwa Wizara mwaka 2006 mapema kabisa na ilipokelewa wakati ule nia ilikuwa ni kwamba kwa kuwa ni 2006 Wizara ipate nafasi ya kujiandaa katika kipindi cha miaka mitatu kabla ya 2009. Lakini zikaanza vurugu palepale migawanyiko Wizarani haikuanza kutekelezwa. Kwa hiyo, hakuna hoja ya msingi kusema Wizara haiwezi kutekeleza.

Mheshimiwa Spika katika maelezo ya jana ya Waziri pia alieleza kwamba baadhi ya mambo yaliyosababisha Wizara isitekeleze jambo hili Azimio la Bunge ni kwamba kulikuwa na mgawanyiko, kulikua na matatizo kati ya Wizara na makampuni ya uendeshaji na kwamba Wizara ilipelekwa Mahakamani.

Jambo hilo mimi ninavyoona Serikali haijawahi kushtakiwa, lakini wamiliki wa vitalu waliomba Serikali ipunguze bei ya tembo, simba, na chui na kuongeza bei ya wanyama wengine ili kufidia bei ambayo ilikuwa imewekwa wakaona ni ya juu kwa wanyama hao watatu na Serikali ikakubali na vitalu pia vikapunguzwa bei ingawa Bunge lilikuwa limekubali na kupitisha kwamba bei zitakuwa Dola 40,000 na 50,000.

Lakini Wizara baadaye walikubaliana na uwindaji ikawa Dola 28,000. Kwa hiyo, nalo pia halikuwa si tatizo maana Wizara ilikubaliana na wamiliki hawa.

Mheshimiwa Spika Wizara ili kutekeleza vizuri na kwa ufanisi Azimio la Bunge waliunda *task force* ya wataalam ikiongezwa na Mwenyekiti kutoka Chuo Kikuu mtu makini kweli na wenzake waliokuwa ndani ya *task force* watu makini wakaishauri Serikali namna ya kutekeleza lile Azimio na kuhusu muda wa umiliki wa vitalu, naomba ni-*quote*, nisome, mapendekezo ya *Task Force* kwa Wizara, *recommendations*, wanasema, limeandikwa kwa Kiingereza, naomba niisome hivyo hivyo. Inasema hivi: *"The transitional period should cover a period of two years, year 2009 and year 2010. This means that the Government should consider extending the current lease of Blocks to outfitters from five to six years, that's to say from 2004 and year 2010"*. Hii ni Kamati, ni Kamati ya Wizara wenyewe wameipendekezea, wao wamekwenda kuongeza mpaka 2012. Sasa kwa nini uweke watalaam wa kukuisadia na ufanye tofauti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema, jambo hili limefanyika kwa msukumo. Kitu ambacho lazima niseme kutoka moyoni mwangu *(from my heart)*, napata shida tunaposukumwa na Wazungu katika mambo ya nchi yetu. Ile *TAHOA* inamilikiwa na Wazungu, ile na ndio wenye vitalu vizuri kuliko Watanzania na wana nguvu ya ajabu.

Waziri jana amesema kwamba, ooh, unajua kulikuwa na suala la mkataba. Nashangaa Wizara hii kila siku wanang'ang'ania jambo la hovyo, hakuna mkataba, kuna kitu kinasema maelewano. Maelewano yale ya miaka kumi iliyopita bado wanang'ang'ania kama ni mkataba. Tungeweza kuleta makaratasi yale mkasoma Waheshimiwa, itazua tena ajenda nyingine. Kwa hiyo, naomba Serikali tusing'ang'anie jambo hili, ni chafu ule siyo mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya maelezo hayo, na bila kuwapotezea muda, nataka niseme tena kwamba itakuwa ni vizuri sana Maamuzi ya Bunge kila wakati kuzingatiwa, vinginevyo tutaondoa maana kabisa ya kuwa na Bunge na linaloendeshwa kwa Kanuni. Bunge siyo *Ward C. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nisome Azimio. Chini ya Kanuni ya 51 na 54, Toleo la Kanuni za Kudumu la mwaka 2007.

KWA KUWA katika Mkutano wake wa Kumi na Moja, Bunge hili lilijadili hoja kuhusu uwindaji wa vitalu vya uwindaji wa wanyapori na bei zake ambayo muda wake unakwisha 2009.

NA KWA KUWA baada ya kujadili hoja hiyo, Bunge liliazimia kwamba ili kuiwezesha Serikali kuongeza mapato na kuweka uwiano, uwazi, usawa katika ugawaji wa vitalu hivyo vya uwindaji wa kitalii, Serikali ianze mchakato wa kugawa upya vitalu vyote vya uwindaji nchini ambavyo muda wake wa umiliki unakwisha 2009.

NA KWA KUWA Bunge liliazimia pia kwamba kwa kuzingatia kuwa muda wa kumiliki vitalu vya uwindaji ulikuwa unakoma mwaka 2009 na kwamba kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya maliasili na wanyamapori kwa pato la Taifa, Serikali iweke mikakati maalum ya kukamilisha utekelezaji wa Azimio la Bunge katika muda uliobakia wa umiliki wa vitalu hivyo vya uwindaji.

NA KWA KUWA Azimio hilo la Bunge kimsingi lilikusudia kuwa vitalu vyote vya uwindaji wanyamapori hapa nchini vigawiwe upya ili wamiliki wapya waanze kuvitumia ifikapo mwaka 2010 baada ya muda wa wamiliki wa sasa 2009 kwisha.

NA KWA KUWA lengo lingine mahsusi la Azimio la Bunge lilikuwa ni kuliwezesha Taifa letu kupata mapato zaidi kutokana na shughuli za uwindaji wa kitalii wa wanyamapori kwa kuvigawa vitalu vikubwa na kupata vitalu vipya 89 vilivyogawanywa kwa ngazi 55 na 34.

NA KWA KUWA pamoja na Waziri kuahidi kwa dhati hapa Bungeni kwamba Serikali ingezingatia na kutekeleza ipasavyo Azimio lililopitishwa na Bunge ikiwa ni pamoja na kuandaa Muswada wa Sheria mpya ya Wanyamapori itakayosimamia shughuli zote za ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa wanyamapori, Serikali imeamua kuongeza muda wa umiliki wa vitalu hivyo kwa miaka mitatu kwa utaratibu wa zamani ambao unaileteа Serikali hasara kwa kiwango cha dola 12,330,000 kama tukiitekeleza sasa.

NA KWA KUWA kitendo hicho cha kuongeza muda wa umiliki wa vitalu kinakiuka na kutokuzingatia Azimio la Bunge kuhusiana na ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa wanyamapori.

NA KWA KUWA maelezo ya Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii katika hakawia yake aliyotoa Bungeni kwamba Serikali ina makubaliano na Chama cha Wawindaji (TAHOA), hayana msingi wowote kwa sababu makubaliano hayo kwa kweli siyo mkataba.

NA KWA KUWA kutokutekeleza Azimio la Bunge kumetokana na matakwa ya wawindaji kupitia TAHOA kwa ushahidi wa barua ya Wizara ambayo imewajibu kuwa maombi yao yamekubaliwa muda wake kuongezwa.

NA KWA KUWA Wizara imeandaa Muswada ambao unawasilishwa mbele yetu leo Bungeni, kitendo cha kuongeza muda wa miaka mitatu ya uwindaji zaidi, itafanya sheria hiyo isifanye kazi yake mpaka baada ya muda huo wa miaka iliyoongezwa.

NA KWA KUWA kitendo chochote cha Serikali kuingia katika mchakato wa kutokutekeleza Azimio la Bunge kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji wanyamapori ni kuingilia Madaraka ya Bunge na kukiuka Haki za Bunge

KWA HIYO BASI napenda kutoa Maazimio yafuatayo:-

Kwanza, kwamba barua ya Wizara ya Maliasili na Utalii Kumb. Na. HD204/401/100 ya tarehe 16 Januari, 2009 inayoongeza muda wa umiliki wa vitalu vya uwindaji wa wanyamapori kwa makampuni ya uwindaji kwa kipindi cha miaka mitatu hadi 2012 ifutwe mara moja kwa kuwa inakwenda kinyume na Azimio la Bunge (ndiyo msingi wake). *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii hakulipa suala hili mwongozo mzuri, Bunge linakemea tabia hiyo ambayo athari yake ni kuleta mtengano kati ya mihimili miwili, Bunge na Utawala.

Tatu, ili kujenga ushirikiano kati ya mihimili miwili, Bunge na Utawala, ni busara kwa Wizara za Serikali kuzingatia mawasiliano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya mihimili hiyo miwili. Sasa tuulinde!

Mwisho, kwa kuzingatia hali halisi ilivyo sasa, na kwa kuwa, Wizara imechelewa utekelezaji wa Bunge, ninapendekeza kwamba ushauri wa kitaalam uzingatiwe ili vitalu hivi viwe vimekamilika na kupewa kwa wawindaji wapya mwaka 2010 na siyo 2012.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa hiyo kwa taratibu za Kibunge itabidi muiamue. Nimepokea majina ya wachangiaji wanne, lakini kwa utaratibu wa hoja kama hizi ambazo zinadai jibu kutoka Serikalini, nafasi ya kwanza nitaitoa kwa Mheshimiwa Waziri mhusika, Waziri wa Maliasili. Baada ya hapo nitapima kama kuna haja ya kuendelea na wote hawa kwa sababu tuna Muswada pia unakuja. Kwa hiyo, wapo Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi na Mheshimiwa Aloyce Kimaro. Nitapima kulingana na jinsi Serikali itakavyosema. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kukiri kwamba Serikali iliahidi kufanyia kazi Azimio la Bunge kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii na bei zake ambavyo muda wake kisheria unakwisha mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoa maelezo yangu ya msingi kupitia kauli ya Serikali kuhusu taarifa ya utekelezaji wa Bunge jana, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu kipindi cha mpito cha mgawo wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kutoa ufafanuzi wa utekelezaji wa Azimio la Bunge, kwa ridhaa yako, naomba pia ninukuu maamuzi ya Bunge yaliyotolewa kupitia Azimio hilo. Nanukuu; “Hivyo basi, ili kuondoa kasoro zote zilizojitokeza na kuwezesha Serikali kuongeza mapato na kuweka uwiano, uwazi na usawa katika ugawaji wa vitalu vya uwindaji na uwindaji wa kitalii, Bunge linaazimia kuwa:-

Moja, kwamba Serikali ianze sasa mchakato wa kugawa upya vitalu vyote vya uwindaji nchini kwa kuzingatia mapendekezo yaliyomo kwenye kiambatanisho (a) cha hoja hii.

Mbili, kwamba kwa kuzingatia kuwa muda wa kumiliki vitalu vya uwindaji utakwisha mwaka 2009 na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya maliasili, ya wanyamapori kwa pato la Taifa, Serikali iweke mikakati maalum ya kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye aya ya 1.1 hadi aya ya 3.3 ya kiambatanisho (a) cha hoja hii katika muda uliobakia wa kumiliki vitalu hivyo”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya nukuu hiyo na kwa kutambua kuwa wakati Bunge linapitisha Azimio hilo, Serikali ilikuwa kwenye mchakato wa kupitia Sheria ya Wanyamapori, Serikali ilichukua hatua ya kutekeleza maagizo hayo ya Bunge kwa kuweka mikakati itakayowezesha vipengele vilivyobainishwa katika Azimio hilo vinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Azimio, Serikali kwa kuzingatia kifungu cha 47 cha Sheria ya Tafsiri, Sura namba 1 na kifungu namba 16 sehemu ya 5 cha Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2000 na marekebisho yake, Serikali

ilichukua hatua ya kuweka kipindi cha mpito kama sehemu ya mikakati maalum ya kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha mpito kinajumuisha mwaka mmoja wa kukamilisha sheria, kanuni na miongozo ya kusimamia shughuli za uwindaji wa kitalii na miaka miwili ya kuruhusu mauzo ya safari za uwindaji kulingana na Kanuni ya 10 ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za mwaka 2000. Kwa msingi huo, kipindi cha mpito kilichotolewa kimewekwa ili kuwezesha mgawo wa kipindi cha miaka mitano utakaozingatia mapendekezo ya Azimio la Bunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo niliyoyatoa kwenye kauli ya Serikali niliyoitoa jana, naomba kuchukua fursa hii kueleza ya kwamba Kikundi kazi nilichokiunda *(Task Force)*, kilitoa mapendekezo kadhaa ya kutekeleza Azimio la Bunge likiwemo na pendekezo la kipindi cha mpito ambapo kulitolewa kipindi cha mwaka mmoja, yaani katika mwaka huu mmoja, ni kwamba vitalu vigawiwe mwaka 2010, na hivyo Wizara yangu iliafiki kabisa na tumeheshimu pendekezo tulililoletewa na Kikundi kazi na tumezingatia hayo yote jinsi ya kutekeleza. Katika kutekeleza hayo katika mwaka mmoja ni kwamba, mwaka 2009 na 2010 ni kuipa fursa Serikali kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kukamilisha mchakato wa Sheria mpya ya Wanyamapori na kuandaa kanuni husika. Kwa hiyo, kipindi hicho ni sasa 2009 hadi 2010 tutahakikisha kwamba sheria kama ikiwa Wabunge watairidhia, itaanza mchakato wake na kutengeneza kanuni zake.

Pili, kukamilisha tathmini ya vitalu vya uwindaji wa kitalii na kuvipanga katika madaraja kulingana na ubora wa rasilimali zilizopo. Mheshimiwa Spika, ni kazi mojawapo tuliyopewa katika Azimio la Bunge kwamba vitalu vifanyiwe tathmini upya na kazi hiyo tumeianza tangu mwaka jana. Lakini wakati nilipoongea hapa hapa ndani ya Bunge lako Tukufu wakati wa kipindi cha bajeti, ni kwamba kazi hii hatukujua itachukua muda gani.

Mheshimiwa Spika, lakini, baada ya kulipa kazi Shirika letu la TAWIRI, ndipo walitufahamisha kwamba kazi hii itachukua miaka miwili, tathmini ni kubwa mno kwani inabidi waangalie vitalu vyote upya, pia watathmini aina ya wanyama na ubora wa wanyama na viweze kugawiwa kwa kufuatana na ukubwa wa kitalu. Kazi zote hizo tulikabidhiwa kama mojawapo ya Azimio la Bunge. Kwa hali hiyo basi, kazi hii inachukua miaka miwili, kuanzia mwaka jana 2008 na mwaka huu 2009 wametuhakikishia hawa watalaam kwamba Desemba 2009, kazi hii itakuwa imemalizika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mwaka huu hadi mwanzoni mwa mwaka ujao, kazi hizo mbili tutakuwa tumezikamilisha za Azimio la Bunge. Baada ya hapo kukamilisha taratibu za kugawa vitalu kwa kuweka mfumo wenye uwazi, uwajibikaji na kuzingatia uhifadhi endelevu, na hii ni kazi ambayo ni muhimu na ambayo pia tumeagizwa na Azimio la Bunge kwamba sasa vitalu vigawiwe kwa kufuata uwazi na uwajibikaji na tuzingatie pia uhifadhi endelevu. Hiyo nayo pia itachukua muda katika maandalizi hayo na ndio sababu kabisa tumekubali pendekezo la *Task Force* kwamba

mwaka 2010 ndio tugawe vitalu, kwa hiyo sasa hivi iongezwe *extention* ya mwaka mmoja, hilo tumekubali kabisa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kufuatana na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, Sura 283, kanuni za uwindaji wa kitalii za mwaka 200 na marekebisho yake, vitalu vya uwindaji wa kitalii vinagawiwa miaka miwili kabla ya kumaliza kipindi cha uwindaji ili kuwezesha kampuni kufanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Kampuni zitakuwa zimegawiwa vitalu mwaka 2010 zitapata fursa ya kujipanga ili kuuza safari Ulaya na Marekani.

Mheshimiwa Spika, pili, Kampuni mpya zitapata fursa ya kununua zana na vifaa vya uwindaji, kuchagua wawindaji bingwa wa Tanzania na kuwajengea uwezo wa mafunzo na kujenga uaminifu na imani kati ya kampuni na wawindaji.

Mheshimiwa Spika, tatu, Kampuni mpya za Kitanzania kuingia kwenye ushindani wa soko la dunia ambapo Tanzania ina ushindani mdogo kutokana na kuwa na bei za juu za uwindaji na vile vile kuwezesha kurudisha soko la Tanzania, wateja waliochukuliwa na nchi shindani.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo ndiyo sababu kuna kipindi hicho ambacho kisheria kimewekwa, tukishagawa vitalu wapate miaka miwili ya kujiandaa katika mambo haya na ndio sababu kuna ile miaka miwili, baada ya 2010, tukishagawa vitalu, 2011 na 2012 wanaingia katika kazi ya maandalizi haya na haya yamewekwa kwenye sheria na nimeieleza sheria ni kifungu gani.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba kwa dhamana niliyopewa katika Wizara hii, isingekuwa busara kuifanya Serikali kwenda likizo ya kupata mapato na kutoa ulinzi stahili wa rasilimali ya wanyamapori na mazingira yake nchini. Kwa hali hiyo, na kwa kutambua Azimio hili lilitokana na Bunge na kwamba Kamati za Kudumu za Bunge zimeundwa ili kulisaidia Bunge lako Tukufu katika utekelezaji bora wa madaraka yake, Wizara yangu ilifanya mawasiliano na kupeleka suala hili kwa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira katika kuwaomba waridhie kipindi cha mpito kwenye kikao kilichofanyika ofisi za Bunge, Dar es salaam tarehe 12 Januari, 2009. Hata hivyo, nikifahamu ya kwamba suala hilo baadae nitalileta katika Bunge lako Tukufu na kuweza kutoa taarifa kwamba tuliomba ruhusa hiyo kwa Kamati kwa sababu lilikuwa ni jambo la dharura na nisingeweza kuliacha kwa kuwa hili lingetusababishia Serikali kupoteza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu barua iliyoandikwa na Wizara yangu kwa wadau, hii ilikuwa kuwawezesha wadau hawa wenye vitalu waweze kupewa ruhusa ya kuuza safari zao huko kwenye soko la dunia kwani ni sheria kwamba uthibitisho kutoka katika nchi yenye vitalu uwe umetolewa kwa wale wote wanaokwenda kuuza safari ndipo waweze kuruhusiwa kuuza.

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako, naomba kutoa mfano jinsi soko la uwindaji wa kitalii linavyoweza kuathirika kutokana na kampuni za uwindaji kutokuwa na uthibitisho wa umiliki wa vitalu. Katika maonyesho makubwa kuliko yote duniani ya uwindaji wa kitalii ambayo hufanyika mwezi Januari kila mwaka Jijini Rino Nevada nchini Marekani. Mwaka huu wakala na wamiliki wa kampuni za uwindaji kutoka Tanzania wasingeweza kuuza safari za uwindaji bila kuwa na uthibitisho wa kumiliki vitalu, hivyo, barua iliyotolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori iliwapa uhalali wa kisheria ili hawa wawekezaji kutoka Tanzania waweze kufunga mikataba na wateja kwa mauzo ya safari za uwindaji kwa mwaka 2010 na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kusema kwamba, kama nilivyoeleza hapo awali, utekelezaji wa Azimio la Bunge kuhusu ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii na bei zake ulikuwa umejikita kwenye marekebisho ya sheria ya wanyamapori. Hivyo basi, kwa maelezo hayo niliyoyatoa, mchakato wa kutekeleza Azimio hilo umeanza na kwamba Serikali haijachukua hatua yoyote ya kulidharau Bunge lako Tukufu, iliyafanya yote hayo kwa nia njema bila kuwa na dharau ya aina yoyote. Ila napenda pia kusema kwamba, naomba kuliomba Bunge lako Tukufu radhi kwa ufahamu wangu niliokuwa nao kwamba baada ya kuwaomba ruhusa Kamati ya Ardhi na tukajieleza na wakaelewa na ilikuwa ni kitu cha dharura, basi nilifahamu kwamba hiyo ilitosha kutekeleza hii dharura na baadae Januari tutakapokuja Bungeni ili kuweza kutaka radhi Bunge na kuwafahamisha kilichotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari kukubaliana na Azimio ya kwamba kipindi cha mpito kifutwe, isipokuwa kama Serikali itafanya hivyo kwa kukubaliana na hilo, naomba kusema ya kwamba Serikali isingeweka kipindi cha mpito na kukubaliana kwamba hivyo vipindi vya miaka miwili vifutwe mara moja, athari mbalimbali zingeweza kujitokeza zikiwemo zifuatazo:-

Kwanza, uwezekano wa baadhi ya wadau kwenda Mahakamani kudai kuwa sheria imekiukwa na hivyo kuchelewesha mkakati mzima wa utekelezaji wa Azimio la Bunge.

Pili, watalii wa uwindaji kuisusia Tanzania na kurudisha nyuma juhudi za nchi katika kutangaza utalii, kufaidika kutokana na mapato ya uwindaji wa kitalii. Kwa mfano, katika mwaka 2007, Serikali iliongeza viwango vya ada za uwindaji na kulenga kukusanya takriban bilioni 50 ambazo ziliingizwa kwenye mpango wa nchi wa matumizi kwa mwaka huo. Matokeo yake, wawindaji walisusa kuja nchini ambapo Serikali iliweza kukusanya kiasi ambacho hakikuzidi bilioni 19, ikiwa ni pungufu ya zaidi ya shilingi bilioni 30 ya malengo tuliyokuwa tumejiwekea. Hali hii ilisabaisha kuvurugika kwa mipango ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, pia athari nyingine inaweza ikatokea ni kuongezeka kwa ujangili kutokana na ukosefu wa mapato na kukosekana kwa ushiriki wa kampuni za uwindaji katika uendeshaji wa shughuli za doria.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda tena kusema kwamba, kuhusu makubaliano *(consensus)* ambayo yaliwekwa na Wizara yangu mwaka 1994 na ambayo

kwa kufuatana na makubaliano ilikuwa yaishe mwaka 2014. Moja kwa moja nilikataa hiyo *consensus*, hata Kamati ya Bunge niliifahamisha na pia hata wadau wenyewe niliwafahamisha kwamba Wizara yangu haitambui hiyo na hali ndivyo ilivyo hivyo, hatuitambui hiyo *consensus* na hata tulipopanga hiki kipindi cha mpito, hakina uhusiano na *consensus* na hakuna popote tumeweka kwamba tunazingatia kwamba *consensus* tunaikidhi matakwa yake. Tulichokifanya ni ile kuona hali halisi ya utekelezaji wa Azimio la Bunge ukoje na ndio sababu tukafikia uamuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena nirudie kwa kumaliza kwamba Wizara yangu na hata Serikali hatukuwa na nia mbaya yoyote ya kulidharau Bunge lako Tukufu na pia tulifanya hivyo kwa nia nzuri ya kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Azimio unakwenda sambamba na tuweze kumaliza mapema, tuingie katika awamu mpya ya utekezaji wa shughuli zote hizo

Mheshimiwa Spika, narudia tena, naomba radhi ikiwa kwa yoyote yale tuliyoyatekeleza kwa nia nzuri, lakini ni kwamba kwa ufahamu mdogo yameleta mtafaruku ambao umesababisha mpaka kuja hoja hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla hujaondoka, nikuelewe kwamba Serikali inashikilia kwamba ni vema vitalu vigawiwe mwaka 2013? Ndiyo hivyo? Hapana, namuuliza Waziri, sikuulizi wewe!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kusema kwamba, kwa kufuatana na hoja nilizozisema, nimesema ya kwamba Serikali tuko tayari kukubaliana na uamuzi ambao hoja imetolewa kwamba tufute mara moja, tuko tayari kufuta mara moja, isipokuwa nimewafahamisha Waheshimiwa Wabunge, kama tutafuta, kuna athari hizo, lakini baada ya hapo kama Wabunge wataridhia, sisi tuko tayari kufuta.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea sasa, naona itabidi watu wachangie tu, nilidhani jambo ni fupi, la kuelewana. Ahsante Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, labda sikueleweka, labda nirudie tena, kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Sawa sawa!

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kwa kufuatana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye Azimio, nimefanya mambo mawili, kwanza, nimeomba radhi kwamba hatukulidharau Bunge na jambo la pili, nimesema kwamba Serikali iko tayari kukubali kwamba hicho kipindi cha mpito kifutwe mara moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kusaidia Bunge, hebu niliweke vizuri tu. Nilidhani tatizo lililopo hapa ni kwamba Serikali inaelekea kung'ang'ania hiki kipindi cha 2009 wala kisihesabiwe kwamba ni mpito, ndiyo maana kinaongezeka sasa, kwa nini inaongezwa inakuwa 2009, inachukuliwa tena 2010, 2011, 2012 kwanza kwa hesabu zangu ni miaka minne wala siyo mitatu, ndiyo! 2014 ukianzia 2009 si inakuwa miaka minne?

Hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya ni kwamba 2009, 2010 vinatosheleza hii miaka miwili kuwa imetoa *notice* ambayo inatakiwa kwenye sheria na kwamba uwindaji sasa ule wa mfumo mpya uanze 2011 siyo 2013 ndiyo hoja imekaa hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo namwita sasa Mheshimiwa Mpendazoe, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kueleza kwamba naunga mkono hoja na mapendekezo yote yaliyotolewa. Nimesikiliza Mheshimiwa Waziri akieleza, lakini katika kuunga mkono hoja na mapendekezo yote yaliyotolewa katika hoja hiyo, naomba nieleze yafuatayo: Kwanza, katika kuchangia hoja yangu na katika kuunga mkono, naomba tu nieleze historia ndogo ya Israel, tunafahamu Israel ni nchi nzuri katika Biblia, tunaifahamu ilivyo kwamba ilikuwa ni nchi nzuri yenye asali na maziwa, Mungu alikusudia nchi ile iwanufaishe wana wa Israel lakini baada ya muda, baada ya Israel kupata mmonyoko mkubwa wa maadili nchi ile iliyojaa asali na maziwa haikuwasaidia wana wa Israel, utajiri huo wa Israel ukawa unaliwa na wageni na wana wa Israel wakitazama na kushangilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Isaya Sura ya 1, mstari wa 1-14, Isaya ilibidi atumwe na Mungu kuwaeleza wana wa Israel kwamba nchi yenu nzuri iliyojaa asali ya maziwa, inaliwa na wageni na nyie mnaangalia na kushangilia, lakini Isaya akawaambia kuna mabaki ya wana wa Israel ambao wamesaidia nchi yenu, kama isingekuwa mabaki hayo, nchi ingeliwa na kuisha ikawa kama Sodoma na Gomora. Nchi yetu ya Tanzania inao utajiri mkubwa sana, madini yako ya kutosha, yangetosha kuwafanya wanafunzi wetu wanaopata matatizo walipiwe ada na Serikali yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina maeneo makubwa sana ya utalii, fedha kutoka kwenye utalii zingine kutosha kusaidia akina mama wanaojifungua na kutakiwa kupeleka vifaa vya kuwasaidia kujifungua, Serikali itoe, tunayo ardhi yenye rutuba, tunao watu wenye nguvu, kama Wasukuma na Wanyamwezi, lakini rasilimali hizi kwa sasa zinaliwa na wageni na Watanzania tunaangalia na kushangilia na wakati mwingine kuwasifu wageni kama wawekezaji wazuri sana na kuwataka wanufaike wao zaidi kuliko sisi (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa mezani na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba Wizara imekiuka, haikutekeleza kabisa azimio la Bunge bali imetekeleza kwa maslahi ya watu wengine na kuacha maslahi ya Watanzania. Nchi yetu ya Tanzania pamoja na utajiri tulionao, unaliwa na wageni, wakishirikiana na Watanzania wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze hivi, sababu moja ambayo nchi yetu na nchi nyingi za Afrika zinashindwa kuendelea ni kutokana na majibu rahisi katika matatizo makubwa. Ningedhani Waziri angeweza kukiri mara moja amekosea, nadhani tusingeendelea zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ni muhimili mmoja, Bunge ni muhimili mwingine, lakini Serikali imepata madaraka kutoka kwa wananchi na Bunge linawawakilisha wananchi na Serikali inatakiwa iwajibike kwa wananchi, kwa kuwa Bunge linawakilisha wananchi, Serikali inatakiwa kuwajibika kwa Bunge bila kusitasita na kuweka sababu zozote zingine. Maelezo ya Waziri hata Spika yamemshangaza na kuona haelekei kueleza bayana kwamba anatakiwa kuwajibika kwenye Bunge bila kusitasita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vurugu zinazotokea hapa duniani kote hazisababishwi na wananchi, bali husababishwa na viongozi waliopewa dhamana na wananchi, kuona kwamba nafasi walizopewa ni nafasi za kujitajirisha. Vyeo walivyonavyo, madaraka waliyonayo ni kama nyenzo za kujipatia nafasi ya kujinufaisha wenyewe, badala ya kuwatumikia wananchi waliowapa dhamana kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Rais Nyerere kuna wakati alisema katika Kitabu cha "Tujisahihishe" dhamana wanayokabidhiwa viongozi wanatakiwa waiheshimu dhamana hiyo na madaraka hayo na hata kuogopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa na kama alivyosema Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, tatizo letu sisi Afrika kubwa kabisa, linalotufanya tusiendelee ni kuweka majibu rahisi sana kwa matatizo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kutokuwajibu kwenye Bunge na kukiuka ni tatizo kubwa sana, ningetegemea ningepewa maelezo yanayostahili kabisa. Watanzania sasa tubadilike tusioneane haya, *"a friend in power is a friend in lost"*. Mtu yeyote aliyepewa dhamana kubwa na wananchi anakoma kuwa rafiki yako ili atekeleze na awajibike kulingana na dhamana aliyopewa, tumezoea kulindana kwamba huyu ni mwenzetu, na ndio maana hatuendelei, tusioneane haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Viongozi Serikalini waheshimu maamuzi ya Bunge linalosimamia Serikali, nilikuwa nashawishika kuongeza pendekezo lingine kutokana na mazingira haya na kutokana na tatizo lenyewe ambalo naliona ni kubwa, nilikuwa nashawishika, lakini kwa leo nadhani ni vema Serikali ielewe wajibu wake kwa Bunge, kwenye ibara ya nne vyombo ni viwili, Serikali ni ya utekelezaji, Bunge linaisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika Ibara ya 8(1)(c), Serikali inawajibika kwa Bunge na Bunge ndio linawakilisha wananchi na madaraka makubwa ya Serikali yanatoka na wananchi na kwa kuwa wananchi wanawakilishwa hapa Bungeni, inatakiwa Serikali iheshimu hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka Serikali ielewe kwamba inatakiwa kuheshimu na Watanzania sasa tubadilike, kama itatokea tena katika mazingira kama haya tukubaliane sasa, napendekeza siyo kwa leo, tukubaliane katika kipindi kinachokuja kama Kiongozi wa Serikali anakiuka maazimio ya Bunge na Bunge ndiyo linawakilisha wananchi na Bunge linatambulika Kikatiba kwamba linaisimamia Serikali Kikatiba hakuna haja ya kuja hapa na maelezo mengine yoyote, kama amekiuka aje na barua ya kuomba kujiuzulu (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tufuate utaratibu wa nchi zingine, katika nchi zingine kama mtu umekosea huwa hakuna malumbano kama mtu umekosea na ulikuwa umepewa dhamana kubwa, unakwenda na kueleza kwamba naheshimu dhamana niliyopewa, nimekosea sikuwajibika ipasavyo, naomba kuachia ngazi.

Mheshimiwa Spika, tubadilike Watanzania na tuanze baada ya tukio la leo na baada ya kueleza hayo, naomba kuunga mkono hoja na mapendekezo yote manne na hili siliongezei lakini naomba sasa tutafakari Watanzania tunapokwenda, tufikie hatua kwamba kama ulipewa dhamana kubwa ukikiuka hakuna haja ya malumbano unajitolea mwenyewe kwamba jamani naomba kujiuzulu kutokana na haya niliyokosea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kwa hoja ambayo Mbunge mwenzetu ameileta, lakini kabla sijaendelea na hoja yenyewe, ningependa kuchukua fursa hii kutoa *clarification* kidogo kwa jambo ambalo lilitokea jana kuhusiana na Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambapo kulikuwa kuna ubishani kuhusiana na masuala ya dini ya Kiislamu ya kuoa na kuolewa, nime-*consult Qur-an Surat Nisaa* na nimekuta kwamba alichokisema Mheshimiwa Nyami ndicho sahihi na sicho nilichokisema mimi, nilitaka ku-*clarify* hilo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hoja muhimu sana mbele yetu, si tu ni hoja inayohusu Haki, Madaraka na Kinga za Bunge, lakini pia ni hoja inayohusu rasilimali za nchi, *natural resources*, hata uzito wa mjadala wake ni lazima uendane na uzito si tu wa kulilinda Bunge kutokana na hadhi yake ya Kikatiba na kwa mujibu wa Sheria namba 3 ya mwaka 1988, Sheria ya Haki, Madaraka na Kinga za Bunge, lakini pia ni lazima mjadala wenyewe uendane na jinsi gani ambavyo sisi kama Wabunge tunasimamia kuhakikisha kwamba uvunaji wa rasilimali za Taifa unaendana na matakwa ya Taifa, kwamba Taifa halitumii rasilimali zake vibaya na wageni hawafaidiki na rasilimali ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba ku-*qoute* ili kuweza kufafanua sekta hii ya uwindaji wa kitalii, inaingiza nini kwenye Taifa hivi sasa, hii ni taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa ya mwaka 2007 ambayo ilisomwa hapa Bungeni mwezi Juni 2008, taarifa mpya itakuja mwezi Juni mwaka huu, eneo la wanyamapori, taarifa inasema nanukuu, mapato yatokanayo na wanyamapori yalipungua kutoka shilingi bilioni kumi na tano mwaka

2006 hadi bilioni saba mwaka 2007, sawa na upungufu wa asilimia 102, upungufu huo ulitokana na wawindaji kukataa kulipia ada mpya za wanyama na vitalu.

Mheshimiwa Spika, hii ni taarifa ya Serikali, tumefikia wakati ambapo tunaamua tunaweka ada mpya, watu binafsi, makampuni binafsi na wawindaji binafsi wanakataa na inaripotiwa kwenye taarifa ya Serikali, lakini licha ya kukataa kwao, licha ya kwamba asilimia 102 hatukupata, Serikali bado imekwenda, bado tumeweza kufanya uhifadhi, bado tumeweza kuendesha Serikali, kwa hiyo hata leo tukiamua ya kwamba kipindi hiki cha mpito kinafutwa na hata tukiamua kwamba leseni zilizokuwa zimekwishia 2009 ziishe msimu huu pasivunwe, hakuna kitakachoifanya Serikali ishindwe kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo jambo la msingi sana ambalo inabidi kulizingatia katika uamuzi wowote tutakaoufanya, hakuna woga wowote kwamba tukiamua tutapoteza mapato kwa sababu tuna vyanzo vingi sana vya mapato ambavyo bado hatukusanyi, dola milioni saba kwa nchi kama hii ni *nothing* kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka kukubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya kuhusu pendekezo la kwanza alilolitoa, hii barua ya ku-*extend* muda wa vitalu isimamishwe na wala siyo suala la mpito kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza, suala zima la barua ambayo Mkurugenzi wa Wanyamapori ameandika kwa wawindaji, tarehe 16 Januari, halafu Wizara inakwenda kukutana na Kamati ya Bunge siku tatu baada ya kuwa barua imekwishaandikwa.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa Wizara imekutana na Kamati kabla ya barua hii kuandikwa na Kamati kwa niaba ya Bunge ikatoa hiyo ruhusa nisingekuwa na *problem* kwa sababu tungeanza kuulizana sasa na Mheshimiwa Ndugai, kwamba haya mamlaka ya kufanya jambo hili kwa niaba ya Bunge umeyatoa wapi? Kwa hiyo tungeanza kumhoji Mheshimiwa Ndugai kwa ku-*overstep* shughuli za Kamati lakini barua hii ni ya tarehe 16, maamuzi yamekwishafanyika, kwa hiyo bado suala la *contempt of Parliamen*t liko pale pale, na *contempt of Parliament* siyo kitu ambacho tunakiongea tu, ni *offence* kubwa sana ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi nilikuwa naangalia sheria namba 3 ya mwaka 1988 ya *Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act*, tukiamua kuwa *serious* leo Mheshimiwa Mwangunga tungeamua aende Keko siku saba, kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, lakini hatuwezi kufika huko kwa sababu kwanza Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameonesha uungwana, ameomba radhi kwa mambo ambayo yametokea, lakini sasa ni lazima tuweke taratibu zetu za kisheria sawasawa kwa sababu tukichezea hadhi ya Bunge, tukishindwa kulinda hadhi ya Bunge, tutachezewa sana. Kwa hiyo, hili ni lazima liwe *very clear* na kila Mbunge aweze kuona, kama Mahakimu jinsi walivyolinda haki yao ndivyo inavyopaswa Bunge liweze kulinda haki hiyo ili kuhakikisha kwamba haki za Bunge hazipotei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jana Waziri ametusomea hapa taarifa yake, nikapata bahati ya kupata taarifa ambayo Waziri ameisoma kwenye Kamati, kuna *omissions*. Sasa sifahamu

kama hizo *omissions* ni kwa nia nzuri au ni kwa nia mbaya. Katika taarifa ambayo Waziri ameisoma jana Bungeni, hakuzungumzia kabisa kuongeza muda wa leseni za uwindaji. Katika taarifa ambayo Waziri ameisoma kwenye Kamati ya Bunge inayohusika na masuala ya utalii ameeleza kuhusiana na kuongeza muda, naomba ku- *quote* aya ya 4.2.2: "kipindi cha mpito cha ugawaji wa vitalu".

Mwisho kabisa Waziri anasema kwenye Kamati kitu ambacho hakukisema jana Bungeni, sasa sijui ni kwa makusudi kwa maana ya kulificha Bunge na Taifa kwamba *extension* imefanyika na bila taarifa ya Mheshimiwa Mzindakaya lisingefahamika hili. Waziri alisema, wamiliki wa vitalu wa sasa wataendelea kutumia vitalu walivyonavyo hadi mwaka 2012 kwa utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, haya maneno yalisemwa kwenye Kamati, hayakusemwa Bungeni jana, kwa nini? Wabunge wasome waone taarifa iliyosomwa kwenye Kamati na Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge na taarifa ambayo Waziri ameisoma jana hapa Bungeni haina maneno hayo. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo ambayo yanatia mashaka na ni mambo ambayo ni lazima tuwe *very clear* bila kuoneana aibu ili kuhakikisha kwamba huko mbele tunakokwenda haya mambo yasije kutokea tena na wala yasichukuliwe kama ni masuala ya kibinafsi kwa sababu kuna shughuli nyingi sana zimeendelea jana na ukiliangalia Bunge lako hata leo wakati Mheshimiwa Mzindakaya anasoma taarifa yake na wakati Mheshimiwa Waziri anaeleza majibu yake, kuna mpasuko, kuna shughuli nyingi sana zimeendelea jana, lakini kwa uongozi wako *this should be a National,* tusimwonee mtu wala tusimpendelee mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuhusiana na maazimio ambayo Mheshimiwa Mzindakaya ameyaleta kwenye Bunge lako, azimio la kwanza la kusitishwa kwa barua ile nilikuwa naliomba Bunge lako Tukufu likubaliane kwamba tusitishe vitalu viishe 2009. Leseni zitakapokwisha, tukakaa mwaka mmoja bila uwindaji… (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika taarifa.

**SPIKA**: Taarifa Mheshimiwa Ndugai.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Zitto wakati akiongea muda mfupi uliopita, amesema kwamba barua ile iliandikwa kabla ya Mheshimiwa Waziri hajazungumza na Kamati, nilitaka tu kuliweka vizuri kama atakubali, ni kwamba Mheshimiwa Waziri alikuja kuzungumza na Kamati tarehe 12 mwezi huu na barua imeandikwa tarehe 16 mwezi huu, ni hilo tu, si kinyume chake kama alivyowasilisha hapa Bungeni (*Makofi*)

**SPIKA**: Endelea Mheshimiwa Zitto, taarifa imepokelewa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa imepokelewa, nilichokuwa naomba tu nimalizie kwenye hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya, kwamba lile la kwanza tusitishe ile barua ambayo Mkurugenzi wa Wanyamapori ameiandika kwa wawindaji na madhara yake ni kwamba hatutakuwa na uwindaji kwa mwaka mmoja

yaani mwaka huu, madhara yake kiuchumi tukichukua takwimu za 2006 achana na takwimu za 2007 ambazo ni ndogo sana tutapoteza dola milioni 15.

Mheshimiwa Spika, Dola milioni 15 tutazipata kwa sheria ambayo tumeipitisha jana ya kuruhusu bajaji na baiskeli kama Mzee Cheyo alivyosema hapa, tukifanya biashara tutapata hizo hela, zitatumika kwa ajili ya kazi za uhifadhi. Kwa hiyo, hatutakuwa na hasara hata kidogo kusimamisha, hivyo nakubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba leseni ziishe mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza. La pili, kwa kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii hakulipa suala hili mwongozo mzuri, Bunge linakemea tabia hiyo ambayo athari zake ni kuleta mtengamano katika mhimili. Mheshimiwa Waziri keshaomba radhi na ni uungwana mtu ambaye anaomba radhi amekiri amekosea, sisi ni binadamu ni lazima tukubali kwamba amekosea, lakini kuna suala zima la barua ambayo imeandikwa ambayo nadhani Mheshimiwa Spika kama utakubaliana nami suala hili lingepata mwongozo mzuri kupitia Kamati ya Bunge ya Haki, Madaraka na Maadili na nadhani kwamba hili suala kwa mwongozo wako na kama utakuwa umekubali suala hili la azimio la pili liende kwenye Kamati ya Bunge ya Maadili ili kuweza kushughulikiwa kwa sababu kule watu wataapa na watatoa maelezo yao watajieleza na kuweza kutoa maamuzi ambayo yatakuwa ni ya haki pia hata Mkurugenzi wa Wanyamapori atapata nafasi ya kuweza kujitetea kwa mujibu wa *principle of natural justice*.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba kuunga mkono pamoja na mabadiliko ambayo nimewasilisha kwenye hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sijui najisikiaje, hivi tukiendelea na mjadala huu ni dhahiri kuna mgawanyiko hapa wala si jambo la kuficha, kwa jambo ambalo tunaweza kulimaliza, kwa hesabu zangu 2009 na 2010 ni miaka miwili, kwa nini basi tusifike mahali tuseme utaratibu huo mpya uanze 2011, inatoa nafasi ya Muswada, inatoa nafasi ya yote yale aliyokuwa anasema Mheshimiwa Waziri. Hizi hesabu za kwenda mpaka 2013 ndiyo zinawakera Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, yupo hapa, hebu tusaidie, hivi Wizara kweli ishikilie mpaka 2013, hata hesabu za shule ya msingi zinatuambia tisa ili ufikie 13 ni 4 ndio tatizo hilo.

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kusema mawili, matatu. Nilimsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, lakini inawezekana pengine katika maelezo yake ya mwisho ndiyo kidogo itakuwa imeleta mkanganyiko na ndiyo maana ukaliuliza mara mbili, tatu. Lakini nadhani kwa kifupi alichokuwa anasema tu ni kwamba, amekubali kutekeleza azimio kama lilivyowasilishwa na Mheshimiwa Mzindakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana kwamba ile miaka miwili tunayozungumza ni *inclusive* 2009/2010 na ndicho wataalamu wa *Task Force* walichokuwa wamekisema. Kwa hiyo nadhani tukikubaliana hilo *then* pengine hata mjadala mzima sio lazima sana.

Mheshimiwa Spika, alichokiongeza ni tahadhari tu kuonyesha kwamba *as a Government* kama alivyosema Mheshimiwa Kabwe, sasa hivi tuna tatizo la kujaribu kusema kama kutakuwa na *gaps* hizo tunazifanyaje. Sasa hizo ni jukumu la Serikali, wataliangalia waone namna ya kwenda nalo mbele. Kwa hiyo, nadhani nakubaliana kabisa kwamba pengine hakuna haja ya kuendelea nalo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tabu niliyokuwa naipata ni kwamba majina ya wachangiaji yameongezeka sana sasa, ndio maana nikamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu anabeba dhamana yote ya Serikali humu ndani atupe tu huo ufafanuzi. Nadhani kwanza Mheshimiwa Waziri amekuwa ni muungwana, ameomba radhi jamani kwa yaliyotokea na hii ndio maana ya kubeba dhamana kwa sababu ukiwa kwenye Wizara sio kila kitu kinachotokea, ushauri unakuja wa aina mbalimbali.

Kwa hiyo kwa maana ya azimio hili lililoletwa na Mheshimiwa Mzindakaya ni kwamba kipengele cha pili au sehemu ya pili ile ametutoshelezaMheshimiwa Waziri na ukichukua hili la kusema ile barua, itarekebishwa kisheria kwa sababu lazima upige *GN*, huwezi kuandika barua tu hivi ukasema umetengeneza vitu kisheria nina hakika Waziri atatoa *GN* ambayo itazingatia hiyo miaka miwili kuanzia 2009.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo sioni sababu ya kubishania, labda mtoa hoja sasa kwa maana ya kanuni nimwite aweze kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Mzindakaya.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa uongozi wako katika jambo hili na vile vile ningependa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kuhusu hoja hii, kwanza ni Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii namshukuru. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mpendazoe, napenda vile vile kumtambua na kumshukuru Mheshimiwa Zitto Kabwe. Pia napenda kumshukuru na kutambua Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mchango muhimu alioutoa.

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wengi walivyochangia, ningependa kumalizia kwa kusema kwamba, katika yale maazimio kwanza nakubaliana mia kwa mia kwamba lile azimio la pili nalifuta rasmi lisiwemo kwenye mapendekezo kwa sababu Waziri amekuwa mstaarabu na muungwana, ameeleza ukweli wa jambo hili kwamba lilifanyika kwa nia njema bila kulidharau Bunge.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo nataka niliseme na hili nalisema kwa faida ya Bunge letu ni kuwa, kwa kipindi chote na hata sasa naweza nikasema kwa jeuri kabisa kwamba Bunge letu lina imani kubwa sana na Serikali. Vile vile utaona hata jana ingawa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uchungu wa kuhurumia wale wenzetu wenye ulemavu wa ngozi alitokwa na machozi. Lakini nilipenda ajue pia kwamba kuna Wabunge wengine pia walimuunga mkono kutoa machozi kwa sababu ya jambo lenyewe lilivyo ovyo. Lakini vile vile kwa kuamini kwamba mwenzetu Waziri Mkuu ni *very humble,*

anaheshimu Bunge na anaheshimu Wabunge. Kwa hiyo, napenda niseme hiyo pia hata kumshukuru katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, bila kupoteza muda nataka niseme kuwa katika maisha ya binadamu na katika kuendesha Serikali hata majukumu tuliyopewa haiwezekani tukafanyia maamuzi ambayo mengine kwa faida ya kesho hayana hasara. Ukikwepa huwezi ukakosa, kila wakati utakuwa mwoga kufanya maamuzi. Lazima maamuzi ambayo una hakika yana faida ya kesho vizuri zaidi uyafanyie maamuzi sasa hata kama utaona unapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili katika sekta moja ambayo *for many years* imeumia ni uwindaji wa kitalii. Tumeumia sana katika sekta hii. Wakikutana wenyewe wanajisifu kwamba wanailetea Serikali mapato, si kweli kwa miaka zaidi ya sita sasa Serikali haijawahi kuvuka dola milioni 10 kwa mwaka wakati wenzetu wa Zimbabwe ambao wana maeneo machache walishafika mpaka milioni 45, sisi tunapigiwa kelele na dola 10. Wenzetu Kenya wana wanyama wengi hawawindishi. Uganda wanyama hawawindishi,unaona! Kwa hiyo, nasema kwamba naishukuru sana kauli ya Waziri Mkuu ambayo uamuzi wake unafanywa watu wajiandae vizuri zaidi na kuweka mipango ambayo nchi itapata faida zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa kusema kwa siku zijazo kwa sababu ya kanuni zenyewe ni kwamba, nataka kutahadharisha Kamati zetu pia zote kwamba jambo ambalo limeamuliwa na Bunge lenyewe Kamati yake haiwezi kuitengua mpaka irudi kwa Bunge ndiyo kanuni inavyosema. Kwa hiyo, Kamati ya akina Ndugai nao walikosea kwa sababu hawana haki ya kubadilisha maamizio ya Bunge. Kwa hiyo, ni vizuri niliseme hili kwa tahadhari, Kamati hizi zijikite katika mamlaka yao wasivuke mamlaka ambayo ni ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kutoa hoja kwamba pendekezo la kwanza na la tatu yakubaliwe na Bunge lako na lile la pili naomba kuliondoa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Napenda nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ujasiri mkubwa kuibeba dhamana ya Serikali na kuliweka sawa jambo hili ambayo imefupisha mjadala na nina hakika imerejesha umoja wetu ndani ya Bunge. Nitoe tu kama tahadhari kwa wenzetu Waheshimiwa Mawaziri, Bunge liko macho sana sasa hivi. Kwa hiyo, mnapotekeleza shughuli zenu na pia kupata ushauri ni vizuri kulinganisha na yale ambayo yamekwishaamuliwa na Bunge ili tusije tukafika hapa tena pa kuanza kuhojiana katika mambo kama haya. Baada ya kusema hayo azimio hilo limepita. Waheshimiwa Wabunge nina udhuru inanibidi kwenda Urambo, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Jenista Mhagama aje ashike hapa, Mungu akipenda tutaonana siku ya Jumatatu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Janista Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kuhitimisha hiyo shughuli nzito ya hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya sasa tutaendelea na *agenda* inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa Mwaka 2008 (*The Wildlife Conservation Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sifa kubwa ya Tanzania ni kuwa na aina mbalimbali na idadi kubwa za wanyamapori kuliko nchi nyingine za Bara la Afrika na Duniani kwa ujumla. Wanyamapori hao hustawi katika mandhari ya asili ambayo inawaongezea thamani zaidi ya kuwa asilia. Uasilia huo ni jambo linalochochea uongezekaji wa watalii wanaokuja nchini kuangalia wanyamapori na wengine kuwinda na hivyo kuongeza Pato la Taifa. Kati ya maeneo yenye sifa za kipekee duniani ambayo Tanzania inajivunia ni pamoja na Hifadhi za Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro, Serengeti na Pori la Akiba la Selous ambayo ni maeneo yaliyotangazwa kuwa Urithi wa Dunia wa Asili *(Natural World Heritage Sites).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi za Taifa za Mlima wa Kilimanjaro na Serengeti zimewekwa kwenye orodha ya vivutio vya utalii 50 (hamsini) vilivyo bora zaidi duniani kwa mwaka 2008 *(The Best 50 World Tourism Destinations for the year 2008).* Ni matarajio yetu kuwa maeneo mengine katika nchi yetu pia yataingia kwenye orodha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kumekuwepo na mafanikio mbalimbali kutokana na juhudi katika uhifadhi, kwa mfano baadhi ya wanyama ambao Kimataifa wako kwenye orodha ya wanyama walio hatarini kutoweka, kama vile Faru na Tembo idadi yao hapa nchini imekuwa ikiongezeka. Kwa mfano idadi ya tembo imeongezeka kutoka 55,000 mwaka 1989 hadi kufikia 142,722 mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya maeneo ya hifadhi yamepanuliwa kwa mfano, Hifadhi za Taifa za Arusha na Kilimanjaro kwa jumla ya kilometa za mraba 1,327 na maeneo mengine kupandishwa hadhi ya uhifadhi. Aidha, maeneo 16 ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori yenye zaidi ya kilometa za mraba 23,086 yameanzishwa kwenye vijiji kwa mpango wa ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi. Kati ya maeneo hayo, maeneo 10 yametangazwa kuwa *Wildlife Management Area (WMA)* na kupatiwa Hati za Matumizi ya Wanyamapori. Vile vile Maeneo ya ardhioevu manne yenye ukubwa wa kilometa za mraba 48,669.7 sawa na 8% ya sura ya nchi, yamewekwa katika orodha ya ardhioevu zenye umuhimu wa Kimataifa *(Ramsar Sites).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa ya kuwekeza katika uhifadhi, Sera nzuri na usimamizi wa Sheria. Aidha, mafanikio katika uhifadhi wa wanyamapori ni mchango mkubwa katika tasnia ya utalii Tanzania tofauti na nchi nyingine duniani ambazo hutegemea utalii wa fukwe za bahari, malikale na utamaduni wa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali ya wanyamapori nchini bado ina fursa kubwa ya kuchangia zaidi katika pato la Taifa na kuondoa umaskini wa kipato kwa Watanzania hususan wanaoishi vijijini. Hivyo, rasilimali hii inapaswa kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo katika uhifadhi wa wanyamapori, ni dhahiri kuwa mabadiliko mbalimbali ya kisera, mifumo ya utendaji, tamaduni na desturi za jamii pamoja na mabadiliko ya mifumo ya uchumi wa dunia na kiteknolojia vimekuwa ni changamoto zilizoifanya sekta ndogo ya wanyamapori kushindwa kupata mafanikio makubwa zaidi, ambayo kimsingi yangeweza kupatikana kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto hizo ni:

Moja, ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya ardhi kwa ajili ya kilimo na malisho ya mifugo kuwa tishio kwa maeneo ya hifadhi;

Pili, migogoro kati ya maeneo ya mapori tengefu na ardhi za vijiji;

Tatu, ushiriki mdogo wa wananchi katika maamuzi ya matumizi ya wanyamapori;

Nne, migongano ya matumizi ya uvunaji na yale yasiyo ya uvunaji katika maeneo yaliyo nje ya Mapori ya Akiba, Hifadhi za Taifa na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro;

Tano, wanyamapori kutopewa thamani stahili;

Sita, kuvamiwa kwa maeneo ya wanyamapori;

Saba, kuzibwa na kuzuia mapito au shoroba (*corridors*) za wanyamapori;

Nane, kuongezeka kwa ujangili;

Tisa, kutokuwepo msukumo wa sheria katika kutekeleza mikataba ya Kimataifa;

Kumi, kuongezeka kwa mahitaji ya wananchi katika kushiriki na kuwekeza katika biashara ya rasilimali ya wanyamapori;

Kumi na moja, migogoro kati ya binadamu na wanyamapori *(human- wildlife conflict);* na

Kumi na mbili, mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha ukame na hivyo kuathiri wanyamapori na makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo zimekuwa ni kero kubwa kwa wahifadhi na wadau wote kwa ujumla. Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori unakusudia kukabili changamoto hizi na kuweka mwongozo na mikakati madhubuti ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kuandaa Muswada huu umekuwa na ushirikishi mkubwa sana wa wadau. Wadau hao ni pamoja na wananchi wa ngazi zote kuanzia Vijiji hadi Taifa, pamoja na Viongozi wa Dini na Taasisi Zisizo za Kiserikali. Katika mchakato wa Muswada wa Sheria hii, kuanzia mwaka 1999 hadi Januari 2009, jumla ya warsha kumi (10) na mikutano tisa (9) vimeendeshwa. Warsha hizo zilizowahusisha wadau wa makundi mbalimbali ziliendeshwa kwenye kanda sita, kwa maana ya mikoa inayounda Kanda za Kaskazini, Mashariki, Kati, Magharibi, Kusini na Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyolalamikiwa sana na wananchi kuwa ni kero yalijadiliwa katika mikutano na warsha mbalimbali. Maoni hayo yamezingatiwa katika kuboresha maeneo yote yaliyoonekana kuwa na upungufu, kwa nia ya kuwa na uhifadhi endelevu wa wanyamapori nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada, kutokana na kukua kwa tasnia ya utalii wa wanyamapori na kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali ya wanyamapori ni muhimu kutunga Sheria itakayolinda na kusimamia wanyamapori na mazingira yao kwa kuzuia uharibifu ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na kuhakikisha kuwa kuna matumizi endelevu ya rasilimali hii muhimu. Lengo ni kuhifadhi na kuongeza mchango wa sekta katika uchumi wa Taifa, ushiriki wa Watanzania katika tasnia ya utalii pamoja na ubora wa huduma zinazotolewa katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada unaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni kutunga Sheria Mpya ya Wanyamapori, ambayo naamini itakuwa ni faraja ya kila mmoja wetu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unapendekeza usimamizi unaozingatia haja ya ulinzi wa wanyamapori, uwindaji wa kitalii, utalii wa picha, biashara ya wanyamapori hai, uanzishwaji na uendeshaji wa mashamba na ranchi za wanyamapori pamoja na umiliki wa wanyamapori wa mapambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyamapori nchini hawana mipaka iliyowekewa uzio. Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, unakusudia kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa zaidi katika kufanya maamuzi ya uhifadhi wa wanyamapori nchini, hususan kwa wale walioko kwenye maeneo ya ardhi za vijiji zenye wanyamapori. Vile vile kwa kutumia rasilimali ya wanyamapori kwa njia endelevu, Muswada huu unakusudia pia kuweka mazingira mazuri ya kuongeza pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Muswada, hadi sasa kwa upande wa Tanzania Bara, masuala ya wanyamapori yanatawaliwa na Sheria ya Hifadhi Wanyamapori, Sura ya 283 iliyorekebishwa mwaka 2002 pamoja na Kanuni zake. Sheria hii ilitungwa mwaka 1974 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1978. Hivyo tangu wakati huo hadi sasa kumekuwepo mabadiliko mengi ya msingi katika tasnia ya wanyamapori ikiwa ni pamoja na kushirikisha wadau katika usimamizi unaolenga uhifadhi na uvunaji endelevu wa wanyamapori na hivyo kusababisha Sheria iliyopo kutokidhi hali na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Wanyamapori mwaka 1998. Aidha, kutokana na mambo muhimu yanayojitokeza katika nyanja za uhifadhi hasa za kisayansi, kiuchumi na kijamii, Sera ya Wanyamapori ilipitishwa mwaka 2007 kwa lengo la kuingiza masuala muhimu yaliyojitokeza katika fani ya uhifadhi hususan ardhi oevu, tathmini ya athari katika mazingira na ufugaji wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nchi yetu imeridhia mikataba mingi ya Kimataifa tangu Sheria itungwe, hivyo basi, mambo mengi yaliyo kwenye mikataba hiyo ambayo yanagusa masuala ya wanyamapori hayakujumuishwa katika Sheria hii. Suala la ardhi oevu halijaguswa kabisa katika Sheria ya sasa ingawa jukumu la usimamizi wa ardhioevu nchini ni la Idara ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu katika Muswada, Muswada huu pamoja na mambo mengine umezingatia yafuatayo:-

Moja, matamko ya Sera ya Taifa ya Wanyamapori ili kuhakikisha kuwa malengo ya Sera hiyo yanafikiwa;

Pili, uanzishaji wa Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori itakayosimamia ulinzi, uhifadhi na uendeshaji wa maeneo yenye rasilimali za wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro;

Tatu, uimarishaji wa ulinzi wa wanyamapori kwa kuunda Kikosi Dhidi ya Ujangili;

Nne, usimamizi na uendeshaji wa bioanuwai katika maeneo ya ardhioevu;

Tano, uanzishaji, usimamizi na uendelezaji wa ranchi za wanyamapori, mashamba na bustani za wanyamapori;

Sita, usimamizi na uendeshaaji wa mapori tengefu *(Game Controlled Areas);*

Saba, utambuzi na usimamizi wa maeneo ambayo ni njia au mapito ya wanyamapori (*corridors*), maeneo yanayozunguka hifadhi *(buffer zones),* maeneo ya mtawanyiko (dispersal areas) na mazalia ya wanyamapori *(breeding sites);*

Nane, kuweka masharti ya tathmini ya athari ya Mazingira kwa uwekezaji kwenye maeneo ya wanyamapori na tathmini za kimkakati katika mazingira kwa programu za hifadhi ya wanyamapori na ardhioevu;

Tisa, uainishaji wa namna ya kushughulikia wanyama wakali na waharibifu na taratibu zitakazofuatwa katika kutoa kifuta machozi kwa wananchi wanaopata madhara yaliyosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu;

Kumi, utaratibu wa utoaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii, umiliki wa hisa kwa Watanzania katika kampuni za uwindaji wa kitalii zinazomilikiwa na wageni na usimamiaji wa masuala ya Wawindaji Bingwa *(Professional Hunters)* pamoja na uainishaji wa masharti yanayoambatana na uwindaji;

Kumi na moja, utafiti na uchimbaji wa madini yenye thamani kubwa katika mapori ya akiba na tengefu kwa masharti maalum;

Kumi na mbili, ubadilishaji wa adhabu ili kwenda sambamba na hali halisi ya kiuchumi na uhifadhi wanyamapori nchini;

Kumi na tatu, uwekaji wa masharti ya usimamizi na utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa;

Kumi na nne, uwekaji wa masharti ya ushirikishaji wa jamii katika maeneo ya hifadhi ya wanyamapori na ardhioevu;

Kumi na tano, uainishaji na usimamizi wa masuala ya utafiti na mafunzo; na

Kumi na sita, ushirikishwaji wa wananchi katika utekelezaji wa mamlaka ya Waziri na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori chini ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpangilio wa Muswada, kutokana na mambo muhimu yaliyojumuishwa katika Muswada huu, Muswada umegawanyika katika Sehemu Kumi na Tisa.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada inahusu jina la Sheria, tarehe itakayoanza kutumika, tafsiri ya maneno na misamiati muhimu iliyotumika kwenye Muswada huu.

Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu madhumuni ya uanzishwaji wa Sheria inayopendekezwa ambayo imezingatia Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007.

Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza uanzishwaji wa Idara ya Wanyamapori, Kurugenzi ya Idara ya Wanyamapori, majukumu na watumishi watakaofanya kazi chini ya Mkurugenzi wa Wanyamapori. Sehemu hii pia inapendekeza mpangilio wa Taasisi na uongozi. Aidha, inapendekezwa kwamba usimamizi wa Mapori ya Akiba ubakie chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ambaye sifa zake zimeainishwa.

Katika sehemu hii Kifungu cha tisa (9) kinapendekeza kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuanzisha Kikosi Dhidi Ujangili kwa kushauriana na taasisi au asasi za ulinzi na usalama baada ya kupata ridhaa ya Rais. Kikosi Dhidi ya Ujangili kitakuwa cha kiaskari.

Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza uanzishwaji na usimamizi wa maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa, yaani mapori tengefu na mapori ya akiba, vilevile usimamizi wa maeneo ya ardhioevu.

Katika Sehemu hii Kifungu cha 21 kinapendekeza kuwepo ulinzi wa ushoroba (*corridor*), mazalio, maeneo ya kandokando ya maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa *(buffer zones)* na maeneo ya mtawanyiko ambayo pia wanyama hupendelea *(dispersal areas).*

Kifungu cha 24 kinampa Waziri uwezo wa kutangaza Mnyama wa Taifa ambaye amezuiliwa kuwindwa; Mnyama huyo anaweza pia kutumika kama Nembo kwenye nyaraka za Taifa au vyombo mbalimbali vya Serikali kama vile Ndege za Kiserikali na fedha.

Kifungu cha 29 kinazuia uwindaji na uvunaji wa wanyamapori katika Hifadhi za Taifa.

Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza uanzishwaji wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Wananchi na uanzishwaji wa Chombo cha Ushauri wa Maliasili kwenye ngazi ya Wilaya.

Sehemu ya Sita ya Muswada inapendekeza kuanzishwa kwa mipango ya ujumla ya usimamizi wa mapori na Tathmini ya Athari ya Mazingira.

Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza matumizi ya wanyamapori ya uvunaji kama vile kuwinda na yasiyo ya uvunaji kama vile utalii wa picha. Sehemu hii ya Muswada inapendekeza jinsi ya kuwinda, ukamataji wa viumbe hai na utalii wa picha. Pia Muswada huu unapendekeza utoaji wa leseni na vibali. Kifungu cha 37 kinapendekeza uundaji wa Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii.

Sehemu ya Nane ya Muswada inapendekeza jinsi ya kutatua migogoro itokanayo na wanyama wakali, hatari na waharibifu. Sehemu hii pia inapendekeza kutoa kifuta machozi pale ambapo binadamu atapoteza maisha au kujeruhiwa na wanyama wakali na hatari. Pia Sehemu hii inapendekeza kutoa kifuta machozi kwa wananchi watakaoharibiwa mazao yao na wanyama waharibifu. Vile vile, Sehemu hii inapendekeza kuua mnyamapori pale anapohatarisha maisha ya binadamu.

Sehemu ya Tisa ya Muswada inahusu taratibu za kusajili nyara na bidhaa zitokanazo na wanyamapori.

Sehemu ya Kumi ya Muswada inapendekeza taratibu za kusimamia biashara ya nyara, kwa kutoa vibali na leseni kama vile vibali vya kusafirisha nyara ndani na nje ya nchi na taratibu za uhamishaji.

Sehemu ya kumi na moja inapendekeza aina ya nyara zitakazotambulika kuwa nyara za Serikali. Kifungu cha 86 kinaweka wajibu kwa wananchi kutoa taarifa za umiliki wa nyara za Serikali kwa mamlaka husika.

Sehemu ya Kumi na Mbili ya Muswada inahusu taratibu za kuanzisha ranchi za wanyamapori, mashamba ya wanyamapori, eneo la kuzalisha, bustani na maeneo ya utunzaji wa wanyamapori waliookotwa au kukamatwa.

Sehemu ya Kumi na Tatu ya Muswada inahusu Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania, ambao lengo lake kuu ni kusaidia uhifadhi wa wanyamapori, utafiti, kuchangia kwenye shughuli za maendeleo ya jamii, elimu na uhamasishaji wa wananchi kuhusu uhifadhi. Mfuko utasimamiwa na Bodi ya Wadhamini.

Sehemu ya Kumi na Nne ya Muswada inahusu uhifadhi wa wanyama walio hatarini kutoweka na wale wanaolindwa na Mikataba ya Kimataifa. Sehemu hii pia inampa Waziri wa Maliasili na Utalii mamlaka ya kutangaza aina ya wanyamapori waliozuiliwa kufanyiwa biashara ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya Mikataba ya Kimataifa.

Sehemu ya Kumi na Tano ya Muswada inahusu Biashara ya Kimataifa ya wanyama na mimea ambayo iko hatarini kutoweka (*Convention on International Trade in Endangered Species of Wild fauna and flora - CITES).*

Sehemu ya Kumi na Sita ya Muswada inahusu elimu, mafunzo na utafiti wa wanyamapori. Kifungu cha 95 kinampa Waziri wa Maliasili na Utalii uwezo wa kuanzisha taasisi za elimu na mafunzo. Kifungu cha 96 kinaitambua Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (Tanzania *Wildlife Research Institute – TAWIRI*) kuwa msimamizi mkuu wa utafiti unaohusu wanyamapori nchini.

Sehemu ya Kumi na Saba ya Muswada inaainisha aina za makosa, viwango vya adhabu, utaifishaji wa nyara na uendeshaji wa kesi zinazohusu makosa yatokanayo na ukiukwaji wa Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Kumi na Nane ya Muswada inapendekeza utoaji wa tuzo kwa mtoaji taarifa zitakazofanikisha uokoaji wa nyara za Serikali na taarifa zozote za ukiukwaji wa Sheria inayopendekezwa zitakazopelekea kutiwa hatiani watuhumiwa. Pia sehemu hii inampa mamlaka Waziri kutengeneza Kanuni za kufanikisha utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Kumi na Tisa ya Muswada inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura ya 283. Aidha, Sehemu hii inaainisha taratibu zitakazofuatwa wakati wa kipindi cha mpito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mawasilisho hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. FUYA G. KIMBITA (K.n.y. MHE. JOB. Y. NDUGAI - MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira naomba nisome taarifa yetu. Ni maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa mwaka 2008 (*The Wildlife Conservation Act, 2008).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa kanuni 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2007 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa wanyamapori nchini unasimamiwa na Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori, Sura 283 ya mwaka 1974 iliyorekebishwa mwaka 2002, Sheria ya Hifadhi za Tanzania, Sura 282 na Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Sura 284. Sheria hizi zinasimamia ulinzi, uhifadhi, maendeleo, kanuni na udhibiti wa wanyamapori na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato mzima wa Muswada huu ulianza mwaka 1999 na umeshirikisha wadau wengi na mabadiliko makubwa yamefikiwa katika kuboresha Muswada huu hasa katika Vikao vya Kamati vya kutafuta maoni ya wadau *Public Hearing* vilivyofanyika mwezi Septemba na Oktoba 2008 Dar es, Salaam, Arusha na Dodoma. Pamoja na semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyofanyika tarehe 2 Novemba, 2007 katika ukumbi wa Pius Msekwa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vikao hivyo Serikali ilikubali kuufanyia marekebisho Muswada huu kwa kuzingatia maoni ya wadau, Waheshimiwa Wabunge na Kamati, masuala hayo yalikuwa mengi kiasi cha kusababisha kuchapishwa upya kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umependekeza kufutwa kwa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyama ya mwaka 1974, Sura namba 283 ambayo imepitwa na wakati na inakizana na Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na hivyo kuwa na haja ya kuwa na sheria mpya ambayo inaitwa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2008. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kumi na tisa ambazo kwa pamoja zina maudhui makuu yafuatayo:-

Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007, Ulinzi, Usimamizi na matumizi endelevu ya wanyamapori, Kuanzisha mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori na majukumu yake, uanzishwaji wa maeneo ya jumuiya za hifadhi za wanyamapori za wananchi *WMC* na uanzishaji na usimamizi wa ranchi za wanyamapori, mashamba na bustani za wanyamapori. Kutatua migogoro itokanayo na wanyamapori kwa njia mbalimbali. Kuhifadhi wanyamapori walio hatarini kutoweka na usimamizi wa

biashara ya Kimataifa ya wanyamapori. Utoaji wa elimu, mafunzo na utafiti wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za wanyamapori zinaonyesha kwamba idadi ya wanyamapori na mtawanyiko wao unapungua katika maeneo yote muhimu ya wanyamapori yaani ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa hasa yenye makazi ya binadamu. Hali hii imetokana na, pamoja na mambo mengine, kuwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 1974 iliyopitwa na wakati hivyo kutokuwa na mfumo mzuri wa usimamizi na uhifadhi wa Wanyamapori. Kupitishwa kwa Muswada huu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008 itasaidia kusimamia mfumo mzima wa uhifadhi wa wanyamapori kwa kuondosha upungufu wowote uliokuwepo hasa katika masuala ya mikataba ya Kimataifa, kufanya tathmini ya athari za mazingira, *EIA*, kulinda maeneo yenye wanyamapori, mapito na mazalia ya wanyamapori na kukuza uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Uhifadhi ya Wanyamapori ya Mwaka 2008. Kamati yetu inaipongeza Wizara kwa kuweza kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu wenye lengo la kuwalinda, kusimamia na kuwahifadhi wanyamapori. Hii itasaidia kukuza uchumi wa nchi kupitia uwekezaji katika wanyamapori na kutatua migogoro baina ya mahitaji ya jamii na Sheria za Uhifadhi na hatimaye kuongeza idadi ya wanyamapori nchini. Maeneo makubwa yaliyohifadhiwa na mengine yenye wanyamapori yanachukua karibu asilimia 30 ya eneo la nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwepo na malalamiko toka kwa wananchi walio nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kwamba hawajaona motisha ya kuhifadhi wanyamapori ukizingatia kwamba kisheria maduhuli yanayokusanywa hupelekwa Hazina na Taasisi za Serikali. Kamati inaishauri Serikali iweke Kanuni muafaka zitakazohakikisha kwamba jamii husika inasimamia kikamilifu na kukusanya mapato yanayopatikana katika maeneo ya wanyamapori wanayoyasimamia kama Sheria mpya inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapori ya akiba bado hayakidhi haja ya hifadhi ya wanyamapori kutokana na kwamba mapori haya yanapata fedha kidogo za uendeshaji. Kamati inaishauri Serikali kubakiza asilimia kubwa ya fedha kwenye maeneo ya mapori ya akiba ili kuimarisha mapori haya badala ya fedha yote kwenda hazina kwa kipindi ambacho Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakuwa bado haijaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndio nchi pekee Mashariki na Kusini mwa Afrika ambayo haitumii kanuni za soko shindani katika sekta nzima ya uwindaji wa kitalii. Tanzania haitumii minada ya wazi badala yake hutumia utaratibu wa kugawa vitalu vya uwindaji vinavyosimamiwa na Idara ya Wanyamapori. Sheria hii mpya ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008 imeweka mfumo bora wa usimamizi wa maeneo ya uwindaji wa kitalii kwa kuzingatia madaraja ya ubora.

Kamati inasisitiza Wizara kuharakisha utungaji wa kanuni mpya za Sheria hii pindi itatakapopitishwa. Wakati umefika kwa Serikali kuwa makini na mikataba ya Maliasili na Utalii ambayo inategemea kuingia. Mikataba mingi iliyosainiwa inaisababishia Serikali hasara kubwa hasa kwa upande wa mapato na inanufaisha watu wachache. Kamati inasisitiza kwamba mikataba ya Maliasili na Utalii ambayo Serikali inategemea kuingia iwasilishwe mbele ya Kamati ili itoe maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008 imetamka wazi kuhusu uanzishwaji wa Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyamapori ambayo itasimamia kikamilifu Mapori ya Akiba na Tengefu. Kamati inasisitiza Serikali ianze mchakato wa kuanzisha Mamlaka hii mara baada ya kupitishwa kwa Sheria hii. Kamati imefurahishwa na Sheria hii mpya kwa kuweka masharti ya Tathmini ya Athari ya Mazingira (*EIA)* kwa uwekezaji kwenye maeneo ya wanyamapori na programu za hifadhi ya wanyamapori na ardhioevu. Hali hii itasaidia kulinda mazingira ya hifadhi hasa kwa upande wa miradi mikubwa na midogo itakayoanzishwa ndani na pembezoni mwa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya Mwaka 2008 imetoa nafasi kwa vijiji kufaidika zaidi na uwekezaji kwenye maeneo ya Jumuiya za Hifadhi Wanyamapori za Wananchi, yaani *WMA's*. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili kuhakikisha kwamba usimamizi wa wanyamapori hauleti migogoro na vijiji vyenye hati za ardhi hasa katika suala zima la Mapori Tengefu na Ardhi za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu J. K Nyerere katika tamko la Arusha mwaka 1961 alisema nanukuu, "Uhai wa wanyamapori ni jambo linalotuhusu sana kote katika Afrika. Viumbe hawa wa porini, wakiwa katika mapori wanamoishi, sio muhimu tu kwa ajili ya kuajabiwa na kuvutia lakini pia ni sehemu ya maliasili yetu na pia ndio mustakabali wa maisha yetu ya baadaye. Kwa kukubali dhamana ya wanyamapori wetu, tunatamka kwa dhati kwamba wajukuu wa watoto wetu wataweza kufurahia urithi huu mkubwa na wa thamani adimu", mwisho wa kunukuu.

Kamati kwa kuzingatia maneno haya ya Mwalimu inatoa wito kwa Watanzania wote kuwa na mwamko wa uhifadhi wa wanyamapori kwa manufaa ya nchi nzima kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo; Mheshimiwa Job Y. Ndugai Mwenyekiti; Mheshimiwa Hassan R. Khatib, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Fuya G. Kimbita Mjumbe; Mheshimiwa James Daudi Lembeli Mjumbe; Mheshimiwa William V. Lukuvi Mjumbe; Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta Charles O. Mlingwa, Mjumbe; Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mjumbe na Mheshimiwa Profesa Raphael B. Mwalyosi, Mjumbe.

Wengine ni Mheshimiwa Phillemon Ndesamburo, Mjumbe; Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mjumbe; Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mjumbe; Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Said Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mjumbe; Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mjumbe; Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mjumbe; Mheshimiwa Dokta Guido G. Sigonda, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mjumbe; Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mjumbe; Mheshimiwa Aziza S. Ally, Mjumbe; Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mjumbe; Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mjumbe na mimi ninayesoma Fuya G. Kimbita Mjumbe pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba nitoe shukrani. Kamati inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati na kushiriki kikamilifu katika kuwasilisha maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia sana katika kuandika na kuboresha Muswada huu. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Dokta Thomas Kashililah kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati Ndugu Michael Kadebe na Elieka Saanya kwa kuihudumia Kamati vizuri wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mbunge na Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Ezekiel Maige, Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Dokta Radislaus Komba, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kanuni namba 62 (d) kinaelezea muda unaotakiwa kutolewa taarifa Bungeni na Msemaji wa Kambi ya Upinzani; nayo inasema, *"Msemaji wa Upinzani anayewasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, atayawasilisha maoni hayo kwa muda usiozidi dakika 30."* Waheshimiwa Wabunge, kanuni namba 104, inazungumzia utaratibu wa kuongeza muda Bungeni lakini utaratibu huo unahusu zaidi shughuli za Kamati, Bunge linapokuwa kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa kuwa, muda wa dakika 30 ambazo tunazisema kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani tulionao sasa hivi hautoshi, basi nitatumia kanuni namba 2 (2) ili nimruhusu Msemaji wa Kambi ya Upinzani aweze kutoa taarifa yake Bungeni na dakika hizi zilizobaki kwa kuwa hazikidhi dakika 30 basi natumia mamlaka hayo ya kifungu hicho cha (2) kumuongezea dakika zitakazokidhi dakika 30 ili aweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani na tutakaporudi mchana basi tuanze na uchangiaji wa Wabunge wa ujumla, kwa sababu mpaka sasa ninayo hapa mezani orodha kubwa kidogo ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wangependa kuchangia hoja hii.

Kwa hiyo, kwa mamlaka hayo sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani ili aweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani na wakati huo huo Makatibu wangu wanisaidie kuongeza hizo dakika ili awe na dakika zake 30 na kama atamaliza kabla basi

nitasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo jioni. Msemaji wa Kambi ya Upinzani, namuona Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kutuwezesha sote kuuona mwaka mpya wa 2009. Pia nikushukuru wewe kwa fursa hii ya pekee ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009, kwa mujibu wa kanuni ya Bunge, Toleo la mwaka 2007, kanuni ndogo ya 86 (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa kutoa salamu za mwaka mpya kwa wananchi wote wa Mkoa wa Tabora na kwa namna ya pekee wananchi wa Wilaya ya Urambo. Nawatakia kila la heri katika kazi zao za kujenga Taifa kwa mwaka wote wa 2009. Mwisho niwatakie afya njema viongozi wangu wa Chama Cha Wananchi *CUF* na viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani Bungeni wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Muhamad na Mheshimiwa Dokta Wilbroad Slaa. Natoa pongezi vilevile kwa Waziri wa Wizara hii ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Naibu wake Mheshimiwa Ezekiel Maige pamoja na timu nzima ya wataalam waliowezesha maandalizi ya Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii ya Uhifadhi wa Wanyamapori inayofuta Sheria ya zamani ya Wanyamapori ya mwaka 1974, Sura ya 283 ni muhimu sana kwa kuboresha uhifadhi wa wanyamapori pamoja na kuinua uchumi wa Taifa letu. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kuna mapungufu ya msingi ambayo yanahitaji kuzingatiwa ili sheria hii iweze kukidhi haja iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu kinachotoa tafsiri mbalimbali za maneno, neno *Hour of Darkness* limetolewa tafsiri kuwa ni kuanzia saa 12.30 jioni hadi saa 11.30 alfajiri. Kambi ya Upinzani inaona kuwa hii tafsiri haikutilia maanani tofauti ya maeneo katika nchi hii. Kwa mfano mawio na machweo katika Ukanda wa Pwani ni tofauti na Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa. Hivyo basi, ni vizuri suala la tafsiri hiyo likaangaliwa ili kuondoa utatanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau mbalimbali wa masuala ya uhifadhi wamekuwa wakitoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ya jinsi gani ya kuboresha sekta ya wanyamapori. Mojawapo ya mapendekezo ya Wabunge na wadau ni kuundwa kwa mamlaka ya wanyamapori ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli zote kwenye mapori ya akiba ikiwepo uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kifungu cha 7(8) cha Muswada wa Sheria kutamka kuwa Waziri atawezesha kuanzishwa kwa mamlaka ya wanyamapori lakini kifungu cha 7(3) kinampa Mkurugenzi wa wanyamapori kuwa yeye ndiye msimamizi mkuu wa Idara ya Wanyamapori. Kifungu cha 7(4) kinasema kuwa Mkurugenzi wa Wanyamapori ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala ya uhifadhi, uendeshaji

wa wanyamapori na bidhaa za wanyamapori. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba kifungu cha 7(8), kiweke muda maalum wa Waziri kuleta Muswada wa kuanzishwa Mamlaka ya Wanyamapori iliyodhaminiwa. Pia inapendekeza sheria iainishe wazi baada ya Mamlaka kuundwa ni majukumu yapi ya Mkurugenzi wa Wanyamapori yatahamia chini ya Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9(1) kinamruhusu Waziri kuanzisha kikosi cha kijeshi cha kuzuia ujangili. Kwa sasa hivi kipo kikosi maalum cha kupambana na ujangili, yaani *anti-pourching unit,* lakini bado ujangili umeendelea kuongezeka kwa kasi kubwa na hata kutishia kutoweka kwa baadhi ya wanyama. Kambi ya Upinzani inaona suala la kupambana na ujangili ni jambo linalohitaji ushirikishwaji wa karibu sana wa jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi. Hata vingeundwa vikosi vingapi, bila jamii kushirikishwa kikamilifu na wao waone manufaa ya wanyama hao ni dhahiri, ufanisi utakuwa ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya hifadhi yanatakiwa doria za mara kwa mara. Hali hiyo sasa ni hatari, hakuna vitendea kazi vya kutosha, kwa mfano magari kwa ajili ya doria, askari ni wachache sana, hivyo maeneo mengine hakuna kabisa doria zinazofanywa na kikosi cha kuzuia ujangili na badala yake Serikali inategemea makampuni ya uwindaji ndio yafanye doria. Msimu ambao sio wa uwindaji ujangili unakuwa ni wa kutisha, hali hii ni hatari sana kwa usalama wa wanyama wetu. *(Makofi).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kwamba njia pekee ya kuimarisha ulinzi wa kupambana na ujangili, kwanza ni Wizara kuboresha mfumo mzima wa utendaji kazi kwenye mapori ya akiba, kuhakikisha uwepo wa vitendea kazi vya kutosha, usimamizi makini na ushirikishwaji wa wananchi. Aidha, Kambi ya Upinzani inaona kwamba ili rasilimali ya wanyama iendelee kuwepo ni lazima Serikali kuhakikisha kwamba 75% ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii inarudi kwenye Idara ya Wanyamapori ili kuimarisha ulinzi na uendeshaji wa mapori hayo, tofauti na ilivyo sasa ambapo fedha yote inakwenda Serikalini, yaani Hazina na 25% tu ndio inayorudi kwa ajili ya uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18(2)(b) sehemu ya faini, kuna maneno yamesahaulika, nina-*quote, "fine not less than 300",* yaani kuna neno *thousand* limesahaulika pale, *"but not exceeding 500",* neno tena *thousand* limesahaulika pale. Kwani haiwezekani wanyama ambao wapo katika sehemu ya pili ya jedwali kutozwa faini ya kiasi cha shilingi 300 hadi 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 30(2) kinasema kwamba, "Mgawanyo wa mapato kwenye maeneo ya hifadhi ya jamii ya wanyamapori ni lazima yaende sambamba na kanuni zitakazotolewa na Serikali mara kwa mara kwa kuzingatia mgawanyo sawa wa gharama na mapato." Lengo kuu la kuanzishwa kwa maeneo ya jamii ya hifadhi za wanyamapori yaani *WMA* ni kuhusisha uhifadhi wa wanyamapori na maendeleo ya jamii kwa kuhamishia usimamizi wa wanyamapori kwa wananchi na kuhakikisha jamii zinanufaika kutokana na uhifadhi huo. Kwa mantiki hiyo, wananchi kwa kupitia jumuiya zao wapewe mamlaka kamili za kusimamia, kuendesha na kupanga mapato na matumizi

yatokanayo na rasilimali wanayoimiliki. Iwe ni jukumu la Serikali kuwajengea wananchi hawa uwezo wa kutosha katika nyanja mbalimbali ili waweze kutumia rasilimali iliyopo kupambana na umasikini na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 34(1), Sheria inatamka kufanyika kwa tathmini ya mazingira kabla ya kuanzishwa kwa mradi wowote kwenye maeneo ya hifadhi. Ni muhimu sana tathmini zikafanyika kwa kuzingatia uhifadhi na maslahi ya Taifa, pale inapoonekana haiwezekani taarifa ieleze wazi kwamba haiwezekani. Wataalam wanaokabidhiwa jukumu la kufanya tathmini ya mazingira kwa lengo la kuwekeza au kukataza uwekezaji kufanyika kwenye maeneo lengwa wafanye kazi hiyo kwa umakini mkubwa na kwa kuzingatia maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya tathmini hiyo ioneshe hali halisi na Serikali izingatie ushauri wa wataalam kabla ya kukubali uwekezaji wa mradi wowote. Hata hivyo, utaratibu unaotumiwa sasa wa wawekezaji kulipa gharama za kufanya tathmini ya mazingira pale anapotaka kuwekeza, unatoa mwanya mkubwa kwa wawekezaji kufanya ushawishi ili matakwa yao yatimizwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia suala hili upya na kwa umuhimu ili kuziba mianya hiyo na kuepukana na matatizo ya uwekezaji sehemu zisizostahili na hivyo kuharibu mandhari nzima ya hifadhi zetu. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwenye Muswada wa Sheria hii kiwepo kifungu kinachombana mtumishi na mwekezaji pale itakapogundulika kuwa tathmini ya mazingira haikufuata kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 37, kuundwa kwa Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji. Kwa muda mrefu Serikali kwa kupitia Idara ya Wanyamapori imekuwa ikiendesha shughuli za uwindaji wa kitalii hapa nchini. Kama zilivyo shughuli nyingine, utalii unaweza kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni na ile kauli mbiu ya Serikali ya "Maisha Bora kwa Kila Mtanzania" kwa kiasi chake ingeweza kuwa na maana iliyokusudiwa. Ili uwindaji wa kitalii uweze kuchangia zaidi katika kumkomboa Mtanzania kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kuifanya rasilimali yenyewe ya wanyamapori kuwa endelevu kwa vizazi vyote, kunahitajika nia thabiti ya kufanya mabadiliko ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji wa kitalii hapa Tanzania umekuwa unanufaisha watu wachache na zaidi ni wawindaji kutoka nje. Taswira iliyojengeka ni kwamba wawindaji kutoka nje ndio wanaomudu kuendesha biashara hii na kwa kuwa wanajua kushawishi wao ndio wamepewa vitalu vizuri, vikubwa, vyenye wanyama wengi, vilivyoko karibu, Watanzania wengi wamenyimwa fursa hiyo. Ni matumaini ya Watanzania kwamba kwa sheria hii mpya Watanzania wengi wataweza kumiliki vitalu na kumiliki biashara ya uwindaji wa kitalii kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii katika pato la Taifa.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke mipango endelevu ya kuwawezesha Watanzania wengi kuendesha biashara ya uwindaji wa kitalii. Wataalam wa fani ya

uwindaji wa kitalii yaani *Professional Hunters* tulionao ni wachache na hata hao wachache wamejishikiza kwenye makampuni ya wageni kwa sababu wengi hawana vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za kuuzia wanyama wetu si ghali kama inavyosemekana ukilinganisha na nchi nyingine. Kwa kuzingatia upekee wa wanyama tulionao, Tanzania ni lazima bei zetu ziendane na hadhi ya wanyama wetu na hivyo kuweza kupata fedha za kutosha kuendelea kuwahifadhi, kuboresha miundombinu na kuinua kipato cha Taifa letu. Haiwezekani kampuni moja ya kigeni inahodhi vitalu zaidi ya 15 kwa zaidi ya miaka 20 huku Mtanzania anayeonesha moyo wa kuingia kwenye biashara hiyo anafuatilia kwa miaka mingi hajapata kitalu. Hii inakatisha tamaa na pia inavunja moyo kwa Watanzania wengine wenye nia ya kuendesha uwindaji wa kitalii. Tunategemea sheria mpya itamlinda na kumthamini Mtanzania zaidi na Kamati ya Ushauri ya Kugawa Vitalu itakayoundwa itazingatia maslahi ya Taifa na siyo maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 49, sheria iainishe maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kukamata wanyama, mbinu za kutumia kumkamata mnyama na nani anayeweza kumkamata mnyama. Kifungu cha 96 kinachohusu usimamizi na uratibu wa wanyamapori, hatuwezi kuwa na uhifadhi endelevu wa rasilimali wanyama kama hatutaboresha kituo chetu cha utafiti wa wanyamapori. Kwa miaka kadhaa kituo hiki kimekuwa kikifanya kazi chini ya kiwango kwa sababu ya kutowezeshwa kimafungu na uchache wa wataalamu. Sheria hii imetamka kuwepo kwa kituo hicho lakini haijaeleza ni jinsi gani ya kukiimarisha ili kifanye kazi kwa ufanisi zaidi. Tunashauri kwenye kanuni ielezwe mkakati maalum wa kusaidia kituo hiki muhimu kwa ajili ya kuhifadhi wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 99(1) kinachosema, na-*quote, "the burden of proofly on the person charged."* Hivyo basi kifungu hiki kinakwenda kinyume na sheria zingine za nchi zinazosema kuwa mtuhumiwa mara zote hana hatia hadi pale Mahakama itakapothibitisha kuwa ana hatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Suala la wananchi wanaozunguka mbuga za wanyama kushirikishwa kuhifadhi maeneo hayo ni la msingi sana. Utaratibu wa Serikali wa kutoa 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii kurudi kwa wananchi ni vizuri ukazingatiwa kwa kila mwaka na kwa maeneo yote. Pia iwekwe wazi kuwa wamepata 25% ya fedha kiasi gani, kwani wamekuwa wanauliza maswali ambayo hayapati majibu. Serikali iweke utaratibu huu kwenye sheria ili utekelezaji wake uwe rahisi tofauti na sasa ambapo inaonekana kama ni hisani ya Serikali kwa wananchi ikiamua inatoa, ikiamua isitoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walinzi namba moja wa wanyamapori ni wale wanaowazunguka. Hata askari wa doria ili wafanikiwe ni lazima watumie wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Serikali ni lazima ihakikishe fedha hizo zinafika kwa walengwa na ikiwa zitapitishwa kwenye Halmashauri, Serikali itoe mwongozo wa jinsi gani ya kuzitumia tofauti na sasa ambapo zikifika tu zinapangwa kwenye shughuli

nyingine na kufanya wananchi wanaoteseka na wanyama kutokuona manufaa ya wanyama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa sheria hii katika kuchangia uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya Watanzania na kwa kuzingatia mambo mengi sana yanayowezesha utekelezaji wa sheria hii yatakayowekwa kwenye kanuni ya wanyamapori, Kambi ya Upinzani inapendekeza kanuni mpya zikishakamilika ziletwe Bungeni, Wabunge wapate fursa ya kutoa maoni yao kabla ya kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nawashukuru sana wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Magdalena, Msemaji wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii kwa hotuba yako na kwa kweli umejitahidi kutumia muda wako vizuri kabisa na kwa muda ambao unatakiwa. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema dakika hizi haziwezi kuturuhusu kuanza zoezi la uchangiaji wa jumla kwa Waheshimiwa Wabunge na orodha ambayo iko hapa mezani kwangu, nadhani itakuwa ni busara ya Kiti, kama nitawasoma wachangiaji wa mwanzo ili waweze kujiandaa kuja mapema kwa shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini na atafuatiwa na Mheshimiwa Castor Ligalama, Mbunge wa Kilombero. Hawa watakuwa wachangiaji watatu wa mwanzo na baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi na nitaendelea kuwataja Waheshimiwa Wabunge wengine kulingana na orodha yangu ambayo ipo hapa mezani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusikiliza hotuba hizo tatu, basi naomba nisitishe shughuli hizi za Bunge, mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni  Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na hoja ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya kuleta Muswada wa Wanyamapori wa Mwaka 2009 na kabla hatujaendelea basi nimwite Katibu ili atupe mwongozo wa shughuli zetu za jioni.

Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea, na kama nilivyosema katika kipindi hiki cha jioni mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Dewji Mbunge na ninaona Mheshimiwa Mgana Msindai yupo, kwa hiyo naomba nimwite Mheshimiwa Mgana Msindai ili aanze kuchangia hoja yetu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili nami nichangie kwenye huu Muswada wa kubadili Sheria ya Wanyamapori, nirudie kuzungumza kwamba nimekuwa kwenye idara hii, nimekulia humo mpaka nimestaafu, kwa hiyo ni idara ninayoifahamu. Kwanza, tunashukuru sana kwa Muswada huu kuja leo pamoja na kwamba umechelewa lakini nina imani utasaidia kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori na shughuli zingine zote zinazofanyika humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na machache ya kuzungumza. Muswada huu nina imani tutaupitisha lakini umekuja wakati ambapo mapori yetu yako kwenye hali mbaya sana. Umekuja wakati ambapo wanyama wamepungua sana kwa idadi na wanyama wenye nyara zile tulizokuwa tunaziona miaka ya nyuma wamepungua sana. Sasa ni juu yetu, ni juu ya Serikali na juu ya Wizara ya Maliasili na hasa wanyamapori kuanza upya kuwalinda na kuwatunza wanyamapori wetu. Tatizo tulilonalo sasa hivi hatuna askari wa kutosha, mapori yetu sasa hayana watu ambao wanaweza kusimama na kulinda wanyamapori wetu. Kwa hiyo ni juu ya Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kazi hiyo na ni juu ya Serikali kuipatia fedha Wizara ili kuajiri askari wa kutosha kwenye mapori yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu, sasa hivi ukienda kwanza askari wetu wako wachache, vitendea kazi vya dhiki usafiri wa shida, na mpaka sasa hivi mapori yetu tumeweka rehani kwa wawindaji. Wawindaji ndiyo wanaofanya kazi badala ya Serikali, ndiyo wanaofanya doria kutumia wale askari wachache waliopo. Ni aibu na hii inaonyesha kwamba tulishawaachia hawa watu wakae na mapori yetu kwa sababu askari kama yupo na mwindaji hana sauti na night yake anategemea kutoka kwa kampuni inayowinda humo na kama idara inachangia, inachangia hela kidogo sana, sasa yule mtu hawezi kumzuia mwindaji kuwinda mnyama anayemtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mapori mengine tunasema sasa hivi kutokana na askari wetu kuwa wachache, wawindaji wanalinda hayo mapori hata baada ya msimu, hilo sikubaliani nalo kwa sababu anapolinda hayo mapori msimu ukiwa umekwisha kuna mambo anayofanya ni lazima apate kitoweo kutokana na wanyama hao na ni lazima awalishe watu wake kutokana na wanyama walioko humo na hiyo *quota* ya kuwinda baada ya msimu sijui inatoka wapi? Kwa hiyo, naomba sana, tumekuwa tunakusanya hela chini ya kiwango miaka ya nyuma lakini hizo hela zote zinakwenda Serikali na zikiingia Serikalini hazirudi kwenda kutunza wale wanyama wanaoleta zile hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kabisa tufanye uamuzi wa makusudi, Serikali iamue kabisa itoe fedha kwa ajili ya kulinda wanyamapori wetu. Wanyama hawaozi, tukiwalinda ndiyo tutapata nyara nzuri, ndiyo tutapata wanyama wengi wa kutusaidia sisi wa ndani na wale watakaokuja kuwalinda. Nashauri kabisa Serikali iliangalie upya, sasa hivi haiitendei haki Idara ya Wanyamapori hata ile *retention* inayotakiwa itolewe haitoki kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee juu ya vikosi vya kuzuia ujangili, toka mwaka 1985 tumekuwa tunaomba idara hii iendeshwe kiaskari, miaka yote hii Serikali haikutoa idhini hiyo. Nashukuru leo nimeona kwenye sheria ipo na naomba ianze haraka sana,

lakini hata hivyo vikosi tulivyonavyo ni vichache na vimepitwa na wakati, sasa sijui tutaanzishaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri askari wa Idara ya Wanyamapori yote kuanzia Wilayani mpaka Taifa iendeshwe kijeshi hapo wanyama wetu watapona. Sasa hivi hata wakienda kwenye *game* zetu waendeshe kiaskari lakini kama huko Wilayani ambako ndiyo mapori yako ambayo ndiyo tunataka tuhifadhi wanyama wote, kama hatutabadili mtindo hatutafanikiwa. Sasa hivi Wilaya nyingi hazina Mabwana Nyama na wanyama wanao.

Kwa hiyo, ni lazima tubadili msimamo ili kuweka vikosi kwa kanda haitoshelezi, tukichukua mfano Kanda ya Kati iko Manyoni inakwenda mpaka karibu mpaka wa Mbeya, mpaka wa Iringa, Mkoa wa Dodoma wote, Mkoa wa Singida, kwa kweli hatufanyi kitu, kwanza askari wenyewe wako wachache na nyezo za kufanyia kazi hazipo. Ni lazima Serikali ikubali kutoa ndiyo tunaweza kuwalinda wanyama wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa tuamue Idara ya Wanyamapori iwe Mamlaka. Ianzishe Mamlaka ya kulinda wanyamapori, hii itafanana na Ngorongoro, itafanana na *TANAPA* na pale tutaweza kujiendesha, lakini kwa mtindo huu hatutafika. Pale idara ya wanyamapori makao makuu ianzishwe mamlaka na idara ya Serikali iwepo yenyewe ishughulikie sera na sheria lakini pia bila kuwa mamlaka kwa kweli hatutakwenda, inatakiwa ianzishe mamlaka ambayo itasimamia *game reserve* zote, *open area* ambayo bado zina wanyama, hapo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbuke kwamba hawa wanyama sasa hivi wamezagaa na ni lazima tuanzishe zile *village scouts* nchi nzima, hiyo ndiyo itatusaidia na wananchi wetu wameshaanza kuona faida za wanyamapori, tukiwawezesha na tukiwashirikisha watatusaidia sana. WMA’s zianzishwe nyingi hizi za majaribio zimepitwa na wakati karibu kila Wilaya nchi hii inao wanyama, inayo yale mapori, tulikuwa tunaita *open areas* wawezeshwe waanzishe hizo WMA’s na wasianzishe tu bali idara isaidie mpaka zikomae, kwa sababu kwa kweli hali ya wanyama wetu inakwenda vibaya mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya uwindaji wa kitalii, maamuzi yameshatoka hapa lakini nina imani kabisa haya maamuzi kwa kuanzia yatatuumiza hata ukiacha hii ya *extension* ya mpaka mwaka 2012 tulishaingia mkataba na wawindaji ambao wanawinda mpaka 2011. Nakubaliana kabisa na uamuzi huu lakini tuwe tayari kupambana na hawa watu, kwa sababu watatushtaki na Serikali ili kumaliza hili tatizo moja kwa moja iwe tayari kuwalipa fidia na gharama watakazotaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote nimekuwa nasema humu tusimamishe uwindaji kwa miaka kama tulivyofanya 1974 lakini leo tumesimamisha lakini ni lazima tuwe tayari kwa yatakayotokea. Kama inawezekana tuanze mapema kujiandaa, lengo letu ni zuri, tupate fedha za kigeni sawasawa na wenzetu ambao wanapata fedha za kutosha. Tujipange sawasawa na Serikali sasa iweke jicho lake kule, wanyamapori ni dhahabu

inayotembea, wanyamapori wanaleta wageni wengi sana, wanaleta watalii wengi sana, ni lazima tuwalinde na tushirikiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mawazo yangu, nasema hivi, Idara ya Wanyamapori kwa sababu tumeamua iendeshwe kiaskari, itolewe kwenye Halmashauri za Wilaya iongozwe moja kwa moja kutoka Makao Makuu kama vikosi vinavyoendeshwa, hiyo itatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri, ana kazi ngumu sana, ni lazima ajiandae na ni lazima sasa abadilishe mtazamo, atafute magari ya kutosha, atafute vifaa vya kufanyia kazi yeye na Mkurugenzi wake ili waweze kuwawezesha askari wetu kufanya kazi. Sisi tuliokuwa ndani tunaumia sana kuona hali ilivyo na tunaumia sana kuona njia za wanyama zimekuwa *blocked* na wananchi. Pia niombe Serikali kupitia Waziri wa Maliasili zile *corridors* ambazo wanyama walikuwa wanapita Kiswahili tunaita ushorolo, kwa mfano, wanyama wa Serengeti wanakwenda Masai Mara wanarudi wanakuja Ngorongoro na wanyama wanavuka kwenda Manyara *National Park*, wanavuka kwenda Tarangire *National Park* kwa kupitia Yai la Chini, Yai la Chini ni pori ambalo lilikuwa na wanyama wengi na ndiyo ilikuwa mapumziko na mazalio ya wanyama na ndege. Sasa ningeiomba Serikali ifanye kama ilivyofanya Ihefu, Yai la Chini ni pori sawa sawa na Ngorongoro.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge namshukuru Mheshimiwa Msindai kwa mchango wake. Kabla sijamwita Mheshimiwa Hasnain Dewji nimekuwa nikiletewa ujumbe hapa Waheshimiwa Wabunge wakitaka kujua mjadala huu utaendelea mpaka lini. Sasa naomba nitumie fursa hii kuwapa taarifa rasmi kwamba hoja hii tunaendelea kuijadili mpaka Jumatatu, hatuimalizi leo na orodha yangu hapa tayari ina Waheshimiwa Wabunge 24. Kwa hiyo, nadhani wataendelea kupata nafasi na tunaendelea na hoja hii mpaka Jumatatu. Baada ya kutoa ufafanuzi wa jambo hilo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Hasnain Dewji na Mheshimiwa Casto Ligallama kama nilivyosema pale awali kipindi cha asubuhi ajiandae.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Wanyamapori wa 2008. Muswada huu nasema umechelewa sana kuja, ungekuja kabla, kwa hiyo umepitwa na wakati, umeanza 1974 tumechelewa sana, hatukuweza kuhifadhi wanyama wetu kwa sababu Muswada umechelewa sana. Hata hivyo, naunga mkono Muswada huu mia kwa mia, Muswada huu ni mzuri na tukiuzingatia, tunaweza kuhifadhi wanyamapori wetu na vijiji vyetu vikafaidika na mpango wa *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Muswada huu ni mzuri lakini kuna matatizo ambayo nataka niyaeleze hapa. Kifungu cha 17(1) kinasema hivi, kuna matatizo ya

kuchoma moto misitu. Kuchoma moto misitu hailingani na uhifadhi wanyama. Tuna matatizo wawekezaji wetu wanachoma moto hovyo misitu. Nalisema hili nina mfano na kwangu kule wameunguza misitu mpaka mikorosho ya watu imeungua, eti ukimwita mwekezaji aje anakuwa mjeuri, kijiji kinamwita anafanya ujeuri wakati hii ni mali yetu, wanyama wetu, anaunguza moto kwenye kitalu chake unakuja mpaka kijijini, mikorosho inaungua, inateketea, yeye mjeuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sheria hii iwabane, iwatoze faini kubwa na watoe fidia kwa wananchi wa kijiji kile. Mkorosho mmoja unachukua zaidi ya miaka saba mpaka uzae, wana ugharimia kwa kununua madawa, anakuja eti Mzungu anaunguza mashamba na ukimwita haji kwenye vikao vya kijiji na Serikali haichukui hatua yoyote. Ukienda Wilayani wanasema ngoja tutamwita mwekezaji lakini ni mpaka tukikaa na vijiji husika. Vijiji hivyo ni Kichonda, Likawage wananchi wanalalamika kwa sababu ya hawa wawekezaji. Haya ni matatizo makubwa, naomba hii faini iwe kubwa na fidia ilipwe kubwa sana kwa waathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yetu asilimia ishirini na tano (*retention)* yale yanayotoka Hazina kutokana na maliasili zetu za wanyamapori, ni kidogo. Nitaomba jibu Mheshimiwa Waziri aniambie atuongezee angalau ifike asilimia sitini, tunapata tabu na wanyama huko, wananchi wangu wa Kilwa wanapata tabu, tunataka Mheshimiwa wakati anajumuisha atuambie lini ataongeza *retention* iwe asilimia sabini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapata *retention* asilimia ishirini na tano, katika asilimia ishirini na tano, asilimia arobaini inabakia Wilayani, inafanya kazi gani pale Wilayani, haina kazi, hizo pesa ziende vijijini kwa hao wananchi ambao ndiyo wanafanya hifadhi kubwa kuliko Wilayani wanakosema. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri hii *retention* iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee uharibifu wa mashamba ya wanakijiji au wakulima wanaopakana na Selous. Asilimia kubwa ya Kilwa imepakana na Selous na athari ya wanyamapori tunaipata sana. Hapa tunaona tunamthamini zaidi mnyama kuliko binadamu au kuliko mkulima, kwa jinsi hii sheria inavyosema. Sikatai uhifadhi, lakini hapa inavyoonyesha hii sheria inamthamini sana mnyama kuliko mkulima aliyekuwa maskini, anayezalisha kidogo na hicho kidogo kinakuja kuliwa na tembo, fidia zenyewe ni ndogo, wakati wakulima wale wanalima kwa mkono, wanapata tabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio haki, sio haki kabisa, tunamuonea mkulima tuache kumthamini mnyama. Nataka niseme hivi, hii sheria ikiletwa Wangindo wengi watafungwa Kilwa kwa sababu wewe umekula shamba langu na wewe nikule nyama yako, wana matatizo wana jadi yao toka asili. Kwa hiyo, tutawafunga wengi, hii tujihadhari wengine watashindwa kulipa faini, tutawaweka kwenye magereza yetu. Tutaonekana wana siasa tuna matatizo lakini haya tujaribu kurekebisha. Wengi juzi kule mashamba yalikuwa yameingiliwa na tembo, nampigia Mkurugenzi ananiambia risasi hatuna Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana hili la wanyamapori, tutatunza wanyamapori, *WMA* inawafundisha watunze, watatunza wanyama wanajua faida za wanyama. Kwa hiyo, hilo jamani tulifanyie kazi hao wananchi wangu wakulima wengi watafungwa kwa sheria hiyo inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu nyama kwa wanakijiji. Hii ni muhimu sana katika kuhifadhi, tulione hili angalau kwenye msimu mara tatu tumewapa nyama waonje, uharibifu utapungua, ile chachu ya kutamani itapungua. Kama tutawapa uhifadhi utaongezeka na watasema kweli wanatujali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema *WMA* itasaidia sana kuwapa elimu, lakini tusifanye mpango wa kuwafukuza tu tuwape elimu, mbona tutawafunga wengi, lakini tukiwapa elimu naona mambo hayo yataweza kwenda vizuri, wale wananchi wakipata elimu wanaweza kuhifadhi, lakini yule wa mjini hawezi kuhifadhi, yule anayekaa kijiji ndiye anaweza kuhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba elimu na *WMA* itatusaidia sana na kama alivyosema Mheshimiwa Msindai hapo kwamba tuongeze *WMA*, kweli naunga mkono kabisa, iko haja tuongeze WMA, tunawapa fursa wanakijiji wanaamua wanachotaka na wanapata misaada gani kutokana na mwekezaji yule naona hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nataka kuongea kuhusu *ranch*, hizi *ranch* zitasaidia sana, Kilwa ina maeneo makubwa sana ya kuweka *ranch*, kama Mheshimiwa Msindai alivyosema wanyama wanakwisha, kama tutakuwa na *ranch* hizi au mwekezaji aje kuwekeza kwenye *ranch*, nasema wanyama watazaliana zaidi, tutapiga picha, watalii watakwenda zaidi na tutahifadhi zaidi kwa kupitia mtindo huu wa *ranch* na utasaidia mno. Nitatoa mfano wa mnyama twiga, mnyama twiga hayupo kwa sababu twiga wako ng’ambo ya pili ya Rufiji, wanashindwa kuvuka kuja Kilwa. Sasa tukiwa na *ranch*, naona tutaweza kuwavusha na kuwaweka kwenye *ranch* wakazaliana ili na Kilwa napo tuwe na twiga. Hili ni muhimu sana Upanda *ranch*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mapungufu mengi sana, hatuna magari, risasi wala wataalam yaani *game wardens. S*asa nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ajira ya *game wardens?* Tuwe na mpango maalum kwa sababu wale ndiyo watatuhifadhia nyama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *hunting blocks*; kuna *professional hunters* pale, wenzetu Wazungu wanapokuja kuwekeza wanakuja na wataalam wao wenyewe; kwa nini tusitoe ajira kwa *professionals* wetu wa ndani ya nchi ili waweze kuhudumia kwenye *blocks* zetu?

Tunamthamini sana Mzungu akija awe *professional hunters;* kwa sababu ni Mzungu ndiyo anamtaka Mzungu mwenzake aende akawindishe, tunakosa ajira hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatetea sana mishahara jamani; hii kazi ya wanyamapori ni ngumu, naiomba Serikali i-*review* upya mishahara ya *game holders* na mishahara ya wakuu wote kwenye Idara ile iongezewe ili kuwaongezea tija zaidi na zawadi ziwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asiliamia mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika Muswada huu wa Wanyamapori. Mimi nina maeneo mawili nataka kuyaongelea:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, linahusu dhana nzima ya uhifadhi na nitajikita kwenye uwindaji wa vitalu. Tuchukulie dhana ya uwindaji kama vile sawa na madini yaliyopo kwenye Mikoa ya Ziwa. Sisi Wilaya ambazo tunazunguka Hifadhi ya Taifa na hayo mapori tengefu, tuna kazi ya kuwalinda wanyama hao na mara nyingine hata kwa gharama ya kupoteza maisha yetu na mazao yetu, lakini bila kupata fidia ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi niliwahi kufanya kazi kwenye Wizara hii, lakini kitengo tofauti. Naiona Idara hii ya wanyamapori, inaendeshwa vilevile nilivyoiacha mimi miaka ya sabini na kitu; kwani ni lazima iwe vilevile si unaweza kuwa mbunifu ukaibadilisha?

Sasa tunapendekeza sisi tunaowahifadhi wanyama hao, tupate siwezi kuita fidia, tupate malipo ya kuwalinda wanayama hao, kama wenzetu wanavyopata malipo kutokana na madini kuwa katika Mikoa yao. Hicho ni kiasi ambacho kitatusaidia na sisi kwa kazi ile ya kulinda bila silaha kiwe kifuta jasho. Hiyo haihusiani na malipo ya ada ya uwindaji, iwe ni malipo tu kwa sababu sisi tumezungukwa na wanyama wale na tunawalinda. Unaweza ukasema sisi tunawalindaje wakati hatuna silaha; tunawalinda kwa kutokuwala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani nilikuwa nasikia wenzetu akina Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kule Ngorongoro, waliruhusiwa kukaa kwa sababu walikuwa hawali wale wanyama, lakini siku hizi nasikia wameanza kuwala sijui kweli wataniambia. Basi na sisi wale wanyama hatuwali tunawahifadhi, tulipwe kwa kazi hiyo ya kuwahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wenzetu wa madini wanalipwa *dollar* 200,000 kila mwaka, kwa sababu tu ya kuwa na madini kule na sisi Serikali kwa kuanzia itufikirie siyo lazima kiwe kiwango hicho, lakini kiasi cha kulipwa kwa kuwa ni walindaji wa hifadhi hizo za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo sasa uwindaji utafanyika kibiashara, litakuwa suala lingine; yale yatakuwa malipo tofauti na bahati nzuri wenzangu wameliongelea hilo. Hiyo asilimia 25 tunayopata huko Wilayani, halafu tena igawanywe asilimia 40

iende kwenye shughuli za uhifadhi Wilayani, asilimia 60 ndiyo zikafanye shughuli za maendeleo ya vijiji; kwa kweli hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kwenye Muswada, nafikiri labda Waziri ataiweka hii kwenye kanuni, nijue itakubalika vipi kwa sababu hata katika maswali ya kawaida tumewahi kuuliza juu ya kuongeza kiwango hiki; kwamba, asilimia 75 iende kwa wananchi na asilimia 25 ndiyo ibaki Serikali Kuu. Kwa nini ninasema hivyo?

Ninasema hivyo kwa sababu ndiyo shughuli iliko; wanyama wapo huko Wilayani na sisi ndiyo tunawahifadhi. Wananchi wakiona kwamba, fedha zile zilizokuja ndiyo zimeezeka shule yao, hawawezi kufanya mambo ya ujangili.

Siku hizi wananchi ni waelewa sana. Wilayani kwangu kwa mfano, tuna Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, hapo awali kulikuwa na watu wanachomachoma moto, lakini tangu waone kwamba milima ile kwa kuihifadhi imetusaidia kutupa *catchment* ya mvua, ikitokea tatizo la moto tu zile Kamati za Mazingira zinakuwa za kwanza ku-*mobilize* watu kwenda kuuzima na kuwashughulikia wale wote waliofikiriwa walifanya kitendo kile. Hii imetokana na faida ambayo watu wanaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa wanyama hao ambao wanahifadhiwa halafu fedha zake hazipatikani waziwazi, inawezekana wenzetu wanaofanya vitalu ndiyo wanaofaidi; ingekuwa vizuri tubadilike badala ya ile *formular* ya asilimia 25 kwa asilimia 75, asilimia 75 iende kijijini na asilimia 25 ibaki kule Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupendekeza hayo, nije kwenye suala la uwindaji wa vitalu. Mimi katika Wilaya yangu nina Kilombero *Game Controlled Area* na yupo mwekezaji pale ana kitalu *Kilombero North Safaris* na tuna vijiji zaidi ya 20, lakini ukiangalia mapato yanayopata vijiji hivi ni shida tu. Sehemu ya mwanzo huku ukitoka Kidatu ni Hifadhi ya Selous, unapoendelea mbele ndiyo unapata *Game Controlled Area* ya Kilombero. Huku mwanzo ni matatizo ya tembo kula mazao ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipengele hapa namba 69, ukurasa wa 49, kinazungumzia kwamba, endapo itatokea mnyama fulani amefanya uhalifu au amejeruhiwa ameingia kwenye eneo la wananchi, piga simu haraka kwa *Game Warden* au *Game Scout* aliyepo karibu. Sawa, siku hizi simu tunazo, sasa ukimpigia atafanya nini; hana hata baiskeli, hana bunduki, hana risasi, labda ukipigia apate taarifa tu kwamba huku tunakufa ajue ni wanyamapori wanaotuharibia? Kwa hiyo, haisaidi kupiga simu na kifungu hiki kimewekwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu, Idara hii ya Wanyamapori ni vizuri ijiangalie upya na utendaji mzuri ni wa kiaskari kama alivyosema ndugu yangu Mheshimiwa Mgana Msindai pale. Utendaji uwe moja kwa moja kuanzia Makao Makuu mpaka kwenye Wilaya. Sisi zamani kwa sababu tumehifadhi sana hao wanyama, mtu ambaye kijijini alikuwa anajulikana sana ni *game scout*. Leo hii katika kijiji changu, hakuna *game scout* na ni vijiji vingi havina *game scouts*. Wananchi

walikuwa wanamjua *game scout,* bwana shamba na mwalimu siyo bwana mifugo, sisi kule hatuna mifugo. *Game scout* alijulikana kwa kuwalinda kutokana na hao wanyama waharibifu na wakali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikija kwenye suala la mapato kutokana na uwindaji; mwaka jana nilimuuliza Waziri mapato ya Wilaya yangu kutokana na uwindaji kwa kipindi cha miaka mitano au sita, alinipa takwimu. Ukiangalia zile takwimu mwaka 2002/2003, vijiji vilipata milioni sita, pungufu ya ile asilimia 60 ambayo tunapewa kwa milioni tisa. Naona hizi takwimu sitoweza kuzitoa, kwa ujumla miaka sita vijiji vimepata milioni 147 na Wizara ikababakiza kwake milioni 442; sasa wapi na wapi? Tutafanya nini hata tukianzisha hizi WMA hao watawezaje na zile fedha zinazokuja Wilayani zinarudi tena kwa Mhifadhi wa Wilaya hata kama ana bajeti yake lakini naye anachukua asilimia 40?

Kwa hiyo, tunaomba Wizara ilifikirie sana hilo jambo kwa kuongeza kiwango ili tufikie asilimia 75 ije kijijini na asilimia 25 ibaki Wizarani. Vilevile waajiriwe *game scouts*, hatuhitaji *park wardens* ni aghali kuwasomesha. *Game scout* ni mtu tu ambaye ana elimu ya kawaida, *form four*, anaweza kwenda kozi ya miezi tisa pale Mweka akapata u-*game scout* wake, akaja akatusaidia kijijini. Kama hii kada mliifuta, naomba Mheshimiwa Waziri muirudishe tuwapate *game scouts* huko vijijini. Zipo sehemu kwa kweli zina matatizo; kila ukienda kutembelea wananchi lalamiko lao kubwa ni hilo, hakuna hata bunduki basi angalau hata kwa kutishia tu kwa kupiga juu hewani wale wanyama wakakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nisisitize tu kwamba, tungependa katika majumuisho, tupate majibu ya mgawanyo wa fedha hizi za uwindaji kama itabaki ile ile asilimia 25. Sisi tunaomba, nafikiri na wenzangu wote, wanaomba ile asilimia 75 iende Wilayani na asilimia 25 ibaki Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Castor Ligallama, nakushukuru sana kwa mchango wako mahiri kabisa. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Yono Kevela na Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nisiwe tofauti sana na wenzangu waliochangia, kuhusu Muswada wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori wa mwaka 2008. Niseme kitu kimoja kwamba, huu Muswada mimi ninauunga mkono kwa sababu mimi ni mdau na kwenye Jimbo langu kuna *Game Reserve,* ambayo inaitwa *Mpanga Kipengele Game Reserve.* Kwa hiyo, ninauunga mkono Muswada huu moja kwa moja, kwa sababu tunafaidika na uhifadhi wa *reserve* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie vitu vichache kuhusu suala la fidia. Fidia ambayo inatolewa hasa kwa wafiwa wanaoumizwa na wanyama wakali, kwa kweli ni kichekesho wanasema kifuta jasho; kwa nini waseme kifuta jasho wakati mtu

ameumia? Sheria hapo irekebishwe, itolewe *substantial amount* angalau hata milioni moja, milioni mbili, kwa sababu ile hela inaweza ikamsaidia mfiwa kuweza kuyakabili maisha ambayo yamekuwa ya juu sasa hivi.

Kwa hiyo, ningeshauri hapo kwamba, lile neno la kusema kifuta jasho lisiwepo, kuwepo na fidia ambayo ni halisi; mtu apewe kutokana na madhara aliyoyapata kutokana na yule mnyama. Mnyama yule alikuwa anaingiza fedha, watalii wanapokuja wawaangalia kwa mfano, tembo, samba na wanatoa hela. Kwa hiyo, kwa nini muanze kubania bania huyu; mtu aliyeumizwa na mnyama ambaye alikuwa anatunzwa na Serikali halafu tunashindwa kumlipa mfiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lingine nizungumzie fidia upande wa mazao. Waangalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba, wenzetu wanaotunza wale wanyama inapotokea kwamba mazao yameharibiwa, inatakiwa zile fidia nazo zilipwe kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nichangie kuhusu ruzuku. Idara nyingi za Wanyamapori ambazo sisi tunaishi nazo kule kwenye Halmashauri, naelewa Halmashauri nyingi hapa nchini ruzuku wanazopewa ni kidogo sana. Nitatoa mfano kwenye Wilaya ya Njombe ninakotoka, ile Halmashauri ilikuwa haipelekwi ruzuku kabisa. Tunaishukuru Serikali, kwa mwaka huu wa 2008/2009, imepeleka shilingi 2,400,000. Shilingi 2,400,000 ni kitu kidogo sana, tungeshauri kwamba, Serikali iweze kupeleka ruzuku ya kutosha ili wafanyakazi wanaofanya kazi walipwe na zile hifadhi ziweze kujiendesha kwa faida. Tuzisiachie Halmashauri, kwa sababu zina majukumu mengi; unaweza kuona Halmashauri inatoa kiasi kikubwa Wizara inatoa kiasi kidogo. Kwa hiyo, tulikuwa tunashauri kwamba, sheria zingerekebishwa angalau Wizara nayo ielewe kwamba, zile Idara za Wanyamapori ni za kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie kuhusu suala la mipaka, hicho ni kilio kikubwa kwa wananchi wangu. Mimi ninatoka Njombe Magharibi, kuna Kata kama za Luduga, kuna Vijiji vya Malangali, Mpanga Mpya, Luduga yenyewe na Mambegu, wananchi wana kilio kikubwa kwamba kila wakati wanaishi kwa wasiwasi, mara wanaambiwa mpaka huu, mara mpaka ule. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali wakati wanarekebisha hizi sheria, waangalie wananchi wasiwe wananyanyasika kwenye maeneo wanayoishi, kwa sababu kuishi jirani na *Mpanga Kipengele Game Reserve* isiwe sehemu kama ni mateso, inaonekana kama wanafaidika wanafurahia na suala la mipaka lionyeshwe mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri ananisikia, nilikuwa nashauri kwamba, tunaomba atusaidie ile mipaka ya zamani ndiyo wananchi wanayoipenda kwamba iwe vilevile, siyo kuonekana kama Vijiji vya Malangali vinafutwa katika jiografia eti tunawaachia wanyama. Tunaelewa kabisa, wananchi wanathamani kubwa kuliko wanyama na bahati nzuri pale kwenye *reserve* hakuna wanyama wengi ni kidogo sana; ni digidigi wadogo. Kwa hiyo, tulitegemea kwamba, wale wananchi hawatasumbuliwa kwamba kuna mipaka inaongezwa, ibaki ile ile mipaka ya zamani kwa sababu watu wamekwishazoea kuishi maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo nazungumzia pamoja na mipaka katika Kata ya Wangama Njombe, kule Kipengele na Imalilo watu wanaishi kwa wasiwasi sana; ile Milima ya Furahini watu wanasumbuliwa sana. Nadhani wananchi wananisikiliza sasa hivi, wanafurahia kwamba ninawatetea. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mnisaidie kwa hilo. Kama itawezekana, nendeni mkawahakikishie kwamba, hawatahama wanabaki kwenye ile mipaka yao waendelea na kilimo. Kule wanalima viazi, kuna mbao na kuna vitu vingi kwa kweli. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mnisaidie hilo, nendeni mkawaeleze wananchi kwamba, wasiwe na wasiwasi hawatahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie kuhusu *Wildlife Corridor* au njia za wanyama. Kule kwetu tuna bahati tuna *reserves* nyingi, sasa kuna vijiji kama vya Iyayi, Lyadengwa na Lyamkena, kuna njia za wanyama kwa sababu zile njie ndiyo zinazopelekea wanyama kwenda *Mpanga Kipengele Game Reserve.* Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, ikiwezekana ipeleke fedha, isisitize zile njia ziimarishwe kwa kuwezeshwa kwamba watoe hela kuwepo na uhifadhi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wanalalamika kwamba, kuna wanyama wakali, kuna wanyama wengi, lakini wanyama hawapo pale *Mpanga Kipengele Game Reserve* na kama wapo ni kidogo sana. Sasa nataka wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha, anieleza ni lini kule kutapelekwa wanyama, pamoja kwamba kuna upungufu wa wanyama katika sehemu nyingine? Tunaona kwamba, watu wamejitahidi kuondoka pale, lile eneo linakaa tupu hakuna wanyama. Sasa ni lini wanyama watapelekwa pale *Mpanga Kipengele Game Reserve*, lakini si kwamba naomba waletwe wanyama wakali hapana, isije ikaonekana kwamba naomba simba halafu watu wakaanza kuuawa kama ilivyo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka nizungumzie kuhusu suala la miundombinu. Tunarekebisha sheria na nilipokuwa nasoma hii sheria, wanasema lengo ni kuboresha; *provision for conservation, management, protection and sustainable utilization of wildlife products.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi na suala la miundombinu. Ninaposema miundombinu ni vile vitu vinavyohusiana na umeme na uwanja wa ndege. Kwa mfano, pale *Mpanga Kipengele Game Reserve,* kutokana na umuhimu wa shughuli ya *reserve,* Kanisa au KKKT Dayosisi ya Kusini, kulikuwa kuna uwanja wao wa Ilembula, waliona ni vizuri wangeukabidhi kwa Hifadhi nadhani ni *through TANAPA.*

Bahati nzuri tuliona kazi inafanyika pale, lakini mpaka hivi sasa naona kazi ile imekaa kimya na kile kiwanja kama kingetengenezwa kingesaidia sana kuleta watalii wengi. Uwanja wa Ilembula ukiwa ni Uwanja wa Maliasili, watalii watafika kwa wingi wakitokea Iringa Mjini wanakuja pale, wengine wanatoka Mikumi wanakuja moja kwa moja Ilembula, ingetusaidia sana. Vilevile ungeweza kusaidia hata hospitali jirani ya Ilembula pale, ambayo sasa hivi tunaipigania iwe Hospitali Teule ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *mutual relationship;* ni kweli umeme upo pale Wanging'ombe, lakini haujafika kwenye nyumba za Maliasili. Zipo nyumba za Maliasili lakini zinageuka kuwa magofu. Nyumba zile zingesaidia sana, kwa sababu tulitegemea pale pawe Makao Makuu ya *Mpanga Kipengele Game Reserve.*

Ninaona kama kuna ujanja ujanja unataka kufanyika, mara wanaenda Mbarali, mara Njombe, sasa hatuelewi tunataka msimamo wa Wizara; je, Makao Makuu ya *Game Reserve* yako wapi?

Sasa hivi tunavyofahamu, nyumba ambazo zimejengwa ambazo Serikali imepoteza fedha nyingi za walalahoi, zipo pale Kijiji cha Wangingombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri zile nyumba tuziboreshe haraka haraka ili Makao Makuu ya *Mpanga Kipengele Game Reserve* yawe pale Wangingombe. Tuna tatizo kidogo na Kijiji cha Wangingombe; hakina umeme, wenzetu wa *TANESCO* wamejitahidi kuleta *transformer* kubwa pale Wangingombe Sekondari, lakini tatizo ni suala la nguzo. Kutokana na mahusiano mazuri, tungetegemea Wizara mtusaidie kushirikiana na TANESCO ili nguzo zipelekwe pale wananchi wafaidike na ule umeme wa Kijiji cha Wangingombe, pamoja na Kijiji cha Utiga, ambavyo vimezungukwa na maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu lingine ambalo nataka kulichangia kwa sababu mchango wangu unaangalia upande wa Wilaya ya Njombe ilipo Hifadhi, nilikuwa najiuliza; watu walihama miaka ya nyuma, kwa mfano, Wananchi wa Mpangampya katika Wilaya ya Njombe, wameacha maeneo yao na waliahidiwa kwamba watapelekewa zahanati, watatengenezewa barabara na watapelekewa maji; lakini hali ilivyo mpaka sasa hivi wale wananchi ni kama yatima hakuna kinachofanyika pale.

Kwa hiyo, wakati tunarekebisha hii sheria kwa sababu hifadhi ni pamoja na kujali hali za wananchi, naomba zile huduma ambazo mlitegemea kuzipeleka mzipeleke kwa sababu wananchi wangu wanalia wanateseka. Hakuna msaada wowote unaopelekwa, kila kitu imeachiwa Halmashauri na uwezo wake ni mdogo. Kwa hiyo, tulitegemea ninyi wenzetu wa Wanyamapori sijui *through* TANAPA au nini, mngetusaidia ili ile hifadhi itusaidie. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba zile huduma ambazo ni za muhimu, mtusaidie ili wananchi wetu wapate kufaidika na hizo huduma.

La mwisho ni suala la uchumi; kwamba, hifadhi zinapokuwepo, kwa hiyo, naomba sana *Community Bank* ziimarishwe. Ahsante sana.

*(Hapa Kengele ya pili ililia kuashiri muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hiyo ni kengele ya pili. Nakushukuru sana Mheshimiwa Yono Kevela kwa mchango wako. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Zitto Kabwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. Nami napenda niseme kama ambavyo wenzangu wamesema kwamba, Muswada huu ni muhimu sana kwa ajili ya uendelezaji wa Sekta ya Utalii, Sekta ya Wanyamapori, lakini pia kuhifadhi maliasili ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu kama nchi. Kwa hiyo, ni Muswada muhimu sana, utaweza kusaidia na kuboresha maeneo ambayo yameonekana yana upungufu. Kupitia michango yetu, tunaweza kuboresha yale ambayo tunaona hayajakaa sawa kwenye Muswada, baada ya kupata maoni mbalimbali ya watu ambao wanahusika na Muswada huu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili ya jumla: Jambo la kwanza ni kuhusiana na maamuzi ambayo tumefanya asubuhi. Nimeona baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wana wasiwasi na maamuzi ambayo tumeyachukua. Nadhani kama nchi, lazima wakati mwingine tuwe tayari kuchukua maamuzi ambayo tunajua madhara yake, tupo tayari kukabiliana nayo, kwa sababu yana umuhimu kwa siku za usoni kuhusiana na Taifa letu.

Nilikuwa naongea na mzee mmoja ni Mbunge mwenzetu, akaniambia kwamba, wakati tunaamua kwenda vitani kupambana na Nduli Iddi Amini, hatukuwa na uwezo wa kupambana naye, lakini dhamira tulikuwa nayo, kama nchi tulienda vitani na tukampiga. Kwa hiyo, hata kama maamuzi tuliyoyafanya leo yatavuruga mikataba ambayo imeingiwa na kadhalika, lakini kama nchi tukiwa na dhamira ya kulinda rasilimali tutawashinda; cha msingi ni dhamira ya kuweza kusimama kidete kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo ningetaka kulizungumza pia ni kwamba, Taifa letu hivi sasa limeendelea kuwa Taifa linalotegemea rasilimali *(resource based economy)*. Kwa hiyo, wakati mwingine Miswada kama hii ambayo inahusu uvunaji wa rasilimali, kama nilivyozungumza asubuhi, inahitaji msaada mkubwa sana wa kitaalam. Baadhi ya nchi wanafanya *impact studies.* Nafahamu kwamba, kuna wadau wengi sana wametoa maoni mengi sana kwenye Kamati na tumeweza kuona maoni ambayo yamesomwa kwenye Kamati ni mazuri kabisa.

Maoni ambayo yametolewa na Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Sakaya ni mazuri kabisa kwa ajili ya kuboresha Muswada huu. Ipo haja kubwa sana huko tuendako, Miswada ambayo inahusiana na rasilimali za nchi iwe inaendana na *study* ambayo imefanywa, kuonyesha *implications* mbalimbali za jamii na za kiuchumi ili kuweza ku-*guide* Wabunge kwenye maamuzi ambayo tunayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ambalo ningependa kulizungumzia, linahusiana na mapato yanayotokana na tasnia ya uwindaji na ni vipi ambavyo Halmashauri zinavyofaidika na mapato hayo. Mkoa wa Kigoma, una mapori kadhaa na Halmashauri ya Wilaya Kigoma ambayo Jimbo langu lipo, ina mapori takriban mawili. Tumekuwa hatuna uhakika na mapato ambayo yanapatikana kutokana na uwindaji. Hali ni hivyo hivyo kwa Wilaya ya Kibondo, kuhusiana na Pori la Muyowosi na kadhalika.

Nilikuwa naangalia takwimu za Kiserikali kuhusiana na mapato ya utalii; Taarifa ya Hali ya Uchumi ambayo asubuhi nilii-*quote* wakati nazungumzia hoja ya

Mheshimiwa Mzindakaya, inaonyesha kwamba, mwaka 2007 Halmashauri 41 zilipatiwa jumla ya shilingi milioni 300 kutokana na mapato yaliyopatikana katika tasnia nzima ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha hizi ni asilimia tano tu ya jumla ya fedha zote, ambazo zilipatikana kutokana na tasnia ya uwindaji wa kitalii. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja zetu atufahamishe, kwa sababu kama ingekuwa ni asilimia 25 ya fedha zote Halmashauri zingepata jumla ya shilingi bilioni 1.8, lakini ni shilingi milioni 300 ambayo ni asilimia tano tu ya fedha ambazo zilipatikana katika tasnia nzima. *Specifically*, ningeomba kwa upande wa Kigoma, tupatiwe *schedule* inayoonyesha Halmashauri za Mkoa mzima wa Kigoma, ambazo zina vitalu vya uwindaji, kwa miaka mitatu iliyopita zimepata jumla ya shilingi ngapi na ni asilimia ngapi ya mapato yote ambayo yalipatikana kutoka Kigoma kutokana na uwindaji. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kuona ni vipi ambavyo hata hii asilimia 25 haifikiwi katika kupatikana kwa mapato hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningependa kulisisitiza sana ni sehemu ya tatu ya Muswada, inayopendekeza uanzishwaji wa Idara ya Wanyamapori, Kurugenzi ya Idara ya Wanyamapori, majukumu na watumishi watakaofanya kazi chini ya Mkurugenzi wa Wanyamapori. Sehemu hii pia inapendekeza mpangilio wa Taasisi na Uongozi. Aidha, inapendekezwa kwamba, usimamizi wa mapori ya akiba, ubakie chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, ambaye sifa zake zimeainishwa.

Sehemu ya saba ya Muswada inapendekeza matumizi ya wanyamapori, upigaji wa picha na kadhalika. Kifungu cha 37 kinapendekeza uundaji wa Kamati ya Ushauri ya Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii. Hili ndio eneo ambalo ningependa niliwekee mkazo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ambayo aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Diallo, aliunda Kamati kuhusu uboreshaji wa tasnia ya uwindaji wa kitalii Tanzania, ambao baadhi ya Wabunge walikuwa Wajumbe; moja ya pendekezo ambalo Kamati ilitoa ni kuunda Wakala wa Serikali wa Kusimamia Shughuli za Uwindaji wa Kitalii, badala ya Idara ya Wanyamapori. Muswada huu ulipokuja na hii taarifa ni ya mwezi Juni, 2006, baadaye ikaja hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya na baadaye ikaundwa *Task Force* ya Wizara kuangalia utekelezaji wa masuala yote haya ya uwindaji wa kitalii.

Ndani ya Muswada, utoaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii bado uko chini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na Kamati inayoundwa ni ya kumshauri tu Waziri. Kawaida Waziri anaweza akakubali au akakataa ushauri anaopewa na Kamati za Ushauri na tumeyaona haya kwenye Sekta ya Madini. Moja ya tatizo kubwa sana ambalo linaifanya nchi leo ilalamike kuhusiana na Sekta ya Madini ni kwamba, ugawaji na uingiaji wa Mikataba ya Madini uko chini ya Waziri tu na ana Kamati moja ya Ushauri kuhusiana na Mikataba ya Madini. Haya ndiyo mambo ambayo hata kwenye Kamati ya Mzee Bomani tuliyapendekeza kwamba, tuondoe nguvu ya mtu mmoja kuamua kuhusu

rasilimali za nchi. Kwa hiyo ni lazima tubadilike na nadhani ndiyo maana Kamati iliyoundwa na Waziri Diallo, ilipendekeza suala zima la Wakala wa Serikali.

Katika mijadala ya kuujadili huu Muswada, tulizungumzia sana uanzishwaji wa Mamlaka. Mamlaka inaonekana huku mwanzo tena imetajwa kwa ujumla ujumla kwamba, kutakuwa na Mamlaka lakini haielezewi hiyo Mamlaka inafanya shughuli gani na mambo kama hayo. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza Serikali ilete *schedule of amendment* ili *Part III* yote ya Muswada i-*establish* Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Majukumu yote yanayozungumzwa ndani ya Idara ya Wanyamapori, yafanywe na Mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 37 ya Muswada, inayozungumzia *Advisory Committee* kuhusu ugawaji wa vitalu, iunganishwe na *Part III* kwenye *institutional arrangement.* Moja ya *function* ya hiyo Mamlaka iwe ni kugawa vitalu na hapa tutaondoa matatizo yote ambayo yanatokea, kwa sababu tutakuwa na Mamlaka itakayokuwa na majukumu ya kufanya hivyo. Tumeona haya TANAPA; wanafanya kazi nzuri. Zipo hifadhi chache sana ambazo zinaingiza fedha nyingi *TANAPA*, hifadhi nyingine nyingi zinategemea Hifadhi za Kaskazini kwa ajili ya kuziendeleza. Hata yale mapori ambayo hayaingizi fedha nyingi, tukiwa na Mamlaka wataweza kugawa rasilimali vizuri na hata malalamiko ambayo Wabunge wanayo hivi sasa na kutaka asilimia 75 ya mapato irudi kwenye Wilaya na kadhalika. Iwapo tutakuwa na Mamlaka, yataweza kuangaliwa vizuri, kwa sababu Mamlaka itaweza kujua ni kiasi gani cha mapato ambacho watakitumia kwa ajili ya kufanya uhifadhi, utangazaji *(marketing)* na kiasi gani cha mapato ambacho kitakwenda kwenye Halmashauri zina hizo hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kutokuwepo Mamlaka ni la kimfumo kwenye Wizara nzima ya Maliasili na Utalii. Juzi tulikuwa tunapitia Hesabu za Bodi ya Utalii, ndani ya Wizara kuna *Licensing Agency* ya Utalii, Bodi ndiyo ina jukumu zima la *policy issues* za masuala ya utalii na kutangaza na kadhalika. Kwa hiyo, tukawa tumependekeza kwamba, ile *agency* inayohusika na kutoa leseni na kadhalika, iunganishwe na Bodi ya Utalii, kuanzisha Mamlaka ya Utalii ili kufanya kazi ya kuendeleza Sekta ya Utalii. Hiki kitu tuliki-*overlook* kwenye Muswada wa Utalii tulioupitisha mwaka jana, ambacho kinapaswa kuangaliwa. Hata kwenye Idara ya Misitu, tunapaswa kuwa na Mamlaka ya Misitu kwa ajili ya kudhibiti ili Wizara ibakie na kazi ya masuala ya kisera na masuala ya *coordination.*

Mfano mzuri ambao tumeuona jana wakati tunapitisha Muswada wa Sheria ya Maendeleo ya Biashara, tumeweza kuanzisha Mamlaka ya Biashara. Kwa hiyo, mtu ambaye ana *instrument* ya ku-*implement policy* ya biashara, inakuwa chini ya Mamlaka ya Biashara. Hayo ndiyo ningependa kuyapendekeza katika Muswada huu ili kuweza kuuboresha na kuhakikisha kwamba, nchi inafaidika kutokana na Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye Muswada huu. Kwanza, naomba

niweke bayana kwamba, mimi nipo kwenye Kamati inayoshughulikia masuala ya Maliasili, kwa hiyo, yale yaliyosemwa na Kamati nayakubali, lakini nilipenda niongezee mambo mengine kama kuboresha mapendekezo au mtazamo wa Kamati yetu. Nitajikita zaidi kwenye mambo mawili makubwa; moja ni suala la uwindaji endelevu na pili suala la ushirikishwaji wa Tanzania kwenye uwindaji wa aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwa kuzungumzia suala la uwindaji endelevu, niseme tu kwamba, uwindaji unaoendelea sasa hivi kwa ujumla sio endelevu kwa sababu kuu moja: Kuna vita kati ya binadamu na wanyamapori kugombea ardhi. Binadamu tunaongezeka sana hapa nchini, wakati maeneo yaliyokuwa yanatumiwa na wanyama, yanaendelea kupungua na wanaoumia ni wanyama. Kwa hiyo, matokeo yake kwa ujumla, tafiti zinaonyesha kwamba, wanyama karibu aina zote; ikiwa ni pamoja na wanyama wale wa muhimu kama simba, wanapungua kwa kiwango kikubwa sana kwa kila mwaka, iwe ndani ya maeneo ya hifadhi au nje ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inategemea sana rasilimali na uwindaji huu unategemea wanyama waendelee kuwepo, kama wanaendelea kubanwa na kupungua, ina maana mwisho wa siku hakutakuwa na wanyamapori na kwa hiyo, hakutakuwa na uwindaji. Suala hili la kuongezeka kwa binadamu v/s kupungua kwa wanyama kwenye maeneo yao kwa kawaida, halizungumzwi sana. Nimewahi kuzungumza hapa Bungeni mara nyingi. Wizara zinazohusika hazipendi kuzungumzia suala la kuongezeka kwa binadamu hapa nchini na kuleta sera inayoeleweka kuhusu tutashughulikia vipi ongezeko la binadamu hapa nchini. Nipo kwenye masuala ya mazingira kwani kuna matatizo yanayotokana na kutumia ardhi kwa kilimo na kuchunga, ardhi ambayo haiongezeki, lakini tumekaa kimya tu hatuzungumzii suala hili. Leo tunaanza kuliona hata kwenye uwindaji ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji unaoendelea umeachiwa wawindaji na kama wengi walivyosema, wawindaji wengi ni wageni ambao pengine hawana uchungu na nchi hii. Mapato yote yanayotokana na uwindaji yanachukuliwa na Serikali, fedha yote inakwenda Hazina na hakuna *retention.* Idara ya Wanyamapori, inapoomba fedha kwa ajili ya kuiendeleza na kuisimamia sekta hii, inapewa fedha kidogo, matokeo yake wawindaji wamepewa kazi ya kusimamia uhifadhi wa vitalu, kugharimia askari wale wanaolinda mapori. Vilevile maendeleo ya miundombinu kwenye maeneo ya uwindaji, yanagharimiwa na wawindaji. Ndiyo maana bei za uwindaji Tanzania, zimekuwa juu sana na hazikubaliki Kimataifa, hata baada ya kuzikataa zile zilizopendekezwa na Mheshimiwa Maghembe, zimerudishwa chini kidogo bado zinakataliwa.

Nimethibitisha mwenyewe kwamba, *rates* zetu ni kubwa kuliko nchi nyingine zote kwa ujumla wake, licha ya *fee* ile inayokwenda Serikalini, wawindaji wamejiwekea *fees* nyingine mbili na kumtoza mwindaji, yaani mlaji, nayo ni fedha kwa ajili ya uhifadhi, imewekwa pale kabisa kwa kila mnyama, fedha kwa ajili ya uhifadhi, kwa kila mnyama na kwa ajili ya maendeleo ambapo vitalu vipo. Ukijumlisha fedha inayokwenda Serikalini; ya *conservation* na ya maendeleo ya maeneo ya vitalu, unapata jumla ambayo ni kubwa kuliko nchi nyingine zozote katika Afrika.

Watalii wanakataa sasa hivi kuja kuwinda Tanzania, pamoja na maamuzi tunayoyafanya hapa, hawakubaliani na bei hizo. Kwa hiyo, Serikali inavuna ambapo haipandi, sasa utaratibu gani huu; kwa nini Serikali hai-*plough back* fedha inayopata ikishapelekwa Hazina na haijali tena uhifadhi wa wanyama wanaoleta fedha? Utaratibu huu ni wa ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwenye hili ni kwamba, Serikali ifanye mawili; aidha, kuwe na *retention* kusudi Idara ya Wanyamapori ipate fedha za kununulia magari na vitendea kazi kwa ajili ya askari na kulipia huduma za askari na usimamizi mwingine ambao mnauita uhifadhi. Kwa utaratibu wa sasa, kuna *zone* na magari yote yanarundikwa kwenye *zone*. Afisa mkubwa kwenye *zone* ndiye anayetumia magari hayo, leo anaendesha hili, kesho lingine. Furaha yake ni kuona *empire* aliyoijenga iko pale, lakini hakuna magari kwenye vituo ambavyo vinafanya kazi za doria. Suala hili niliwahi kulisema hapa kwa Waziri, lakini halikuchukuliwa hatua. Sasa aidha, tuweke *retention* au Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kugharimia shughuli za uhifadhi na maendeleo ya miundombinu na mambo mengine kwenye maeneo ambako uwindaji unafanyika. La sivyo, hata tungeweka hii sheria hatufiki popote na hatutapata wawindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa tuwe na tabia ya kufanya *evaluation* mara kwa mara ili kutathmini ubora wa vitalu hivyo ili pendekezo linalotolewa na Muswada huu kwamba, ifike muda tuone ubora wa vitalu umepungua, kusimamisha uwindaji ili namba ya wanyama au ubora wa kitalu urudie hali yake ilivyokuwa mwanzo. Kwa vile sioni hii *evaluation* ikizungumzwa, kuna haja kila mara ku-*evaluate* vitalu vyetu kujua vina ubora gani na kuchukua hatua, ikiwa ni pamoja na kusimamisha uwindaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwenye suala hili niseme kwamba, binafsi sitakubali kuingia mkumbo kwamba na sisi tubadilishe bei zetu zifanane na za nchi nyingine, kwa sababu Tanzania kwenye suala la wanyamapori ni *unique*. Tunahitaji kuendeleza *uniqueness*, lakini ni vyema tuangalie bei zetu kwa utaratibu nilioueleza. Tu-*maintain* bei zile ambazo zinaonyesha sisi ni tofauti, anayetaka kuja kuwinda Tanzania atapata ile *value added* na lazima watakuja, lakini tukiiga nchi nyingine tumekwenda na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninataka kuzungumzia kuhusu ushirikishwaji; lengo la Muswada huu ni kutaka Watanzania wengi zaidi, waingie kwenye shughuli za uwindaji; ni vyema na mimi ninaafiki kwa sababu wanyamapori ni mali yetu, tuna haki kufaidi kutokana na mali hiyo. Tukubaliane vilevile kwamba, biashara hii inahitaji fedha, inahitaji mtaji, inahitaji kununua vifaa vya uwindaji kama magari, lakini lazima ugharimie hawa *professional hunters*. Kwa utaratibu wa sasa, lazima mwindaji alipie uhifadhi na alipie miundombinu ya maeneo anayofanya uwindaji. Vilevile kuna umuhimu wa kufanya *marketing,* ndiyo maana kuna pendekezo la *transition period*. Tuwape muda Watanzania, watakapopata vitalu watahitaji kuwezeshwa kitaalam na kimaarifa, kwa sababu si suala la kukurupuka na kufanya uwindaji. Hiki kitu ni *profession,* lazima uwe umesomea, una ujuzi, unaelewa a, b, c, d’s za kufanya biashara ya

uwindaji. Sisi Watanzania hatuwezi, hatuna fedha, hatuna mtaji. Tunahitaji Serikali iwawezeshe Watanzania watakaotaka kuingia kwenye biashara hii kwa kuwapa mikopo na vifaa vingine ili waweze kushindana na Wazungu ambao wana uwezo wa vitu hivyo ambavyo sisi hatuna.

Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba, wale watakaopewa vitalu, wapewe elimu ya kutosha na wawezeshwe. Vilevile kuwe na muda wa watu kujiandaa na kujipanga. Mimi nimegundua kitu kikubwa kwenye uwindaji ni kufahamiana na *clients.* Wakala wa Tanzania ni hao hao wanaofanya kazi Kenya na nchi nyingine. Inategemea wauzaji wa vitalu vya Tanzania wanazungumza vipi na wawindaji hao ili kushindana na uwindaji katika maeneo mengine.

Kwa hiyo, tusipowawezesha, tusipowapa elimu na wasipofanya *marketing* ya kutosha, hawataweza kuwinda. Lengo letu la kuutaka huu Muswada ni kuwawezesha Watanzania kuingia kwenye biashara hii, kama haitawezekana tutashindwa tutawaachia Wazungu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tulikubaliana kufanya *Regulatory Impact Assessment,* ukitaka unaweza kuiita *EIA.* Muswada huu tayari umepambana na dhoruba tuliyoipata leo asubuhi. Kwa hiyio, lazima kutakuwa na athari na ni lazima Muswada huu ufanyiwe *Regulatory Impact Assessment* au *EIA.*

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. Nitangulize tu kusema kwamba, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Niliamua kuchangia kwa sababu mimi ni mdau katika suala hili la Wanyamapori. Sisi ni wafugaji kwenye maeneo yetu na tunafuga wanyama wa nyumbani wa kufugwa na wanyama wa porini, wote wanachanganyikana sehemu moja ni usiku tu ndio tunawatenganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kuishukuru Wizara kwa kulinda wanyama hawa, kwa sababu kuna kitu kinachoitwa uvamizi au mauaji makubwa sana ya wanyamapori katika nchi hii. Kama sio Wizara hii kufanya jukumu kubwa sana la kulinda wanyamapori, kwa kweli wanyama wangeisha kabisa. Kwa hiyo, nawashukuru *TANAPA,* Ngorongoro na Mfuko wa Wanyamapori, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Bado nasema tuendeleze uhifadhi wa wanyamapori, kwa sababu ni sehemu ya utajiri tuliopewa na Mwenyezi Mungu, ndio mafuta tuliyopewa Tanzania na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kwa gharama yoyote tujaribu kuhifadhi hawa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia faida tunayopata kutokana na wanyamapori, tuna maeneo matatu; tuna eneo la *National Parks* tuna hifadhi karibu 14, hifadhi nne tu ndio zinaendesha hifadhi nyingine zote. Kwa hiyo, ina maana tukiziimarisha hifadhi nyingine kumi zizalishe kama zinavyozalisha hizi hifadhi nne, nadhani itakuwa ni pato kubwa sana ambalo linaweza kuliongezea Taifa fedha nyingi sana. Kuna *game reserves* ambazo zina wanyama katika maeneo hayo. Vilevile kuna makambi mengi sana yaliyoko ndani na kuna watu wengi sana ambao wameajiriwa kwa ajili ya kuwalinda wanyama hawa.

Fedha nyingi sana zinakwenda kwenye ulinzi wa wanyamapori. Fedha nyingi sana zinatengwa na *TANAPA* na Ngorongoro na Mfuko kwa ajili ya kuwalinda wanyama hao. Hakuna fedha zinazotoka Hazina, ingawa fedha zote zinakwenda huko. Hazina irudishe fedha kwa ajili ya ulinzi wa wanyama. Hazina inabaki na fedha kwa ajili ya kulinda wanyama haitoi na asilimia 25 kwa ajili ya kuwapa jamii nazo hizo fedha zinakuwa shida zinakwama huko. Naona Waziri wa Fedha ananiangalia; ni kweli Hazina hairudishi fedha hizo. Naomba sasa zirudishwe, kwa ajili ya ulinzi wa wanyama na irudishwe asilimia 25 kwa ajili ya wananchi, jamii ifaidike na wanyama, ndiyo maana wananchi wanalia sana kwamba hasara ni kubwa kuliko faida tunayopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *WMA.* Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa kukubali suala hili la WMA. Naipongeza sana kwa sababu jamii inafaidika na inaona kwamba ni jukumu lao nao kuhifadhi hawa wanyama kama tunavyowahifadhi muda mrefu. Nadhani jamii yetu ni wahifadhi wakubwa sana wa wanyamapori. Kwa hiyo, tunastahili kama Serikali ilivyoamua kutupa ardhi, kuna ardhi ya vijiji na wamepewa hati ya vijiji vyao na kuna wanyama waliopo katika vijiji vile na walikuwepo tangu zamani wakiwa wanamilikiwa na Serikali, hatujawafukuza, hatujawaua. Kwa kuwa sasa tumepewa ardhi yetu na wanyama, nadhani tutawalinda zaidi. Naishukuru sana Serikali kuiondoa ile *game controlled area* iliyoko katika maeneo ya vijiji, ambayo ilikuwa ni kero sana kwa jamii, badala yake sasa imekuwa ni *WMA.* Naishukuru sana Serikali, naomba mzidi kutupa elimu na kuharakisha hili suala la WMA lianze mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawindaji walioko sasa na watakaokuja, hata Waheshimiwa Wabunge wanaotaka *blocks*, watakuja kuiomba jamii. Wote watakuja kwenye maeneo ya jamii kuomba hizo *hunting blocks*, lakini ni heshima Serikali ikawapa jamii isaidie katika kulinda baadhi ya maeneo na Wizara ibaki na *game reserve*, itakuwa ni kazi rahisi sana kulinda *game reserve* mkaachana na maeneo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba, ulinzi wa wanyama ulioko katika maeneo yote Tanzania ni gharama kubwa sana. Mpaka sasa zinahitajika hizo fedha kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi wanyama. Kwa hiyo, hata tukisema tusimamishe uwindaji kwa muda, itakuwa hakuna fedha zitakazoingia kwa sababu tumesimamisha uwindaji. Gharama ya kulinda na kuhifadhi wanyama ni ile ile, kwa hiyo, tutafute namna ya kuimarisha zaidi ulinzi wa wanyamapori ili baadaye tukiweka utaratibu, tukute wanyama wapo na tuweze kuvuna kwa utaratibu utakaokubalika.

Mimi nawapongeza sana wawindaji na uongozi wote, waliofanya kazi ya kulinda wanyama hawa, baadhi wameisha lakini kuna wanyama walioisha kabisa ambao hawaonekani nchi hii. Baada ya kusimamisha uwindaji wa aina hiyo ya wanyama, sasa wameanza kuongezeka. Kwa mfano, faru wameisha kabisa nchi hii, kwa sababu ya uwindaji haramu na sasa wameongezeka; kuna karibu zaidi ya faru 200 wapo Tanzania ingawa wakati ule waliisha mpaka kukawa na faru kumi. Tukiwalinda wanyama hawa kama simba na wengine wataongezeka, kama ulivyofungwa uwindaji wa tembo na sasa tumeanza kupiga kelele kwamba, tembo wameongezeka tunataka wavunwe. Kwa hiyo, ningeomba tuangalie sana uhifadhi wa wanyama hawa, tusiruhusu kuwindwa na waporaji kutoka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mimi nipo mpakani mwa Kenya na Tanzania; Wakenya hawawindi, lakini majangiri wengi sana wanatoka Kenya wanaua pundamilia, kwa siku wanaweza kuua pundamilia 30 mpaka 40 na kuchuna ngozi na kusafirisha kupeleka Kenya na hizo ngozi zinauzwa zinarudi Tanzania. Kwa hiyo, tusipoliangalia suala hili, tutakuta wanyama wameisha katika nchi hii. Naomba niseme tena kwamba, Serikali kama walivyofuta *Game Controlled Area* katika maeneo ya vijiji, hiyo *WMA* ambayo inaingia mbadala, ianzishwe haraka sana ili jamii iweze kukabidhiwa basi uhifadhi wa wanyama waliopo katika maeneo ya *WMAs*, waweze kupata utaratibu na sisi tuweze kufaidi wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nasema ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa masikitiko makubwa, nalazimika kuwa Mbunge wa kwanza, ambaye haiungi mkono hoja hii kwa sababu inakwenda kinyume na maslahi ya wapigakura wangu wa Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ni mzuri, lakini mgogoro dhidi ya Muswada huu na wapigakura wangu wa Tunduru, unaanzia Sehemu ya Nane, kifungu cha 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua ukurasa wa 49, Kifungu 70(i) kinasema, nitasoma kwa kiswahili: “Waziri anaweza, kwa kuzingatia maslahi ya Taifa baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha, kuandaa utaratibu wa kuwafariji kwa kiwango cha fedha waliofiwa, kuumizwa au kuharibiwa mazao na wanyama hatarishi.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinaendelea kwa kusema kwamba: “Fedha hizi zisichukuliwe kuwa ni haki kwao au isitafsiriwe kuwa ni fidia, kwa tafsiri nyingine hii ichukuliwe kwamba ni hisani ya Serikali.” Ukifungua Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, ibara ya 14 inasema: “Kila mtu anayo haki ya kuishi, kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa Sheria.” Wananchi wa Tunduru wanayo haki vilevile ya kupata hifadhi ya maisha yao.

Hapa tunazungumzia uhai na uhai huu utakuwepo endapo huyu mtu atakuwa amehifadhiwa vile vitu vinavyomhakikishia uhai wake, hii ni pamoja na mazao ya

kilimo. Sasa leo katika Muswada huu, kila kosa ambalo linafanywa na binadamu dhidi ya wanyama, imetolewa adhabu na uthibitisho upo katika kifungu cha 71(ii) kinasema hivi: "Mtu yeyote atakayemjeruhi mnyama hatarishi, anawajibika kutoa taarifa." Kifungu cha 71(iv) kinasema: "Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na vifungu vidogo vya (i), (ii) na (iii), atakuwa amefanya kosa na anastahili adhabu ya kulipa si chini ya shilingi 200,000 na si zaidi ya shilingi milioni tano au kifungo gerezani si chini ya miezi sita au si zaidi ya miaka mitatu au vyote kwa pamoja."

Binadamu anapomkosea mnyama, Sheria hii imesema moja kwa moja kifungo kitakuwa kiasi gani au faini itakuwa kiasi gani, lakini mnyama yule yule anapomkosea Mwananchi wa Tunduru inasema kwamba, Waziri atafikiria tena baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha na malipo hayo yasichukuliwe kwamba haki ili ni fidia na hisani ya Serikali. Waziri akitaka atatoa, asipotaka hatoi. Siwezi kuunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 70(ii), Muswada unasema kwamba: "Bila kuathiri kifungu kidogo cha (i), Waziri ataandaa utaratibu wa kutoa kifuta machozi. Kifuta machozi kwa maana ya fedha kwa watu watakaojeruhiwa, kuuawa au kuharibiwa mazao yao na wanyama hatarishi. Malipo hayo hayatazidi ukubwa wa shamba zaidi ya heka tano. Hapa maana yake, Mwananchi wa Tunduru akijaaliwa kulima heka 10 na kule Tunduru makundi ya tembo yanaweza yakawa zaidi ya 50; tembo 50 wakiingia kwenye shamba la heka 20 ni dakika 10 tu wameshaangamiza kila kitu. Leo mwananchi huyu ambaye ameahirisha mambo yake yote, mkewe anataka khanga, watoto wanataka ada ya shule, wanataka matibabu, wanasema subirini tulime shamba tuvune tutakachokipata basi tutanunua hayo yote. Tembo amekuja ameangamiza shamba la heka 10, Serikali inasema tutaoa fidia si zaidi ya heka tano. Kwa msingi huu, siwezi kuunga mkono Muswada huu mpaka marekebisho yafanywe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali fidia ya uharibifu wa wanyama hawa iwe halisia, kama ni heka kumi zilizoharibiwa basi malipo yawe heka 10 tena kwa thamani ya bei ya soko, kama ni mpunga debe moja linauzwa shilingi 6,000 basi iangaliwe heka ile moja ingeweza kuzalisha mpunga kiasi gani, ndiyo fidia ya mwananchi itolewe. Masuala ya kufumbafumba, kwa kweli siwezi kuyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 71(ii) kinasema: "Mtu yeyote atakayemjeruhi mnyama hatarishi, anawajibika kutoa taarifa kwa Afisa muhusika kama walivyoorodheshwa kifungu kidogo cha kwanza. Kati ya maofisa hao waliotajwa, hakuna cheo cha Afisa Mtendaji ambao ndiyo walioenea katika maeneo yetu. Vijiji karibu vyote vya Tunduru hakuna *Game Warden* na *Game Scout*. Utampata Afisa Wanyamapori au Afisa Misitu Tunduru Mjini. Vijiji kwa mfano Makande, Kazamoyo, ili uweze kufika Tunduru Mjini unahitaji kutumia siku moja na nusu. Gharama za kumtoa mtu Makande kwenda Tunduru Mjini zitalipwa na nani?

Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba, miongoni mwa watu ambao wanastahili kupokea taarifa hii ya kujeruhiwa na mnyama mharibifu, basi iwe pamoja na Maafisa Watendaji ambao wanapatikana katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifungua ukurasa wa tisa wa Muswada huu, ninapenda nipate ufafanuzi tu wa Mheshimiwa Waziri. Ukienda kwenye Kifungu cha pili, Matumizi ya Sheria imeeleza kwamba, Sheria hii itatumika Tanzania Bara. Ukienda kwenye tafsiri ya maneno, hakuna mahali ambapo pana tafsiri Tanzania ina-*reflect* wapi. Sasa ukienda kifungu cha 5(i)(a) kinasema kwamba: "Azma ya Sheria hii ni pamoja na ku-*promote and enhence the contribution of the wildlife sector to the sustainable development of Tanzania and conservation and management of wildlife and natural resources for the benefit of present and future generations, without any discrimination.*"

Sasa hapa inaonyesha kwamba, Sheria hii inazungumzia Tanzania na Tanzania tunavyoelewa ni Tanzania Bara na Visiwani. Nilitegemea itaeleza katika tafsiri kwamba, Tanzania wana-*reflect* wapi. Tunaomba maelekezo kutoka kwa Waziri kama kuna marekebisho yoyote yanaweza yakafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza awali kwamba, siungi mkono hoja hii, hadi hapo marekebisho muhimu yatakapofanywa kulingana na vile vifungu ambavyo nimevieleza. Nimetimiza wajibu wangu kama Mwananchi wa Tunduru na nimewaahidi kwamba, yale watakayonituma hata kama yana ukakasi mbele ya Viongozi wa Serikali, nitayafikisha kama yalivyo. Bahati nzuri ahadi hii niliitoa mbele ya viongozi wangu wa Chama, kipindi hicho Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi alikuwepo ha hakunikosoa kwamba, kauli hiyo sio sahihi. Kwa hiyo, ninachozungumza hapa ni sahihi kwa maslahi ya Wananchi wa Tunduru, ambao mimi ndiyo msemaji wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu. (*Makofi*)

**MHE. DKT. CHRISANT M. MZINDAKAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuchangia juu ya Muswada huu wa Sheria ya Wanyamapori.

Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake, kwa kuleta Muswada huu. Zaidi ya yote ni namna walivyotushirikisha sisi Wabunge katika kufikia hatua hii tuliyofikia. Kwa hiyo, natoa pongezi nyingi na shukrani nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kabla sijasema yale ninayotaka kusema, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia akili ambayo inatosha mwenyewe kuishi duniani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitaendelea kumkumbuka na kumshukuru Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliyesaidia taifa hili kupata uhuru. Mimi nilipata bahati ya kufanya kazi chini yake, alinisaidia sana kuondokana na unyonge. Mimi si mnyonge duniani. Kwa hiyo, kwa mambo haya mawili ambayo nimeyasema, ningependa sasa kutoa maoni.

La kwanza, baada ya kuwasikia Waheshimiwa Wabunge, hasa Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na ndugu yangu Lekule Laizer, nimekumbuka jambo ambalo nimekuwa nalifikiria siku zote, lakini leo nalisema. Mimi mkiniuliza na ningepata nafasi, kazi yangu ya kwanza ingekuwa ni kuweka Sheria ya Kufuta Kuua Wanyamapori kama biashara, yaani ningezuia vitalu vya kuwindisha na badala yake ningeanzisha *National Parks* nyingi na kuongeza hifadhi za wanyama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, niliwaomba Wajerumani wakakubali tukapata fedha za kutosha ili kupanua Hifadhi ya Katavi. Mzungu mmoja sitamtaja jina, akaniandikia barua kwamba, Bwana Regional Commissioner huelewi faida ya uwindishaji wa kitalii ndiyo maana wewe unataka kuchukua maeneo ya kuwindisha uyafanye hifadhi. Nikamwambia *you are a fool*, unawindaje wanyama bila kuwepo; lazima wanyama wawepo kwanza ndiyo utawinda. Huu ugomvi wote tumekaa hapa tunapiga kelele kwa maslahi ya watu wachache tu, tunatoka jasho hapa ndani ya Bunge, lakini maslahi yako wapi kwa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge jukumu letu la kwanza ni kutetea maslahi ya nchi yetu na watu waliotuchagua. Ndiyo maana ndugu yangu alipokuwa anasema, nilikuwa sijamuelewa aliposema ujumbe wa wananchi, nikasema ana haki maana ndiyo kazi aliyotumwa hiyo, sasa angesemaje? Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa kwamba, maelezo aliyoyatoa na ndugu yangu Mheshimiwa Lekule, lazima tuanze sasa kufikiri kwanza watu wanaongezeka, nchi yetu baadae itakuwa na watu wengi na hivyo tutahitaji ardhi.

Wanyamapori ni maendeleo, Mwenyezi Mungu alitupatia zawadi. Mimi ningefurahi sana kama mngesema tuanzishe Vyama vya Ushirika, Wananchi wa Tanzania wawinde wapate mboga. Nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, ikatokea mambo ya kuchekesha kidogo; nimefika pale kwa akina Juma Ngasongwa, nikakuta mama mmoja amekamatwa amewekwa ndani kwa sababu alikutwa amepika nyama ya tembo. Mimi niliwaambia Polisi nendeni mkamtoe huyo mama sasa hivi, halafu kanileteeni aliyeua tembo. Mtakamateni anayekula nyama, kasoro ya waziwazi.

Wananchi wa Kilombero anakotoka rafiki yangu Juma Ngasongwa kule, hawakuwa wanafuga ng'ombe, nyama ya porini ni nyingi, lakini ni marufuku kuwinda hata swala. Watalii wanakwenda kuwinda, nyama na ngozi wanaibeba. Wananchi wenye mali hawawezi hata kula mboga; sasa haya mambo mnayaelezaje? Mimi ningefuta biashara yote, wanatuletea maneno ya kugawanyika hapa bure tu na nchi haina faida yoyote kwa jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kumuunga mkono Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, ambalo muda wake uliisha ni kuwa ndani ya Muswada huu Waziri atakuwa na Mamlaka ya kutengeneza *regulations* ambazo zinasaidia namna ya kugawa vitalu. Ili mtu apate kitalu, kwa utaratibu wa sasa, lazima Kamati imkague au wataalam wakamkague wakute ana mahema, magari na fridge ndipo wamjadili. Kwa utaratibu huu, haiwezekani Mtanzania wa kawaida akapata kitalu kwa sababu

kinachotangulia ni mtaji alionao. Sasa kama mtu ameonyesha vitu na hakupewa kitalu anafanyaje?

Viongozi wetu mmepewa madaraka kwa niaba yetu, ninaomba Wizara ya Maliasili, pamoja na Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kutumia *Empowerment Act* tuliyoipitisha wenyewe na kubaki makaratasi tu; tutengeneze programu ya kuwawezesha Watanzania. Ijulikane kabisa kwamba, wewe ukipewa kitalu utapewa muda wa miezi sita kujiandaa na barua aliyopewa imuwezeshe kwenda Benki kupata mkopo. Hayo ndiyo yatakuwa mapinduzi. Sisi tuna sera nzuri na mipango mizuri ya uwezeshaji, lakini haitekelezeki kwa sababu hatujarudi kwa wale wasionacho, bado tunahangaika na walionacho; sasa hii haiwezi kutusaidia. Kwa hiyo, mimi naunga mkono maneno ya Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, lakini kuwe na mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikiwa hai mwaka kesho, nitakuja kuuliza watu wangapi wa Tanzania wameandaliwa ili wafaidi matunda ya nchi yao. Lingine, ndiyo maana nasema mimi si mnyonge, mara nyingine nashindwa kuelewa; nilikuwa Mwenyekiti wa *SIDO* wakati ule na nilifanya kazi na Mramba, tulikuwa tunajenga *Industrial Estate,* tunapeleka watu Ulaya kusoma wakirudi wanarudi na mitambo. Hatukuwahi kumpa tajiri yeyote mkopo, tulijifungia kwenye Bodi tukasema ni wanyonge *and we did it* na hatukupiga kelele hadharani, lakini tulitoa mikopo na Watanzania walikuwa wanalipa *80 percent* ya mikopo tuliyowapa. Sitaki kusema tuliwazuia akina nani, lakini tulilizuia kundi fulani kwamba lina uwezo hatuwezi kuwapa mikopo.

Lazima watu wenye *political will* muamue wenyewe namna ya kusaidia watu wenu, kama hamtaki basi. Sisi Wabunge wote hapa ni *transit passengers*. Bunge litaendelea kuwepo, wananchi wataendelea kuwepo, lakini *individuals* hatuwezi kuendelea kuwepo. Wale marafiki zangu Mawaziri kule ni *transit passengers*, kwa uhakika ni huku mnakotuona tulipo, sasa haifai kusahau. Wananchi wanainua mikono hawawaoni viongozi wao, hii haitakiwi, lazima tugeuke tena sio kugeuka kwa shingo, geuka mwili mzima uone walio nyuma yako na tuwasaidie kwa dhati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kiongozi mmoja alisema Waswahili wakipewa vitalu wanauza au wanapangisha wageni; sasa angefanyaje wakati hana uwezo, uwezo wake ni kupangisha apate dola zake ishirini hizo ale na watoto wake? Mngemuwezesha angeingia, hata *participation* inahitaji fedha. Kwa hiyo, mimi nasema msingi wa mambo yetu ni kuamua kusaidia watu wasio na uwezo na ndiyo walio wengi katika nchi na ndiyo waliotuleta hapa Bungeni. Kwa nini tunahangaika na kundi la watu wachache? Huo ndiyo ujumbe wangu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka niliseme ambalo ni unyonge; Viongozi wetu tunatembea duniani, hivi mkitembea duniani unakwenda kuona kama mtalii au unajifunza jambo? Faida ya kutembea duniani ni kujifunza, uige yale mazuri. Kote huko tunakokwenda, kila watu wana kanuni na taratibu zao, kwa mfano, ukienda Uarabuni kote hakuna mtu atakayepewa ardhi wala shamba, wala hataruhusiwa kuanzisha mradi bila kuwa na mwenyeji wa nchi ile. Hiyo ipo ndani ya Sheria. Sisi

tukitaka kuweka Sheria, tunabanwa kwa sababu ya unyonge wetu, kana kwamba tunataka kufanya dhambi kwa Mungu.

Mimi nilikwenda Malaysia; utajiri wote wa Wamalesia upo kwa Wachina. Nilikwenda mara mbili Malaysia na mara zote nilipata nafasi ya kukutana na Waziri Mkuu wa wakati ule, Mahatim Mohammed. Akaniambia kwamba, Mr. Mzindakaya *let me tell you* hawa Wamalesia tumekaa tunawatawala, lakini uchumi wote upo mikononi mwa Wachina. Wakaanzisha mpango wa hadharani, sio wa kujifungia chooni, kuwasaidia Wamalesia nao waingie kwenye uchumi. Sisi ukisema hapa ni kama unakufuru kwa Mungu, lakini wao ni nani si tule sote?

Mgeni aje kuwekeza pamoja na mwenyeji, wala mimi sisemi wageni wasije kwa sababu wageni wasipokuja hamuwezi kuendelea, lakini kwa nini wale peke yao si tule sote mbona kwingine wanafanya? *Investments* za Uarabuni ni kubwa kuliko hapa, mbona Wazungu hawajakataa kwenda kule kwa sababu wale wameweka sheria ya namna ile. Kwa hiyo, ninasema katika mambo ya maslahi ya nchi yetu na watu wetu, tusiwe wanyonge. Unyonge ni mbaya; hata hii tuliyokuwa tunabishana asubuhi, watu wengine bado wananung'unika; tumeshamaliza kazi asubuhi wewe Mbunge bado unanung'unika; ulichokosa ni nini? Tumeshamaliza kazi asubuhi wewe bado unalia mchana huu, aise tukoje, wewe unamwakilisha nani hapa? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeanza mchezo mbaya sana, inapofika kuzungumzia maslahi ya nchi yetu, kuna kundi la wanaofaidi linakuja kutugawa hapa Bungeni. Hatuwezi kuwa na Bunge linalogawanywa kwa maslahi ya watu wachache, wanahamia hapa kufanya kampeni. Hata jana kuna watu walikuwa wanatembea, hawataki kulala kwa ajili ya vitalu vya Wazungu; wanaumia nini mimi sielewi? *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu. Mimi nimeifanyia kazi Sheria iliyopita, ambayo inafutwa kwa Sheria hii kwa miaka yote niliyokuwa Serikalini, naifahamu vizuri na nimepata fursa ya kipekee kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na wenzangu katika Kamati kupitia Sheria hii ambayo leo ipo hapa mbele yetu. Tumeifanyia marekebisho makubwa sana, mpaka ikafikia kipindi cha kuichapisha upya kabisa. Napenda kwa hatua hii, nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Wataalam wao, kwa usikivu mkubwa waliokuwa nao wakati tunafanya mabadiliko makubwa katika Sheria hii, ambayo yameifikisha mahala hapa ilipo. Kwa kiasi kikubwa ni Sheria ambayo inaweza ikatusaidia kutupeleka katika hatua nyingine katika uhifadhi wa maliasili ya wanyamapori katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya uhifadhi wa wanyamapori, yanazidi kupungua kwa sababu idadi ya watu inaongezeka. Kila mahali kama mnavyojua, tuna tatizo kidogo na sera yetu ya makazi, ambapo mtu anafungasha virago anahamia popote pale anapoamua kuanzisha makazi yake bila utaratibu. Kwa hiyo, maeneo mengi ambayo

ni mapito ya wanyama, yamefungwa kwa mashamba na makazi. Tatizo la uhifadhi wa wanyamapori na changamoto zake ni kubwa zaidi tunakokwenda, kuliko hata tulikotoka. Matarajio yetu ni kwamba, Sheria hii itakuwa ni sehemu moja ya kusaidia na kuona kwamba, wanyama wetu hawa wanaweza kuwepo kwa vizazi vijavyo. Tumepoteza maeneo mengi ya hifadhi na wanyama wengi wamepotea na kuwarudisha itakuwa ni kazi kubwa sana. Suala hili la ongezeko la watu, imefika mahali ambapo lazima sasa tulizungumze vizuri na mtawanyiko wake; vinginevyo ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ni Kamati makini, ya uhakika na yenye Wajumbe makini kama zilivyo Kamati nyingine za Bunge. Yalisemwa maneno ya kejeli asubuhi kuhusu Kamati hii, nimesikitishwa sana. Mambo kama haya katika Bunge si mazuri, tutafika mahali katika Bunge hili watu hawatasema ukweli, watabakia watu wachache wanachokisema ndicho kitawale siku nzima. Tutajikuta tanakwenda pembeni na hakuna anayeweza kutuambia kwamba kazi hili vipi, kwa sababu ya vitisho vinavyoendelea na mambo yanayoendelea mpaka kufika mahali kuidharau Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kusema ni kwamba, hii ni Kamati makini, ina watu ambao baadhi yao ni wataalam waliobobea akina Mheshimiwa Prof. Mwalyosi na wengine, hata mimi mwenyewe. Mtaona hata mjadala wa asubuhi, hakuna Mjumbe hata mmoja aliyepata fursa ya kuchangia. Kwa hiyo, maoni mazima ya Kamati hayakupata nafasi. Sasa ushauri wangu, mbele ya safari twende taratibu, tutafika tu mahali tunapopataka kwa kushirikiana kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii, lipo jambo moja muhimu sana niliseme mapema; Sheria inapendekeza kuunda taasisi mpya *(Wildlife Authority)*, itakayosimamia shughuli ambazo hivi sasa kwa kiwango kikubwa zinafanywa na Idara ya Wanyamapori. Jambo hili halikuwemo, tumelipendekeza sisi kama Kamati, tumelishikilia mpaka sasa limo ndani ya Muswada huu. Jambo hili ni ukombozi mkubwa sana huko mbele tunakoenda. Sheria hii itatusaidia sana Shirika hili likianza mapema. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali baada ya Muswada huu kupita, hebu mchakato wa kuanzisha taasisi kubwa itakayotusaidia maeneo yote nje ya Ngorongoro na *TANAPA*, uende kwa haraka. Wenzetu Kenya ndivyo walivyo, wana *Wildlife Service*. Wenzetu Uganda wana *Uganda Wildlife Authority*, wenzetu Zambia wana *Zambia National Park Services*. Zimbabwe pia wana shirika moja kubwa. Sasa sisi Ngorongoro iendelee, *TANAPA* iendelee, lakini tuwe na shirika kubwa litakalosimamia mambo yote haya yanayohusiana na masuala ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nisemee kidogo sana kuhusu hapa tulipo; tumekwishafanya maamuzi, lakini kwanza nianze kwa kuuliza kwa nini kuna uwindaji wa kitalii? Hii ni *concept* ambayo imekuja kutokana na ukweli kwamba, wanyamapori walioko Tanzania, walioko Uganda, walioko Kenya na sehemu nyingine, lazima uhifadhi wao kwa namna moja au nyingine, utokane na mapato yanayotokana na wanyamapori wenyewe, ndio maana inaitwa *resource*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kitu hakina faida, hakileti uchumi, hakiwezi kuwa ni rasilimali. Kwa hiyo, rasirimali ya wanyamapori lazima ituletee uchumi; sehemu fulani ya uchumi tufanye kwa maendeleo yetu ya nchi na sehemu fulani ya uchumi huo tuhifadhi wanyamapori. Hatuwezi kuwa na wanyama ambao hatupati uchumi, wamekaa tu pale, tuchukue hela ya mkulima ya pamba twende tukahifadhi wanyamapori! Hilo kulieleza kwa wananchi baadae tutapata tabu, ndio maana basi ya hii kitu kuingia kwamba, una pori kama *Selous Game Reserve*, unao Tembo 40,000 ndani ya *Selous Game Reserve* au zaidi, natoa kama mfano; kati ya 40,000, unaamua kuvuna madume 100; katika 40,000 ukitoa 100 una hasara gani? Wale 100 unawauza kwa bei nzuri kwa matajiri wa dunia wanaoweza kuwinda vizuri na si lazima wawinde wote 100 maana wanawalipia. Wale wanaweza kulipa hata wasimuwinde, lakini ameshalipa. Fedha unayopata ya wale Tembo 100 ndio unalinda hawa 39,900, ndiyo *concept* yake, ndivyo Idara ya Wanyamapori inavyokwenda; ni fedha zinazotokana na uwindaji ndizo zinasaidia kulinda mapori yetu yote ya akiba.

Kwa hiyo, ukisema hapa inawezekana, tusifanye hivyo; inawezekana kweli? Maana yake ni kwamba, Waziri wa Fedha awe tayari kutoa mabilioni ambayo yangeenda kwenye elimu, kwenye afya na mambo mengine, yaende kuhifadhi wanyapori. Unaweza kufanya kwa mwaka mmoja, miwili, lakini huwezi kwenda mbali, mwisho wa siku itakuwa tabu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unawinda kidogo sana ili kulinda walio wengi sana, ndiyo *concept* yake. Ndiyo maana basi Zambia uwindaji upo, Msumbiji upo, Zimbabwe upo, Namibia upo, Botswana upo, South Africa yenyewe upo na unaendelea kwa sababu hiyo. Unachukua katika wanyama wachache ili kukusaidia kulinda wale walio wengi. Ndiyo maana hata mfugaji anauza dume moja au mawili, anapata fedha za kumsaidia kuweza kuhifadhi lile kundi kubwa lililoko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nilitaka kulizungumzia ni moja tu kwamba; ni muhimu kwa Serikali ifanye *impact assessment* ya maamuzi yetu ili ijiandae kukabili vizuri yatakayotokana na kilichotokea, maana uamuzi wowote una *prons* and *cons*. Tufanye *impact assessment* mapema na tujiandae na yatokanayo mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mikumi tulikuwa na hoteli, yakafanywa maamuzi fulani fulani ya haraka haraka, ile hoteli imekufa na leo wala haipo na mwenye hoteli amelipwa na Serikali shilingi bilioni tatu kufidia gofu kwa sababu ya haraka fulani na kwa sababu haikufanyika *impact assessment* mapema. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, ifanyike *impact assessment* ili kuziba mianya yoyote ile ambayo inaweza ikatokea. Mheshimiwa Waziri, katika hilo, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, itakuwa tayari kushirikiana na Serikali, kuangalia katika mazingira haya sasa tujaribu kukaa vizuri maeneo gani, tusije tukajikuta katika kona ambayo ni ngumu sana, ambayo nisingependa kuisemea katika eneo hili ambalo ni kama mkutano wa hadhara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, la mwisho kabisa, niiombe Wizara ya Fedha, iangalie sana Mapori haya ya Akiba; *National Parks* hazina tatizo sana, Ngorongoro haina tatizo sana, wana fedha zao wenyewe wanazokusanya, vilevile wana

wafadhili wengi. *Game Reserves* nyingi zina shida kubwa sana, kwa mfano, Rungwa *Game Reseve* ni kubwa sana, ina maeneo matatu; ina Rungwa, Mgwesi na Kigosi ni kama *Reserves* tatu ndani ya moja. Wana magari manne; mawili mazima, mawili mabovu. Magari mawili huwezi kwenda kwenye mapori matatu; kwa hiyo, kuna maeneo ambayo kabisa mwaka unaisha, hakuna askari wa wanyamapori amewahi kukanyaga maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiwezeshe Idara ya Wanyamapori katika eneo la *Anti-Pouching*, vinginevyo ujangili ambao sasa hivi unaendelea, utakuwa mkubwa sana katika miaka mitatu, minne, hatutakuwa na kitu. Tuiwezeshe Idara ya Wanyamapori kimiundombinu, waweze kutengeneza barabara, waweze kuweka mapori haya katika mazingira ambayo yanakubalika ili yafikike. Tuiwezeshe Idara ya Wanyamapori katika kuwawezesha watumishi wake kuweza kuwa na moyo wa kufanya kazi. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, yenye mbung'o, wanyama wakali, yenye makorongo makubwa, mito, wakati wa masika mvua inawanyeshea huko porini, mishahara yao ni midogo sana. Tuwaangalie kipekee watumishi hawa ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuangalie idadi ya wafanyakazi. *Selous Game Reserve* ni sawa sawa na Rwanda na Burundi kwa pamoja ni kubwa sana, kilomita za mraba 50. Miaka kumi iliyopita, *Selous Game Reserve* ilikuwa na watumishi 600, mimi nikiwa ni mmojawao; leo hii ninavyoongea ina watumishi 280. Watumishi 280 kuangalia Rwanda na Burundi, haiwezekani! Kwa hiyo, lazima idadi ya watumishi iongezeke. Kwa utaratibu huo, tutajikuta rasimali yetu hii ya wanyapori itaisaidia nchi yetu na itaendelea kuwepo katika vizazi vijavyo, kama ambavyo tumedhamiria katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, nimalizie kwa kusema, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ni Kamati makini, yenye watu wenye uhakika, wanaotoa ushauri ambao ni wa uhakika, ningeliomba iheshimike kama Kamati nyingine, isidharaulike hata kidogo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu mdogo au mfupi katika kuchangia Muswada huu wa Hifadhi za Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa na wenzangu na kwa hiyo mchango wangu utazidi kuwa mfupi. Nitapenda tu kuendelea kusisitiza baadhi ya maeneo nikizingatia kwamba, mimi siyo mtaalam sana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni wa kuboresha huduma na hifadhi ya wanyapori na huduma endelevu kwa ajili ya kuboresha mapato yanayotokana na maliasili yetu kwa manufaa ya Watanzania. Eneo ambalo nimelifurahia zaidi ni pale ambapo nimeona imesisitiza kwamba, maliasili ama wanyamapori wetu sasa watawanufaisha wale wananchi ambao pia wanakaa katika maeneo ya hifadhi, jambo ambalo mwanzoni halikuwa limetiwa msisitizo wa kutosha. Kwa ajili hiyo, niungane na wenzangu kusema kwamba, Muswada huu basi umekuja kwa kuchelewa kwa mambo makubwa mawili:

Kwanza, kwa kuwa tunayo maliasili hii miaka mingi iliyopita; miaka nenda rudi tunao wanayama wazuri tu Tanzania yetu hii katika hifadhi zetu, lakini wananchi hawakuwa wananufaika. Sasa kama huu Muswada utashirikisha wananchi kunufaika na mazao yanayotokana na wanyamapori, basi niseme kwamba umechelewa, lakini basi wananchi wategemee kunufaika nao na kwa hiyo ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwa kuwa wananchi ama jamii zinazozunguka hifadhi zitanufaika, nadhani hii itapunguza mikwaruzo na mitafaruku ambayo ilikuwa inatokana na mipaka na mambo kama hayo na hivyo, uboreshaji huu utaenda sambamba na manufaa hayo na faida zinazotokana na wanyamapori zitaweza kuwa za manufaa hata kwa kuongeza Pato la Taifa. Kwa hiyo, sheria hii inaweza ikarahisishwa kwa sababu itaonekana ni hifadhi shirikishi kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria hii inalenga uboreshaji endelevu kwa maana ya kuboresha *Game Reserves, Game Controlled Areas, Corridor Areas, Marine* na kadhalika, naamini kwamba, suala zima la utandawazi hapa halitatugusa, kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Mwalyosi kwamba, tunao *unique animals* Tanzania. Kwa hiyo, hapa tunachoboresha siyo wanyama, tunaboresha huduma na utendaji na kwa hiyo, nadhani suala la utandawazi hapa halitakuwepo kwa maana ya kwamba, hatutakuwa na *competition* ya namna yoyote. Pato letu la taifa litaongezeka maradufu kutokana na uboreshaji huu na hasa kutokana na Muswada huu kadiri utakavyokuwa umeboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hatuhitaji kuboresha wanyama, bali tunahitaji kuboresha huduma za hifadhi kama tulivyoboresha mikataba. Wanyama ni rasilimali yetu ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu, kama jinsi ambavyo Tanzania tulipewa madini na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, kwa kuwa tunaboresha huduma, ninadhani pato letu litaongezeka maradufu na kwa hiyo, Watanzania tutaendelea kunufaika na wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka niongezee, nimeisoma soma kiasi, lakini sijaona mahali ambapo Muswada umesisitiza suala zima la *Game Viewing* kwa mfano. Nadhani tunapata pato katika nchi yetu linalotokana na watalii wanaokuja kuangalia wanyama. Sasa katika eneo hili, sijaona Muswada umesisitiza suala la usalama wa watalii kutoka nje kwa sababu katika *incidences* chache, imetokea kwamba, pengine wengine wameporwa mali zao na wengine wameweza kuuawa na mambo kama hayo.

Sasa ninadhani ni vizuri pia Muswada ukagusia jinsi ambavyo watu hawa wanaokuja kutuongezea pato letu kwa kuangalia wanyama, nao wakawekewa usalama ama sheria ya aina fulani. Kwa mfano, hata magari yale watalii wanayotumia kwenda mbugani, mara nyingi utakuta ni magari ambayo ni ya watu binafsi na usalama wake hauna uhakika. Kwa hiyo, ninadhani ni wakati muafaka kama tunataka kuboresha utalii wa nchi na tunataka kuwa *unique* ni eneo la kuliangalia kwamba watalii walindwe ipasavyo na usalama wao uangaliwe vizuri na pia vyombo hivi wanavyosafiri navyo vihakikiwe na Serikali na hatimaye itakuwa ni hifadhi endelevu na mapato yetu yatazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imekwishasemwa, nchi yetu ina mapori makubwa, lakini kama nilivyosema, mimi siyo mtaalam. Vilevile nadhani kuna wataalam wanaosomea katika fani hii ambao wanaweza wakaendesha *Environmental Impact Assessment*, kuona ni mapori yepi ambayo yanaweza yakawa kwa ajili ya hifadhi na hatimaye kupanua maeneo ya kuhifadhia wanyama. Tulisikia vilevile kwamba, *population* ya nchi yetu inaongezeka na kwa hivyo, maeneo yanakuwa madogo. Bahati nzuri tuna mapori makubwa ambayo wataalam wanaweza waka-*assess*, wakaona kwamba tunaweza tukahamishia wanyamapori. Sielewi uwezekano wa namna hiyo; ni mawazo ninayatoa, lakini nadhani ni sahihi vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nadhani ni vizuri kufanya *survey* na kuangalia misitu ambayo inaweza ikatupa manufaa. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Manyara, tuna msitu mmoja wenye manufaa makubwa sana unaitwa SULEDO, upo katika Jimbo la Kiteto, nadhani Mbunge wa Kiteto atakubaliana na mimi. Mimi nilibahatika kuuona huu msitu ambao unajulikana na una hata wafadhili kutoka nje, jinsi ambavyo umeweza kuwanufaisha wananchi wa eneo hilo. Hifadhi hii ni kubwa sana, ambayo inajumuisha Tarafa tatu za Wilaya na ndio maana ukapata jina la SULEDO (Sunya, Lengatei na Dongo). Sasa ninadhani ni wakati muafaka kuiga msitu huo ili iweze kuanzisha misitu mingine ambayo inaweza ikaboreshwa, ikawanufaisha wananchi hasa wale wanaoishi maeneo ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulisisitiza tu, kwa kuwa sheria hii inalenga hifadhi shirikishi, nadhani ni vizuri kutoa tahadhari kwa wale ambao watakiuka taratibu hizo ambazo zitawekwa, kwa sababu mara nyingi kuzuia ni bora kuliko kutibu. Kwa hiyo ni vizuri sheria hizi zikatafsiriwa kwa lugha nyepesi, ambayo wananchi wanaweza wakaisoma kwa urahisi kwa sababu wengine wanaofanya uovu katika maeneo ya hifadhi, pengine wanafanya si kwa kutaka ni kwa kutoelewa sheria hizo. Watakapokuwa wamesoma na kuzielewa, wataweza kushirikiana na Serikali ili kuweza kuhifadhi vizuri wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka niongezee tu kwa msisitizo ni eneo la watalii wa ndani. Mara nyingi tumekuwa tukiegemea watalii kutoka nje, kuongeza pato kwa kuja kuangalia mbuga zetu za wanyamapori na kadhalika. Ninadhani ni wakati muafaka kusisitiza ama kuhamasisha wananchi wetu wa Tanzania, wakati ule wa *off Season* ambao hatuna watalii kutoka nje ni vizuri wakawa na tabia pia ya kwenda kuangalia wanyama ili kuongeza pato, lakini kwa bei ambayo ni *affordable* kwa Watanzania ili iwe sehemu ya kuongeza pato la taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa kusisitiza tu kwamba, kwa kuwa sheria hii imeonyesha dhamira ya Serikali kushirikisha jamii katika hifadhi na katika kunufaisha, ni vizuri kama jana tulivyosikia pendekezo kwamba, hata hizi Bodi zinazoundwa za Wanyapori, zikawahusisha ama zikawa na wawakilishi wa kuwasemea wananchi, kwa sababu kuna maeneo nimesoma huku kwenye Muswada kwamba, Muswada pia unathamini *indigenous knowledge* ya wananchi. Ninadhani wananchi

wanaweza wakawa na mchango mkubwa kama watakuwa na ushiriki katika Bodi na Bodi ziwe na uwakilishi wa wataalam wenye kutoa mchango mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Martha Umbulla. Waheshimiwa Wabunge, nilisema ningemwita Mheshimiwa Luhahula, lakini amesema kwamba mchango wake ameshautoa kwa maandishi na hivyo basi ameruhusu niendelee na anayefuata. Basi nitamwita Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda ajiandae kama muda utaturuhusu.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tunavyofahamu, wanyama ni rasilimali nzuri sana na ya muhimu, tukiitumia vizuri tutanufaika kama nchi, lakini pia ni rasilimali ambayo isipotunzwa vizuri, inaweza ikatoweka, kwa sababu siyo siri, kuna maeneo mengi ambayo wanyama hawapo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria hii inakuja kwa wakati muafaka; ni wakati tunapohitaji sana kutazama rasilimali zetu na kuona jinsi ya kuhifadhi na kutumia rasilimali hizo kwa manufaa yetu sisi wenyewe na manufaa ya vizazi vijavyo. Sheria ambazo zimekuwa zikitumika mpaka leo, kwa kweli zilifaa kwa wakati ule kwa sababu ni sheria zilizotungwa katika mazingira ya wakati huo. Changamoto zimebadilika na kwa sasa tunapaswa kuwa na mbinu mpya, mikakati mipya, pamoja na sheria mpya zitakazotusaidia katika uhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea maeneo mchache; moja, nianze na Mamlaka inayopendekezwa kuundwa kwa mujibu wa Muswada huu kama unavyopendekeza. Hili ni wazo zuri, lakini kule mbele tunakoenda, ningelipendekeza kutafuta namna ya kuwa na Mamlaka itakayounganisha *TANAPA*, Ngorongoro na Wanyamapori, kwa maana ya Idara kama inavyosimama kwa sasa. Kwa njia hii, Mamlaka itapata fursa nzuri ya kuratibu masuala mengi yanayoonekana kugongana sasa kwa sababu ya kuwa na mamlaka tofauti. Kwamba, mnyama anaweza kutoka kwenye Hifadhi ya *TANAPA*, huku hawa wanawaambia jamii msiwaue wanyama, akitoka kidogo anawindwa chini ya mamlaka nyingine. Nadhani huo ni upungufu, lazima tutazame kule tunakoenda, tunawezaje kuboresha uratibu ili masuala yote yanayowagusa wanyamapori yaweze kuratibiwa vizuri zaidi.

Kwa hiyo, mimi nitalifurahi huko mbele, hii mamlaka itakapopandishwa hadhi, badala ya kushughulikia Idara ya Wanyamapori kama ilivyo sasa, ikajumuisha hata na mamlaka nyingine hasa nikiongelea *TANAPA* na Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyamapori wanakabiliwa sana na changamoto nyingi sasa, kwa sababu kama wenzangu walivyosema, watu wanaongezeka na matumizi ya ardhi yanaongezeka. *Habitat* ya wanyamapori inazidi kupungua, lakini pia inazidi kudhoofika. Ningelipenda kuona kwamba, mkazo pia uwekwe kwenye *echo-system* kwa ujumla na *habitat* itakayosaidia wale wanyama nao kuweza kustawi. Uvunaji utafaulu tu endapo mkazo mkubwa utawekwa katika suala zima la yale mazingira, *echo-system* inayohitajika kuweza kuwahifadhi wale wanyama. Kwa hiyo, hili pia ningelishauri kwamba, Mheshimiwa Waziri ajaribu kulichukua, lakini pia kulipa uzito sana kwa sababu tusipochukua tahadhari mapema, tutaishia kuwa na maeneo yaliyozingirwa, ambayo mwishoni wanyama hawataweza kutoka wala kuingia na kidogo kidogo wale waliopo mle wataishia taratibu. Kuna haja ya kuwa na hiyo picha pana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala zima la *WMAs*; ni kweli kama wengine walivyosema kwamba, uvunaji wa wanyamapori umewaneemesha wageni zaidi. Kwa mujibu wa sheria hii inayopendekezwa, lakini pia kwa kanuni zitakazotungwa, ningalipenda kuona zaidi na zaidi wenyeji na nikimaanisha wenyeji kwa maana ya Utaifa, lakini jumuiya pia zile zinazoishi jirani na maeneo haya, wanufaike zaidi kuliko wanavyonufaika sasa. Hili ni muhimu, kwa sababu pamoja na kuongelea vikosi vitakavyohusika na ulinzi wa wanayamapori, bado walinzi wakubwa wa wanyama watakuwa ni watu wanaoishi katika maeneo yale, wawe ni wakulima wadogo wadogo, wafugaji wadogo wadogo, hawa ndio wahifadhi wakubwa na ni sharti tutambue nafasi yao katika hifadhi ya wanyama, katika matunzo ya wanyama na katika kuhakisha kwamba wanyama wale wanaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na kawaida ya kuwa na hofu mno juu ya hizi *WMAs*, kwa sababu utaratibu ukifuatwa, mamlaka itashuka kwenda ngazi ya chini. Kumekuwepo na kusita kuachia madaraka hayo yaende kwa watu walio karibu na wanyamapori. Hili ningaliomba Mheshimiwa Waziri, afalinyie kazi na kuhakikisha kwamba, *WMAs* badala tu ya kuwa na haya maeneo ama hizi *WMAs* chache kwa ajili ya majaribio, kuwa na nyingi zaidi kwa sababu hii ndio kesho ya hifadhi ya kweli ya wanyamapori. Hakuna sababu ya kuwa na hofu, vijiji vikisimamia vikafanya kazi ya uhifadhi, bado Serikali itapata mapato yake na ninadhani watapata mapato zaidi kuliko hata kiasi kinacholipwa na wawindaji wa sasa. Kwa hiyo, ni sharti uwindaji utazamwe kwa sura nyingine, lakini tuone zaidi na zaidi kwamba, hifadhi ya kweli ya wanyama itatoka zaidi kule chini, kati ya hawa watu wanaowatunza hao wanyama. Manufaa yakiwa bora kwao, watakuwa na kila sababu na moyo wa kuhakikisha kwamba, wale wanyama wanabaki kwa sababu ya manufaa yao kama jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kutazama ustawi wa wanyamapori ni lazima mkazo uwekwe kwamba ni wanyamapori pamoja na watu wanaoishi katika maeneo yale, si wanyamapori badala ya watu. Wazo la zamani kidogo la kwamba ili wanyama waweze kuhifadhiwa ni lazima kuwaondoa watu. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mapokeo yamekuwa kwamba kitu kinaanza na hadhi inasemekana inabadilika, lakini inabadilika kwa kubadilisha miliki ya maeneo yale, miliki ya rasilimali hiyo na kidogo kuanza kuwasukuma pembeni watu wambao wamekuwa wanaishi na kuwahifadhi hao wanyama kwa miaka mingi. Ninadhani picha yetu ibadilike, tuanze

kuona mkamilishano wa maana kati ya watu ambao wamekuwa wanaishi katika maeneo haya pamoja na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupendekeza kwamba, nimeona katika sehemu inayoongelea uwindaji wa wanyamapori, mkazo umewekwa zaidi katika uwindaji wa kitalii. Kumekuwepo na watu ambao kijadi wanawinda kupata kitoweo na aina ya uwindaji huo kama wanavyofanya wenzetu Wahadzabe ama Waakye si tishio kwa hifadhi ya wanyamapori, kwa sababu wanachukua kiasi kidogo wanachohitaji kwa ajili ya maisha yao na maisha ya familia zao. Ningelipenda kuona katika kanuni, baadaye uwindaji huu pia unapata nafasi, watu wapate kitoweo kwa sababu wamekuwa wakiishi hivi na bado hawakuwa tishio kwa wanyama kutoweka katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza kwamba, jambo hili lifanyiwe kazi ili uwindaji huu mdogomdogo nao upate nafasi katika sheria na katika kanuni ambazo zinapendekezwa kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu mdogo, nashukuru na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, kwa mchango wako. Msemaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo atakuwa Mheshimiwa Guido Sigonda.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho katika mjadala wa leo. Mimi nadhani umenifanya niwe wa mwisho kwa sababu umeshanitambua kila wakati ninapozungumza, huwa sina tabia ya kutafuta maneno pale ambapo wenzangu wamekwishazungumza. Nakushukuru sana na nitajitahidi ili nisivuke dakika zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Waziri wa Utalii, pamoja na kundi lake lote, kwa jinsi walivyoonesha kushirikiana na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo na nasema kwamba, yote ambayo yametolewa kwenye taarifa, mimi ninahusika na ninaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru Mheshimiwa Spika, kwa jinsi alivyofikiria kuiteua Kamati hii ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Alizingatia mambo yote muhimu, ambayo Mjumbe wa Kamati anapaswa kuwa nayo; kwa mfano, taaluma. Kamati hii ina wanataaluma waliobobea katika suala hili ambalo tunalizungumzia leo; tunao wanataaluma wa wanyama, mwanataaluma ambaye akimwona mnyama tu anajua yule mnyama anafikiria nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia *conservation* ni lazima umwelewe mnyama. Utajuaje hiyo tabia ya mnyama, kuna vipengele vya *animal ecology*. Vilevile lazima ujue kwamba, kuna mtu atakuja kumuwinda huyu mnyama *(human ecology)*. Ujue kabisa huyu mnyama ni lazima atapita katika mazingira tofauti, ndiyo tunakwenda

huko kwenye *soil ecology*. Yote hayo ni lazima uyafahamu na wanataaluma wamo katika hii Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalolizungumzia leo ni *management* ya hawa wanyama; sasa labda nisijisifie tu mimi ni mwanataaluma wa *animal ecology and management. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ufuzu ni lazima uende kwenye *management and implementation;* yote hayo ninayo. Siyo hayo tu ni lazima uwe na *knowledge* ya *Environmental Impact Assessment*, hawa wanyama kama unazungumzia suala la kuleta Muswada, utaona namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wataalamu wake, kwa kuzingatia yale yote ambayo Kamati iliyatoa. Wenzangu wamezungumzia karibu mambo yote yanayohusu Muswada huu, faida na hasara; mimi nitajitahidi sana kuzungumzia yale ambayo pengine hayakugusiwa. Bahati nzuri yale ambayo hayakugusiwa, nitayaainisha katika maeneo ambayo ninatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu utatusaidia sana hasa sisi ambao ni Wajumbe wa kutoka Kusini. Utakumbuka tumekuwa kila wakati tukijaribu kuishawishi Serikali, iangalie vivutio vilivyopo Kusini mwa nchi hii. Mimi nimekuwa nikisimama wakati mwingi tu nikijaribu kuonesha kwamba, Wilaya ya Chunya kuna vivutio ambavyo havionekani na hivi vyote ni kutokana na hali halisi tuliyonayo ya kutokuwa na miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa uwindaji wa kitalii, tunalo Pori la Lukwati, ambako bahati nzuri tuna mwekezaji mmoja yupo kule. Kitu ambacho ninataka nikisisitize hapa ni kwamba, huu Muswada ukishapitishwa hapa utatusaidia sana sisi kutangaza hali halisi ya kule ilivyo na nafikiri tutapata wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hayo yote yameshazungumzwa, niende kwenye hili suala ambalo limesisitizwa sana katika Muswada la kuwashirikisha Watanzania katika suala lote la wawindaji na zaidi kumiliki vile vitalu. Hili siyo suala la kulikimbilia ni suala ambalo linatakiwa kukaa. Ninawashukuru sana hawa watendaji kwa kufikiria kuwa na kipindi cha mpito, kwa mfano, unaosema *profession hunter*, anajifunza mambo mengi huyu mtu na anatakiwa ayajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mimi ni mtaalam wa kutumia bunduki ambayo naitumia kwa mnyama, kwa binadamu hata kwa kuku. Ukimchukua mtu ambaye anajua kwamba ana uwezo wa kuwekeza maturubai na kadhalika, hajui namna ya kuitumia bunduki, tutakuja kuuana sisi wenyewe binadamu. Ninajua kabisa kuna wawinaji wa asili wapo, lakini unapoingia kwenye *professionalism*, ipo tofauti kubwa sana. Kwa hiyo, kipindi cha mpito hiki ndicho ninashauri sana wale tutakaowapata, tujue wana taalama ya kutosha ambayo itawasaidia, siyo lazima ukasomee lakini ni lazima ujifunze. Ninataka nilisisitize hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limezungumzwa kidogo sana na nilikwishalizungumza kwenye mikutano iliyopita ni fidia kwa watu ambao wamejeruhiwa ambayo imesisitizwa kwenye Muswada. Suala hili linatia uchungu sana. Mkutano uliopita, nilizungumzia madhara ninayoyapata kule kwangu kutokana na mamba; hivi tunashindwa nini ikiwa tunasema kwamba ana haki ya kuishi na ndiyo maana tumeweka sheria za kumlinda binadamu anayedhuliwa na binadamu mwenzake; hawa wanaodhuriwa na wanyama, mtu ameuawa, ama amekatwa mguu, tunasema tumfidie; kuna wanyama wengine ni wazoefu kama walivyo binadamu, binadamu wengine ni wazoefu wa kufanya madhara na wanyama wengine ni wazoefu vilevile, mamba akishamla mtu hataacha kumfuata mtu; kwa nini tusifikie hatua kwamba yule mnyama ambaye anaonekana ni mzoefu, wananchi wa sehemu ile wachukue jukumu la kumuua? Mimi ninafikiri hilo nalo tulifikirie, kwa nini aendelee kuharibu na ameshakuwa mzoefu? *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine kama ndugu yangu mmoja alivyosema kwamba, hadi ukatoe ripoti itakuchukua siku moja na nusu; mtu ameshakatwa mguu huku na mnyama unamwona, unangojea ukatoe ripoti! Hilo naomba tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni ile hali ya Muswada itakavyonisaidia katika jimbo langu. Jimboni kwangu kuna mlima unaitwa Mlima Kwimba. Miaka iliyopita Mlima huu kulikwa na wanyama wengi sana, ukipanda juu utaona ni *plateau* ambayo inatunza wanyama wengi. Kutokana na sababu mbalimbali ambazo zimezungumzwa hapa za uharibifu wa mazingira, uwindaji, kilimo kisichokuwa endelevu na kadhalika, imefikia hatua wale wanyama wameanza kutoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa masika wale wanyama huwa wanakuja, msimu wa kiangazi wanakwenda kwa ndugu yangu Mheshimiwa Paul Kimiti, wanakimbilia Katavi. Ninashauri kwamba, kama Muswada ulivyozungumza, basi tuwe na maeneo ya kuhifadhi hao wanyama katika lile eneo, pengine kwa kuwaletea mazingira mazuri kama ya kuwawekea mabwawa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wafadhili ambao tayari wameshaonesha kwamba, wanaweza wakafanya hiyo kazi, nangojea Muswada ukishapita basi tumwone Waziri ili tujaribu pale mahali wanyama hawa waendelee kuwepo kwa nyakati zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, eneo langu lina *square kilometre* 17,000, nina gari moja la wanyamapori, watu wanashindwa kufanya kazi yao vyema. Wanakwenda mahali ambapo gari linaweza kufika kwa wakati ule lakini mwaka mzima unaweza kuona wametembea maeneo mawili tu. Ninashauri kwamba, Wizara ifikirie namna ya kuwawezesha wale wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki ni dhahiri kabisa hauwezi kumruhusu mchangiaji yeyote kuendelea na uchangiaji wa hoja hii. Nikubali tu kwamba, Waheshimiwa Wabunge, walioomba kuchangia hoja yetu ya leo, wataendelea na uchangiaji Siku ya Jumatatu kama nilivyokuwa nimetoa tangazo langu hapo awali.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niendelee kuwakumbusha kwamba, kesho saa tatu asubuhi tutakuwa na semina kwenye Ukumbi wetu wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, tuzingatie muda ili kuwa na ufanisi wa kutosha wa semina hiyo. Hapa mezani sina tangazo lingine lolote, ninawashukuruni nyote kwa ajili ya shughuli ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuahirisha shughuli zetu za Bunge mpaka Siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 2 Februari, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*